ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza /Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe.

18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/ Kuteuliwa na Rais.
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara,Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete

40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
56.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
57.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
58.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
59.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
60.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
61.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
62.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
66.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
67.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
68.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe

69.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
71.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
72.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao Cha Kumi na Saba - Tarehe 9 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizaraya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2014/15.

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Mwenyekiti naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2014/15.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 39

Umuhimu wa Matengenezo ya Barabara ya Jambiani Mfumbwi-Kibigija kwa Kuimarisha Sekta ya Utalii

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Barabara ya Jambiani Mfumbwi mpaka Kibigija ipo katika eneo muhimu la ukanda wa utalii ambao unasaidia sana kuongeza mapato ya Serikali. Barabara hiyo imejengwa kwa kiwango cha kifusi licha ya umuhimu wake katika eneo ilipo.

Je, kuna mpango gani wa Serikali kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami ili iweze kuhudumia kwa ufanisi wananchi na sekta ya utalii katika ukanda huo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 39 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Jambiani-Mfumbwi mpaka Kibigija ni barabara ya mchepuo inayokwenda sambamba na inayounganisha barabara kuu mpya ya Makunduchi-Paje hadi Jambiani. Barabara hiyo iliyokuwa ikitumika kabla ya kujengwa kwa barabara kuu hiyo iliachwa ili kutoa nafasi kwa Wawekezaji mbalimbali wa sekta ya utalii katika ukanda huo. Kwa kuwa barabara aliyoitaja Mhe. Mwakilishi haiko kwenye dhamana ya miundombinu, barabara kwenye maeneo hayo ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu, inamshauri awasiliane na Wizara ya Viwanda, Masoko na Utalii ili wamweleze mipango iliyokusudiwa ya matumizi ya maeneo inamopita barabara hiyo sambamba na mikakati ya uimarishaji wa Miundombinu ya barabara kwenye maeneo hayo ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, barabara ambayo anaizungumza pia inapita katika nyumba nyingi za vijiji, kwa hivyo kutokana na gharama kubwa ya ujenzi wa barabara hiyo wakati wa kufanyiwa *survey* ilionekana dhahiri kwamba haitowezekana kujengwa katika ile barabara ya mwanzo ya asili, na ikachukuliwa njia nyengine ambayo inapita katika maeneo hayo hayo ambayo Mjumbe ameyazungumza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kutoridhisha ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Niendelee kumpongeza Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutaka Mawaziri kujibu maswali kwa ufasaha na kwa manufaa ya wananchi, na Serikali kama Wizara ya Miundombinu majibu

ya Wizara leo Waziri ananiambia tokea lini Wizara ya Biashara na Viwanda imekuwa inajenga barabara, kama ulikuwa huwezi kujibu Mhe. Waziri, hili swali ungenijibu nikupe muda au vipi, leo unaniambia Wizara ya Biashara na Viwanda inajenga barabara. Mbona unalipotosha Baraza Mhe. Waziri.

La pili, kwa kuwa Wizara haina majibu, imeshindwa vipi muda mrefu kuwasiliana na Mamlaka husika kuhusu barabara hii iliyojengwa ili kuondoa kero za wananchi.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, Mjumbe hataki kufahamu. Nilivyojibu mimi ni kwamba barabara inayopita katika maeneo hayo hiyo ambayo anaitaja yeye ilikuwepo zamani, lakini kutokana na masharti ya ujenzi wa barabara haikutimiza masharti imepita chini ya nyumba nyingi za watu, na ingekuwa ni gharama kubwa ya ujenzi wa barabara hiyo.

Lakini la pili ni kwamba iko karibu sana na bahari; chini ya mita 500 karibu na bahari. Kwa hivyo kutokana na *survey* iliyofanywa katika kupita maeneo hayo hayo ya Jambiani - Paje - Makunduchi imejengwa barabara nyengine mpya, kwa hivyo ile ni barabara iliyoachwa kutokana na kwamba haikutimiza masharti ya ujenzi wa barabara, na ingekuwa ni barabara yenye gharama kubwa kutokana na kwamba imepita chini ya nyumba za watu. Kwa hivyo ni barabara ambayo inaachiwa ili wawekezaji au sehemu za utalii waitumie lakini sio barabara kuu kama ambavyo inatakiwa na Serikali.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ukurasa wa 27 kifungu No. 37 "Waziri au Mjumbe yeyote anayeuliza suali ambalo ana madaraka nalo, atakuwa na wajibu wa kujibu suali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba suala aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Waziri nafikiri hii barabara hujaijua, naomba tupange siku twende mimi na wewe ukaione hiyo barabara, maana yake nimeuliza maswali hamwendi kufanya utafiti kwanza halafu mnakuja kujibu mnavyotaka nyinyi humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa umeuliza sawa nimekufahamu ahsante. Mhe. Waziri umepokea hili.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa barabara mimi naijua, na hizi zipo nyingi hata sisi Pemba kule ilipojengwa barabara ya Ole/Konde ziko barabara zilizobaki lakini sasa sio barabara tena wala hazimo tena katika mpango kwa sababu ikija *survey* mpya ikapita barabara zile zilizobakishwa zile huwa tena sio za Mawasiliano ni njia tu zilizobaki lakini sio barabara za Mawasiliano, hapa kumepita *survey* mpya ikaachwa ile ambayo ilikuwepo asili, kwa sababu ya vigezo vipya vya ujenzi wa barabara. Sasa sio kweli kwamba mimi sijui wala hatuna haja ya kwenda, akitaka twende *ahlan wasahlan* tutafika Muyuni lakini sio tatizo kwenda.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b) kama ifutavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri amesema kwamba sababu kubwa ambayo imesababisha barabara hii ya asili iachwe ni kutokana na idadi kubwa ya makaazi ya watu ambayo yangesababisha gharama kubwa, lakini anasahau kwamba SMZ hivi sasa imeleta dhana ya utalii kwa wote, sasa ili tuweze kufikia utalii kwa wote maana yake ni kujenga miundombinu iliyo karibu na sekta ya utalii pamoja na makaazi ya watu. Je, haoni kwamba kufanya hivi kuacha barabara ile ikiwa sio kiwango cha sasa, haoni kwamba ile dhana ya SMZ ikiwa yeye ni Mjumbe wa Baraza la Mapinduzi anaipotosha.

Lakini jengine mwaka jana Baraza lako Tukufu lilipitisha sheria ya hifadhi ya barabara, kuna sababu gani ya kutolipa fidia wananchi wale ili kuimarisha miundombinu ya barabara.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mheshimiwa barabara ile haiwezekani sisi kuijenga, kwa sababu nilizozijenga lakini haizuii uwezekano wa kufika katika maeneo kwa sababu Wizara yetu ina utaratibu wa kujenga *feeder roads*, na huo utaratibu upo zinazounganisha barabara kuu niliyoisema ya Paje, Jambiani na Makunduchi na maeneo ya utalii, lakini sio kuijenga barabara ile hizi zitakuwa ni *feeder road* zinazotoka kwenye barabara kuu ya Paje, Jambiani na Makunduchi na kuelekea huko katika maeneo ya utalii. Na ukijenga barabara hizi kila mmoja atafika tena kwa wakati, na sio lazima

kuishughulikia barabara hiyo ambayo ina vikwazo vingi na havitoshelezi masharti ya ujenzi wa barabara.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri wa Mawasiliano na Miundombinu Mhe. Rashid Seif Suleiman naomba niulize swali dogo tu la nyongeza kama ifuatavyo.

Kwa kuwa mtandao wa barabara Mhe. Spika, ni muhimu sana katika kuimarisha uchumi wa nchi, na kwa kuwa barabara hii ya Jambiani/ Mfumbwi ni muhimu sana sio tu katika sekta ya kuimarisha utalii wa nchi pekee, lakini ni muhimu hata kuwaunganisha wavuvi kutoka Makunduchi, wakulima wa viazi na majimbi kutoka kule na kuyaleta huku mjini kwa ajili ya futari kesho kutwa ambapo Ramadhani imekaribia.

Je, kuendelea kung'angania tu kwamba barabara hii isijengwe mara ya mwanzo Mhe. Waziri katwambia kwa sababu ya nyumba za watu ni nyingi, lakini akumbuke kwamba barabara ya Ole/Konde ilipoteza majumba mazuri ya kifahari ikiwemo ya kwangu vile vile na tumepewa sehemu nyengine ya kujenga. Je isingekuwa vyema katika kuimarisha uchumi wa nchi hii pamoja na utalii na wavuvi wale wa Makunduchi, Mfumbwi na maeneo ya kule Kibigija ikajengwa hii, ili wakapata urahisi wa kuleta samaki wao, majimbi yao vizuri hapa mjini na sisi walaji tukatumia.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema katika majibu yangu kwamba barabara hii mpya ya Jambiani, Paje, Makunduchi ilijengwa barabara mbadala ya ile ambayo imepita katika majumba na iko karibu na bahari, lakini hao wakulima na wavuvi ambao anawataja nishawazungumza mimi kwamba barabara ambazo zitaunganisha barabara kuu na hayo maeneo ambayo ameyataja na mengineyo ni *feeder roads* ambazo zimo katika mpango wa ujenzi wa wizara, lakini sio barabara hiyo inayotajwa.

Vile vile namuomba Mhe. Mjumbe na wengine wote warudie sheria tuliyokuja tukaipitisha hapa kwa kuifanyia marekebisho. Aina za barabara zinazojengwa na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano zimetajwa barabara za mikoa, wilaya na nyenginezo. Kwa hivyo wazipitie, sio kila barabara itajengwa na wizara hii, kuna barabara maalum.

Kwa mfano, kama Mhe. Jaku Hashim Ayoub na Mhe. Saleh Nassor Juma wamejenga kasri yao halafu wanataka barabara haihusiani na wizara, wajenge barabara yao kwenye makasri yao. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru ahsante.

Nam. 9

Kutofuatwa Matakwa ya Sheria Juu ya Upakizi wa Abiria Melini

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:

Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano ilisema meli yoyote inaruhusiwa kupakia abiria kulingana na muundo wake asilia, lakini meli ya *Sea Link* imekuwa ikiruhusiwa kuongeza idadi kwa awamu 3 tofauti kinyume na kauli ya Waziri aliyoitoa ndani ya Baraza mwaka jana.

(a) Kwa nini meli hiyo ambayo kwa uhalisia wake huchukua abiria 700, iruhusiwe kuchukua hadi abiria 1,000 baadaye 1,200 na hadi hivi karibuni imeongezwa hadi kufikia abiria 1,440.

(b) Kwa kuwa Waziri aliahidi kulinda Sheria ya Usafiri Baharini ndani ya Baraza hili Tukufu, kwa nini Sheria zinavunjwa na yeye yupo.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Meli ya *Azam Sealink* iliomba kupewa kiwango cha kuchukua abiria 1,500, mwanzo iliruhusiwa kupakia idadi ya abiria kulingana na muundo wake na idadi ya viti vilivyomo na nyaraka zake za kubeba abiria 1,500. Lakini mara baada ya kusajiliwa kwa meli hii hapa Zanzibar kutokana na

kuzingatiwa kuwa muundo wa meli hiyo ni aina ya *"RO-RO"* na aina hii ni wa mara ya kwanza kwa hapa Zanzibar, hivyo ikawa inaongezewa abiria hao kwa awamu.

Awamu ya kwanza meli hii iliruhusiwa kuchukua abiria 700, awamu ya pili ikaongezewa kuchukua abiria 1,200 na awamu ya tatu ambayo ni ya mwisho ikaongezewa kuchukua hadi abiria 1,440. Kutokana na ukaguzi wa sehemu za kukaa kila abiria atakuwa na kiti chake, hakuna ambaye atakaa chini isipokuwa kwa kutaka yeye mwenyewe kutandika mkeka wake, lakini kiti chake kipo. Kwa hivyo, abiria wote hawa wana viti vyao ambavyo wizara kupitia Mamlaka ya Usafiri Baharini (*ZMA*) wamekwenda kuvihesabu na kujua hasa kwamba abiria walioruhusiwa kila mmoja ana kiti chake cha kukaa. Hivyo, tumeweka nafasi ya akiba ya abiria 60 ili kuweza kupisha msongamano ambao ungetokea. Kiwango cha juu kabisa ambacho cha kuchukua meli hii kilichoombwa ni 1500. Nakushukuru.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana Mhe. Waziri kwa kutuelimisha zaidi na kukubaliana na takwimu ambayo nimeitoa kwenye swali langu, lakini pamoja na majibu yake mazuri naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mhe. Mwenyekiti, meli imetengenezwa uhalisia wake ikiruhusiwa kuchukua abiria 700 kama ambavyo Mhe. Waziri amekiri, na hayo Waheshimiwa Wajumbe ukiangalia kwenye mtandao kuwa IMO watakuonesha kuwa asili ya meli hii ni kuchukua abiria 700 kama Mhe. Waziri ambavyo amekiri, na ili ufanye marekebisho lazima upate kibali cha IMO. Sasa Mhe. Waziri atakumbuka kwamba mwaka juzi Baraza hili ile sheria ya kulinda uhalisia wa meli.

(a) Ni kwa nini wameruhusu kuongeza abiria 700 mpaka 1440 wakati uhalisia wa meli hii ni kuchukua abiria 700 kwa mujibu wa IMO.

(b) Ikiwa Mhe. Waziri hayo atayapinga atakuwa tayari Mhe. Waziri kutuletea usajili wa meli; IMO unaonesha kwamba wamekiuka utaratibu huo na kwamba sheria ya ZMA Zanzibar wameikiuka na kwa msingi huo Baraza hili la Wawakilishi wamepinga maagizo yetu, na kwa msingi huo atakuwa tayari kujiuzulu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimwambie kwamba katika kipindi ambacho meli hii iliingia ilikuwa ni mara baada ya ajali ya MV. Skgit. Kwa hivyo katika kipindi kile kulikuwa na marekebisho makubwa ambayo yalifanywa katika sheria ya ZMA; na moja katika jambo ambalo lilifanywa katika utaratibu wa kazi za ZMA ni vyombo vyote sio hiyo tu, vyombo vyote vilikaguliwa upya ikiwemo MV Maendeleo ambayo ni meli ya serikali, vilikaguliwa upya na kufanyiwa *test* inayoitwa *stability test* ili kujua uwezo wake wa kuchukua abiria.

Kipindi hicho hicho MV Serengeti ilishushwa kutoka abiria 600 mpaka 350 mpaka watakapofanya marekebisho yanayotakiwa. Kwa hivyo kipindi hicho kilikuwa ni kipindi cha kuibadilisha hali ya usafiri wote wa Zanzibar kulingana na usalama wa vyombo.

Baada ya kutokea kipindi hicho tulipoendelea vyombo vikapewa muda vijisahihishe na vikapimwa, kwa hivyo sio hii tu ndio iliyopewa abiria wa ziada. MV Serengeti baadae tulirekebisha akaongezwa kutoka 350 mpaka 600 kama ambavyo kawaida yake, na MV Maendeleo ilipewa kutoka abiria 450 mpaka 600 kama ambavyo waliomba kutokana na nafasi iliyomo baada ya kukaguliwa.

Kwa hivyo hakuna cha ziada chochote kilichofanywa *special* kwa hii, isipokuwa ni taratibu ambazo zilibadilika kulingana na tokeo lile lililofanywa. Na hii meli hii kutokana na upya kama ilivyozunguzwa mwanzo wa mtindo wake, mwanzo ilipokuja humu ndani ya Baraza ilizungumzwa kama ni *LCT*, *Landcraft* ambao *landcraft* chini ni bapa kabisa inaweza hata kukaa juu ya mchanga, lakini baada ya kukaguliwa na watu kuiona kweli sio *landcraft* haiwezi meli ile kukaa juu ya mchanga lazima ipate maji ya kina fulani ndio iweze kukaa, kwa hivyo ina tofauti na *landcraft*.

Hata rafiki yangu mpenzi hapa Mwenyekiti wangu wa mwanzo Mhe. Mshimba alikuwa na fikra hiyo hiyo kwamba ile ni *landcraft*. Kwa hivyo huu utaratibu wa uongezaji wa abiria haukufanywa kwa upendeleo, ulifanywa kutokana na taratibu mpya za kuziangalia meli *stability* yake wakati zikienda baharini.

Muongozo

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti natumia kanuni ya 37 ili nipate majibu sahihi, na naomba nimwambie Mhe. Waziri kwa kutumia kanuni hii kwamba anapozungumza *stability* maana yake anazungumza uwezo wa meli.

Original stability ya meli ile tangu ilipotengenezwa ni abiria 700, na kwa mujibu wa kibali cha IMO *stability* ipi mpya ambayo imekuja baada ya uwezo huo. Atwambie tu kwamba ameongeza viti na kwa msingi ambao wanaojua wao lakini sio *stability*, *stability* ya meli ile ni abiria 700, *stability* nyengine ipi ambayo anatwambia hapa.

Mhe. Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, haya mambo yana utaalamu wake, kwa hivyo mimi naomba nimjibu kwa maandishi nini maana ya *stability*, na hizo za IMO anazozitaka zote zitakuja kwa maandishi. Kwa sababu tukishindana mimi sijui kitu kuhusu mambo hayo na yeye ni hivyo hivyo. Sasa tukishindana itakuwa hatufikii pahali.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa hii miongozo hata Mhe. Waziri hajamaliza, tumwache kwanza ajibu halafu utaleta muongozo wako. Mwache Mhe. Waziri amalize.

Mhe. Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Ndio nasema Mhe. Mwenyekiti, haya mambo ya kitaalamu lazima wale wataalamu waandike kwa viwango vyao, nikisema mimi maneno yatakuwa hayajawatosheleza kwa sababu ni mambo ya kitaalamu.

Sasa tumletee zile *terminology* za kitaalamu zilizotumika nini maana ya *stability,* inapimwa vipi na ile ina uwezo gani, *tonnage* yake, na *stability* yake kutulia katika bahari. Ile meli Mhe. Mwenyekiti, ina urefu wa mita 99. Sasa sisi kuja kuzungumza tu hapa maneno itakuwa haitoshelezi, ndio nikasema Mhe. Mjumbe astahamili nimletee kwa maandishi. Mambo yote ambayo ameyataka kwa sababu yeye kataja mambo ya IMO, sasa hapa tuna *dictionary* hapa la IMO, lazima tumletee kwa maandishi aliyoyataka. Sasa hawezi kustahamili nikamletea kwa maandishi? Ninamuomba Mhe. Mjumbe aweze kupokea hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli sisi humu wengi si ma-*engineer*, mimi nina sehemu ndogo ya u-*engineer* kwa sababu nimepita Mbweni pale na fani ndio hiyo *mechanical engineering* lakini si mtaalamu wa meli, lakini Mwakilishi aliye makini anatakiwa asome na ajifunze.

Nimepewa *reference* kwenye IMO na naelewa nini maana ya *stability*, yeye mwalimu wangu wa chemistry Fidelcastro. Sasa atwambie tu kwamba suala la *stability* wamelikiuka, na kwa hivyo walitoa vigezo gani kuipa meli ile ya abiria 1450. Yeye mwalimu wangu wa *chemistry* anajua maana ya *stability* nini, akitwambia hajui na kwamba humu si wataalamu basi kamati yako sasa ikiwa wewe ndie Mwenyekiti wa Kamati ya Miunduombinu twende tukaangalie, wamekiuka utaratibu wa usajili wa meli kwa kukiuka hata *stability* ambayo wanaijua.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mhe. Mjumbe Mhe. Waziri amelisikia hilo, na sisi tutalifanyia kazi kama zilivyo taratibu zinavyoturuhusu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha kufika siku hii ya leo katika hali ya uzima na afya. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Waziri kajibu maswali kivaga ubaga, ameeleza mambo mengine ambayo siyo suala mama lilivyoulizwa. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba ni kutufunika macho sisi Waheshimiwa humu.

Pili Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali mama kasema kwamba sheria zimebadilishwa, hajui kama kakiuka, wakati wa kutunga sheria ni sisi na wa kubadilisha ni sisi, ataliambiaje hili Baraza lako Tukufu.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, mimi nilichofanya ni kuwafunua macho na sio kuwaziba macho. Kwa hivyo nilivyoeleza utaratibu uliopita kwa meli nyengine ili Wawakilishi waweze kufahamu kwamba taratibu hizi zinapita kwa meli zote na boti ambazo zinasafiri katika bahari yetu zilizosajiliwa na ZMA.

Lakini swali la pili Mheshimiwa haya mabadiliko tunayoyazungumza yamepitishwa hapa mabadiliko ya sheria ya ZMA yamepitishwa hapa hapa. Mhe. Bi. Asha Bakari naomba unisikilize kidogo swali lako nikujibu.

Utaratibu

Mhe. Asha Bakari Makame: Tulipitisha sheria hapa ya mabadiliko lakini katika jibu lake mama kasema kwamba na wao wamebadilisha ndio alivyosema *hansard* ipo. Sasa wamebadilishaje, wakati wa kubadilisha ni sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Asibabaishe hapa!

Mhe. Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Mhe. mabadiliko yalifanywa na Wizara yakapitishwa na Baraza la Wawakilishi, kwa hivyo nilivyosema sisi tulibadilisha ina maana nilikusudia ile *initiative;* kile chanzo cha mwanzo kilitoka kwenye Wizara yetu ndio ikabadilika ile sheria.
Sasa na Baraza la Wawakilishi ndio lililopitisha hatukuleta kitu kipya. Kile kile kilichopitishwa kwenye Baraza hapa ndicho tulichokitumia.

Mhe. Makame Mshimba: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini naomba nitoe kijisentensi kidogo tu. Mwaka uliopita mimi nilisema katika bajeti ya Wizara hii na nilitoa tahadhari mapema kabla chombo hakijaingia nchini, na nikakionesha hapa nikatoa *full document*. Chombo kile cha masafa mafupi, ambalo kwa jina jengine linaitwa pantoni, na ndio maana *model* yake iko pantoni sio *landcraft* kama alivyoeleza Mhe. Waziri. Je, Mhe. Waziri huoni kuwa leo Baraza hili umetudanganya kiasi kikubwa sana.

La pili, Mheshimiwa kutokana na uundaji wa vyombo nani muhusika zaidi, IMO au muundaji ndiye mwenye *capacity* ya kujaza watu.

Mhe. Waziri wa Miundumbinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, hivi vyombo duniani vya aina hiyo ya IMO viko vingi sana, kwa hivyo kuna sheria zinazoambatana na za kimataifa lakini kuna sheria ambazo zinaambatana na nchi wenyewe. Kwa mfano vyombo vya baharini Shirika lake ni (*IMO) International Maritime Organization*, lakini vyombo vya anga Shirika lake ni ICAO *International Civil Aviation Organization.* Lakini humu ndani ya nchi kwa Zanzibar upande wa baharini tuna ZMA na upande wa Bara kuna SUMATRA na vya anga tuna Jumuiya hapa au *Organization* inaitwa TCAA *Tanzania Civil Aviation Authority.*

Sasa hizi kwa mujibu wa sheria za ulimwengu zina uwezo wa kuunda sheria zao kutokana na vyombo vinavyo-*operate* ndani ya nchi. Ushahidi ninao wala Wawakilishi wasifanye nini hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mwezi huu uliopita tulipata ziara hapa ya Katibu Mkuu wa ICAO yaani Jumuiya ya *Civil Aviation* ya ulimwengu, mambo ya anga. Mimi nikamuuliza yule kuhusu ndege ndogo ndogo hizi na taratibu zake akanambia sheria zake zipo katika vyombo vya ndani ya nchi yaani *regional organization* au *authority* zilizomo ndani ya nchi. Sasa si kila kitu kitazungumzwa na IMO, si kila kitu kitazungumzwa na ICAO, si kila kitu kitazunguzwa na jumuiya zile za ulimwengu. Wale wanataja mambo yao lakini jumuiya za kikanda zina taratibu za kuweka sheria zao.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti swali nililoliuliza na swali alivyonijibu Mhe. Waziri ni vitu tofauti. Mimi nilitaka nijue tu nani mwenye sheria baina ya muundaji wa kujua idadi ya watu au mwenye kutunga sheria IMO au nani, basi *simple case*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe pamoja na Wajumbe wengine mliokuwepo hapa hili suala liliulizwa na muulizaji wa swali tokea mwanzo, na Mhe. Waziri alikwishatoa maelezo kwamba atajibu kwa maandishi. Naomba mumpe nafasi Mhe. Waziri ili akafanye *consultation* na watu wake baadae aje kuleta jawabu ambalo litakidhi haja, ninawaombeni sana Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, kunakuwa na maswali ya nyongeza mimi nimeuliza *difference* na swali la yule aliyeuliza mwanzo. Kwa maana hiyo kwa mantiki haiwezekani kuwa swali ambalo lililokuwa ajibiwe yule liwe *correction* na mimi, *no,* hiyo haiwezekani. Mimi nilichomuuliza *simple* tu kwa sababu IMO inatunga sheria jinsi gani ya uendeshaji wa vile vyombo, lakini kuna muundaji ambaye ndiye mwenye kujua *capacity* ya meli hii itachukua watu wangapi, nilitaka nijue nani ni mwenye sheria zaidi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe swali lako halina tofauti kabisa na swali ambalo Mhe. Hija ameliuliza, na Mhe. Waziri amekwisha kusema kwamba atajibu kwa maandishi. Naomba tumpe nafasi Mhe. Waziri alete majibu kwa maandishi ili sote tuneemeke. Ahsante sana.

Nam. 68

Wajibu wa Viongozi wa Wizara ya Afya Kutembelea Vituo vya Afya

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Tangu mwaka 2010 hadi mwaka 2014 Waziri wa Afya, Naibu Waziri wa Afya wamekuwa hawatembelei vituo vya Afya kwa kusikiliza shida za vituo vya Afya, ili wapate kujua changamoto za ukosefu wa madaktari na kadhalika.

(a) Je, kwa nini viongozi nao hawafanyi angalau mwezi mara moja kutembelea vituo vya Afya ili kujua kilio cha wananchi wanyonge wanaopata huduma katika vituo hivyo.

(b) Je, mnawaeleza nini wananchi kwa kutofanya hivyo, hamjui wajibu au kufanya hivyo sio wajibu wenu.

(c) Je, ni vituo vya Afya vingapi vyenye matatizo ya ukosefu wa vifaa pamoja na dawa.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim swali lake Namba. 68 (a), (b) na (c) kma ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kwa heshima zenu mnapotoa maswali, muchukue hadhari ya kupata taarifa za kutosha juu ya yale mambo unayoyauliza. Sina hakika kama Mhe. Mwakilishi anachokisema kwamba hatujatembelea vituo hivyo tangu mwaka 2010 kuwa ni sahihi, sina hakika, lakini ninawajibika kujibu kwa sababu ni swali ambalo lina heshima ya kujibiwa.

Kwa taarifa ya Mhe. Waziri na Naibu Waziri wake mara tu baada ya kuapishwa huwa tunapewa hadidu rejea ya kazi zetu ambazo hutakiwa kuzitekeleza wakati tukiwa katika ofisi zetu.

Ninavyoamini mimi tunajitahidi kutekeleza kazi zetu kama vile tulivyopewa maagizo na Rais. Ni vizuri ikaeleweka kwamba katika Wizara ya Afya kuna watendaji ambao wanaanzia ngazi za juu mpaka kwenye kituo kidogo cha afya. Ukiacha ngazi ya utawala wa Wizara kwa jumla, kuna Kamati Tendaji chenye vikao kila mwezi na kuna kawaida kila Jumatatu, Waziri au akiwa hayupo Naibu wake huwa anakutana na watendaji yaani ni kikao cha *briefing*, na pia kuna Kamati ya Uongozi ambayo huwa tunakutana kila mwezi au baada ya miezi miwili mpaka mitatu, na kwenye hospitali zetu na idara huwa tunafanya hivyo hivyo.

Bahati nzuri kuna Mkurugenzi wa Tiba ambaye ni daktari, kuna Mkurugenzi wa Kinga ambaye ni Daktari na Mkurugenzi wa Mnazi Mmoja Hospitali ambaye pia naye ni mtaalamu wa mambo ya kaputi. Chini ya Utawala huo kuna mfumo ambao nadhani ni wa pekee kwa wizara za serikali unaitwa mfumo wa kanda (*zonal and district committees*) kila Mkoa na Wilaya Unguja na Pemba.

Ngazi inayofuata baada ya *zone* kuna Kamati za Wilaya 10 ambazo huwa zinasimamia shughuli za utendaji wa afya siku hadi siku, hao niliowataja ndiyo wanaohusika na kazi za kila siku za utawala na mahospitali na vituo, na hivi sasa tunakamilisha mfumo kufikia dhamana ya mambo ya afya kuzipeleka kwenye kijiji ambao tunaita *community health strategies.* Kwa hivyo, mfumo wa Wizara ya Afya umeanza juu mpaka chini

a. Kwa nyadhifa hizo zilizotajwa na Mhe. Mwakilishi, viongozi hao huwa wanakwenda vituoni au hospitali kukiwa na jambo kubwa la Kitaifa, kwa ufunguzi au kwa haja maalum. Hakuna kokote katika ulimwengu huu ambao kila wakati Waziri anatakiwa awe vituoni.

Lakini Mheshimiwa katika utaratibu wa kugawana madaraka mimi na mwenzangu Naibu Waziri kwa sababu yeye ni daktari anashughulikia na dhamana nilizompangia ikiwemo hiyo ya kusimamia vituo na hospitali kwa mambo ya kitaalamu, na mimi kusimamia mambo ya jumla pamoja na mambo ya uongozi na utawala ambao ndiyo fani vile vile niliyoisomea.

Katika hali hiyo Mhe. Spika, Naibu Waziri wa Afya na Waziri wake mwaka wa kwanza tulitembelea hospitali zote na vituo vyote, na bahati nzuri Naibu wangu aliendelea akafika kwenye vituo mpaka vile ambavyo haviwahi kufikwa na mtu yeyote isipokuwa na Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na Naibu wangu. Na hiyo ameshafanya mara mbili tena kwa uangalifu, kukaa, kuzungumza na wafanyakazi na kujua matatizo yao.

Mhe. Mwenyekiti, Naibu Waziri alipotembelea vituoni kuna wafanyakazi wa zamani ambao baadhi yao hivi sasa wameshastaafu, walimtaarifu kwamba tangu waanze kazi mtu aliyewahi kufanya ziara kama hiyo vituoni ni Dr Ali Mohamed Shein, na yeye wa pili. Kama Wizara tulifarijika kuona kwamba Mhe. Rais wetu alipokuwa na yeye Waziri wa Afya au Naibu alifanya hivyo kama tunavyofanya sisi.Wizara inaona fakhari kwa hilo tuna wasaidizi wetu wa *DANIDA* huwa wanatusaidia visenti, na kama mnavyojua juzi mmetujadili hapa kwamba tuna vipesa vichache kufanya shughuli hizo, lakini Wizara inaamini kabla kipindi hiki kumalizika, na kwa kazi tuliyoifanya kwa miaka hii mitatu iliyopita tutafanya tena ziara za pamoja kwenda kujipima lile ambalo tumefanikiwa na lile ambalo limetushinda.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Afya sina hakika na waziri wenzangu lakini Wizara ya Afya ni pekee yenye Kamati Maalum inayosimamia ugawaji wa wafanyakazi (*deployment committees*) na kabla hawajafanya kazi wafanyakazi hawajagaiwa popote, tunahakikisha kwamba wakuu wote wa vituo na hospitali wanakaa pamoja chini ya Mwenyekiti wa Naibu Waziri kujadili jinsi ya kuwagawa wafanyakazi waliokuwepo sasa na upungufu wa kila mahali.

b) Kwa upande wa madaktari na wafanyakazi wengine hilo limeshasimamiwa na wafanyakazi wanapangwa Unguja na Pemba tena kwa mahitaji yaliyopo. Wizara imetengeneza kitengo cha taarifa ya nguvu kazi (*Human Resource Information System*) ambapo wafanyakazi wote wa Wizara ya Afya wamesajiliwa. Pia wizara ina mpango wa miaka mitano wa kusomesha wafanyakazi, na kwa sasa mengine nitakuja kueleza pale ninapojibu hoja zetu tunajua upungufu wa kila hospitali, wa kila kituo na upungufu wa mfanyakazi gani anahitajika, na yupi angepasa kupatikana.

Kuhusu (c) vituo vya afya vyote vinaomba vifaa na dawa kwa mujibu wa mahitaji yao baada ya kubadilisha mfumo wa kuomba unachotoka badala ya ule wa kuletewa tulichonacho (*pull system* mpaka *push system*). *Push system* ilikuwa zamani, sasa kuna *pull* ambao wao wenyewe wanatwambia. Kwa hivyo, tunafanya kazi hizo katika mfumo wa kujua uhaba wa kila aina ya shughuli za vituo.

Uhaba wa madawa nimeueleza kwa urefu wakati nikijadili hotuba yangu ya bajeti, na sababu za uhaba huo zinafahamika na pale nitakapokuja kutoa maelezo ya majumuisho nitaeleza zaidi. Kwa miaka mitatu sasa wizara yetu imebadilisha hata mfumo wa uagizaji wa dawa. Moja katika tatizo ambalo lilikuwa linaleta usumbufu sana wa upungufu wa dawa, tunategemea matokeo ya mfumo huo utazidi kuwa mzuri baada ya matatizo ya fedha kupungua. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama suala ni kutembelea vituo tunatembelea hospitali tunajua matatizo yalivyo, kama ni suala la kutembelea kituo maalum inawezekana kuna baadhi ya vituo hatujafika. Mhe. Mwenyekiti, Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya rafiki yangu Mhe. Waziri kuwa hayana afya kama wizara yake wala kiwango, naomba nimuulize maswali madogo sana ya nyongeza.

Kwanza nimuombe aondoshe kauli yake ya kusema Wawakilishi tunauliza jambo ambalo hatuna uhakika nalo, yuko tayari kupokea risiti kama ni ushahidi wa Kidongo Chekundu kabla ya bajeti yake juzi na hivi sasa kumpa ushahidi wa stakabadhi ya bili ya umeme, watu walivyoendelea kukaa kiza siku mbili. Sisi hatuulizi swali hasa Wizara ya Afya, siulizi swali nikabahatisha, yuko tayari kupokea stakabadhi hii. Mimi ninachouliza huwa nina uhakika nacho, kwanza aombe radhi kwa kauli yake au aondeshe kauli yake, aliposema kwamba tunauliza swali kuwa hatuna uhakika nalo.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, ninachosema hana uhakika kwamba kwa miaka mitatu iliyopita hatujatembelea vituo Unguja na Pemba, na ndiyo maana nikasema afanye *research*, vituo vya Unguja na Pemba tumetembelea vyote. Naibu wangu amefika *stage* kufika katika vituo vyote mara mbili na huo ni utaratibu wa kugawana kazi katika wizara.

Kama sijatembelea kituo maalum hilo nalikubali lakini kama suala la kutembelea vituo, na bahati mbaya sisi wengine hatuna televisheni kama kila tunapokwenda tujulikane kwamba sasa tumetembelea kituo, lakini kama ni kutembelea vituo na mahospitali kazi hiyo tumeifanya, na ndiyo maana nikasema kwamba kwa suala hilo anahitaji kujitafutia zaidi, hospitali zote tumetembelea si mara moja wala si mara mbili. Kama ni kituo maalum kutembelewa hilo sikatai, kwa hiyo sina sababu ya kuomba radhi ili nionekane kwamba hatujatembelea sisi hospitali.

Mhe. Mwenyekiti, suala la kukatika umeme wa Kidongo Chekundu si Kidongo Chekundu tu umeme ulipokatika, umekatwa hata Mnazi Mmoja, na kwa sababu madeni yote ya tangu Juma Duni hajazaliwa; ya miaka yote nyuma tumeambiwa tuyalipe na uwezo wa kuyalipa wakati mmoja hatuna, na ndiyo kuna mpango maalum wa kulipa madeni hayo.

Kwa hiyo, kukatiwa umeme na kuniletea risiti najua sana umeme umekatwa Makao Makuu ya wizara, umeme umekatwa hospitali ya Mnazi Mmoja, umeme umekatwa Wete, umeme umekatwa kwenye vituo vyote, lakini madeni yote hayo ni madeni ya miaka ya nyuma ambayo yamekusanyika kwa pamoja na tumeagizwa tuyalipe kidogo kidogo.

Kwa hiyo, bila shaka anaweza akawa na risiti, na juzi alisema hapa kwamba na Kindongo Chekundu hospitali wendawazimu umeme umekatwa. Ni kweli umekatwa mote lakini mmeeleza juzi hapa kwamba fedha tunazopewa ni ndogo, tulipe madeni tukose huduma au tulipe madeni kidogo kidogo na huduma ziendelee. Mhe. Mwenyekiti, nakubali umeme umekatwa Kindongo Chekundu, lakini namwambia na Mnazi Mmoja pia ulitaka kukatwa mpaka tukatoa taarifa Ikulu ndiyo ukazuiwa kukatwa. Tumefanya mpango sisi na Wizara ya Ardhi na Maji kwamba madeni haya tuyalipe kidogo kidogo, kila penye uwezo wa kulipa tunalipa. Sasa kama umekatwa Kidongo Chekundu namuarifu na Makao Makuu umekatwa na hospitali ya Mnazi Mmoja pia umekatwa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kituo cha Afya cha Kangani, Makoongwe na Chambani ni vituo ambavyo hutoa huduma ya jamii pamoja na mama na watoto.

Je, Mhe. Waziri ni lini vituo hivi utavitembelea ili kuondosha matatizo waliyonayo wanawake na wanaume wa hospitali hizo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, lini nitavitembelea, bila shaka mpaka tumalize bajeti, lakini suala sikuvitembelea, suala ni kwamba nikifika nikisikia matatizo ambayo ni sawa visiwa vyote viwili ni vya kupatia ufumbuzi. Kwa hivyo, naweza nikatembelea nikaambiwa hakuna dawa, nikaenda kwengine nikaambiwa hakuna dawa. Sasa muhimu si kuvitembelea tu ni vyema nikatembelea nikaviona watu wanavyofanya kazi, lakini suala nikishapewa matatizo niweze kuyapatia ufumbuzi, na ufumbuzi ni lazima nipate fedha tununue hizo dawa, na hivi sasa tumo katika utaratibu huo. Kwa hivyo, nitatembelea baada ya bajeti nitakuja Bi Mwajuma.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naomba kwa unyenyekevu kabisa Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima kwako wewe nikumbushie tu kwamba jukumu la Baraza la Wawakilishi miongoni mwa majukumu matatu makuu moja wapo ni kuihoji, kuiuliza na kusimamia utendaji wa serikali.

Majukumu mengine mawili ndiyo hayo ya kupitisha bajeti na matumizi ya serikali na kutunga sheria. Sasa katika majukumu yote hayo matatu jukumu hili la kwanza nililolitaja ndiyo lilopewa muda mchache kuliko majukumu yote mengine, na nishawahi kukwambia hilo kabla Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nimuulize swali la nyongeza Mhe. Waziri lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo;

Kwanza naomba kumwambia kwamba mimi nilibahatika kufanya *research* kidogo, kwa hiyo hilo alitambue kwamba nilifanya *research* katika vituo vitatu vilivyomo ndani ya Jimbo la Kiembesamaki. Kituo cha kwanza ni Chukwani pale nilifanya *research* ya kujua watoto wangapi kwa wastani wanazaliwa kwa mwezi, kwa siku, mapungufu yaliyokuwepo pale mpaka mishahara ya wafanyakazi, mpaka kuangalia kitabu cha wageni mara ya mwisho lini kama Waziri alipita au Naibu Waziri alipita niliangalia, kuangalia ile *log sheet* ya dawa. Kwa hiyo, huo mfumo wa *push* ni kweli unafanyika hivyo, kuangalia mfumo wa kuweka *record* zao za hospitali. Mhe. Mwenyekiti, kituo cha pili ni Mbweni Matrekta sikuwa na *camera* wala sikuwa na Afisa wa Habari, kituo cha tatu ni Kisima Mbaazi.

a) Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba kumuuliza Mhe. Waziri ni lini mara ya mwisho yeye Mhe. Waziri au Naibu Waziri walifanya ziara katika vituo hivyo vitatu ndani ya Jimbo la Kiembesamaki, Kituo cha Chukwani, Kisima Mbaazi na Mbweni Matrekta.

b) Naelewa sana kwamba watendaji jukumu lao moja wapo pia ni kuwa na uangalizi wa karibu wa vituo hivyo, lakini kwa kuwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri ndiyo wanaojibu maswali ndani ya Baraza la Wawakilishi, na wao ndiyo wasimamiaji wakuu wa sera nzima ya afya katika wizara, naamini kwamba wanawajibika na wao kufanya ziara hizo. Lakini hapo hapo naamini Rais Dk. Ali Mohamed Shein aliunda vitengo maalum katika kila wizara vya Sera, Mipango na Utafiti, na kila wizara kumekuwa na vitengo hivi pamoja na Maafisa Habari ambao wamewekwa kwa ajili ya kutoa habari ambapo juzi nilitaja gazeti la Ikulu pia nayo inatoa habari zake kikamilifu.
   Je, anamtumiaje Afisa huyu wa Habari katika kutoa habari ya ziara zake kama hizo ili zijulikane. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, sina hakika wala siwezi kusema kwamba lini tumetembelea vituo vitatu hivyo, siwezi kusema lini kwa sababu kwa kweli mimi sijaenda na mwenzangu leo kunambia kaenda lini. Kwa hivyo, hilo siwezi kujibu, ninachoweza kusema kwamba nitamuahidi kwamba nitavitembelea, lakini narudia kutembelea ni jambo moja na kutatua matatizo ni jambo jengine.

Matatizo ya vituo vya afya, hospitali za afya yote yanalingana anapogundua kwamba hakuna dawa katika kituo anachokisema kwa utaratibu wa ugawaji wa dawa *almost* unakuwa ni namna hiyo hiyo, tatizo la ugawaji wa dawa na upatikanaji wake tumekuwa tunaendelea kulitatua tatizo hili kwa miaka mitatu, sasa na kila nikija hapa kwenye bajeti hoja ya dawa huwa inatajwa. Ninachoamini kwamba kabla sijamaliza miaka yangu ya Waziri wa Afya nitakuwa suala moja ambalo nimelipatia ufumbuzi wa kudumu ni juu ya upatikanaji na usambazaji wa dawa. Kwa hivyo, siwezi kumwambia lini nilikwenda hapo au Naibu wangu lini amekwenda hapo, ninachoweza kuahidi kwamba nitakwenda.

Suala la Afisa wa Habari tunamtumia kila inapostahiki kumtumia, ninachotofautisha mimi siyo lazima ninapokwenda kutembelea nichukue Afisa Habari na atangaze maredioni. Kila mmoja ana utaratibu wake kwa jinsi ya kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamkaribisha Mhe. Waziri kuja kusoma hotuba yake kwanza kuna taarifa ya kupokea wageni siku ya leo. Wageni wetu kwa siku ya leo ambao wako pale juu ni wageni ambao wametoka *Tanzania Peace Initiative Foundation (TPIF);* wageni hawa ni wageni wa asasi ya kiraia ambayo lengo lake ni kuchangia katika kujenga jamii yenye amani kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Jumla yao ni wageni wanane wapo pale juu, wageni hawa wanaongozwa na Mwenyekiti wa Asasi ambaye anaitwa ndugu Modest Damiel Hassan, hebu anyooshe mkono tumuone, Katibu wao ni ndugu Imamu Mtumwa Vuai na waliobakia ni wajumbe wa asasi hiyo. (*Makofi*)

Pia kuna wanafunzi wa kitado cha pili wa Skuli ya Bububu jumla yao ni wanafunzi 70, hebu wanyanyuke tuwaone. Hawa ni wanafunzi kutoka skuli ya Jimbo la Mhe. Hussein Ibrahim Makungu, na

wanafunzi hawa wameongozwa na walimu wao watano, wale walimu hebu wasimame tuwaone pia . Ahsante sana. *(Makofi)*

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 - Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyeiti, naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia kwa mara nyengine kukutana hapa leo, tukiwa wazima wa afya. Aidha, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia mimi mwenyewe afya njema na uzima, nikaweza kusimama hapa leo kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu, Muhtasari wa Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuendelea naliomba Baraza lako liingize kwa ujumla wake maelezo yote ya kitabu changu cha hotuba ya bajeti na muhtasari katika taarifa rasmi za Baraza (*Hansard*).

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba yangu na Wafanyakazi wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jami, Vijana, Wanawake na Watoto, nachukua fursa hii adhimu kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kutuongoza vyema katika safari yetu ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Uongozi wake mahiri, thabiti na makini umeendelea kuwa dira katika utendaji wa kazi zetu. Tunaomba Mwenyezi Mungu azidi kumjaalia afya njema, maarifa na hekima katika kuiongoza nchi yetu, ili tuweze kufikia matarajio na malengo tuliyojiwekea katika kufikia maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, pia napenda nichukue nafasi hii kuwapongeza Makamu wa Kwanza wa Rais, Maalim Seif Sharrif Hamad na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi kwa kumshauri na kumsaidia kwa karibu Mhe. Rais wa Zanzibar katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea kuliongoza Baraza hili tukufu kwa hekima, busara na uadilifu. Umahiri wako katika kuliendesha Baraza hili, umewezesha kuwepo kwa mijadala makini, ambayo imesaidia sana kuimarisha utekelezaji wa majukumu yetu ndani ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wananchi wote kwa kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Sherehe za maadhimisho haya zilitupa fursa ya kutathmini mafanikio tuliyoyapata kupitia sekta mbali mbali katika kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi yetu. Aidha, zilitupa fursa ya kutafakari changamoto tunazopaswa kuzifanyia kazi, ili kuleta maendeleo endelevu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii. Napenda sana kumpongeza Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na Wafanyakazi wake wote kwa kuratibu Sherehe hizi kwa ufanisi mkubwa, na hivyo kuweza kudhihirisha maendeleo ya kupigiwa mfano yaliyopatikana katika miaka hii 50 ya Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuzipongeza serikali zote mbili; Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuandaa na kufanikisha sherehe za miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Aidha, sote tunapaswa kujipongeza kwa kuweza kuudumisha Muungano huu hadi kufikia miaka 50 na huku tukiendeleza amani na mshikamano katika nchi yetu. Sherehe zilionesha namna gani tumejizatiti kuendelea kuudumisha Muungano wetu, ambao ni wa kipekee na wa mfano Barani Afrika. Napenda kuwapongeza viongozi wetu mahiri Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na Dkt Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa mafanikio hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuishukuru Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii ya Baraza lako Tukufu chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma, pamoja na Wajumbe wake wote kwa ushirikiano, mawazo na michango waliyotupa, ambayo imeisaidia Wizara kuimarisha utekelezaji wa majukumu yake. Ni matarajio yangu kwamba tutaendelea kushirikiana kwa pamoja katika kuimarisha utekelezaji wa majukumu yetu, ili kuleta mabadiliko yanayotarajiwa ya hali za wanawake, vijana, watoto, wazee na jamii kwa ujumla. Pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa miongozo na michango yao iliyotuwezesha kutekeleza majukumu ya wizara kwa ufanisi.

Aidha, napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo kwa kuchaguliwa kuwa Mwakilishi wa jimbo la Kiembesamaki na kujiunga nasi katika shughuli za Baraza hili. Hongera sana Mhe. Mahmoud Thabit Kombo.

Mhe. Mwenyekiti, utakumbuka kwamba mwaka jana nilisoma mbele ya Baraza lako Tukufu Hotuba ya Bajeti kwa Wizara ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto. Mabadiliko ya baadhi ya Wizara yaliyofanywa mwezi Agosti 2013, yalipelekea kuanzishwa kwa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kuniamini na kuniteua kuiongoza wizara hii.

MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015

Mhe. Mwenyekiti, bajeti na shughuli zilizopangwa kutekelezwa na wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2014/2015 zimezingatia Mipango Mikuu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo ni Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini Zanzibar (MKUZA II – 2010-2015), Malengo ya Milenia 2015, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa mwaka 2010-2015, Mwelekeo wa Sera za CCM 2010-2020, Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015, Sera za Kisekta pamoja na Mpango Mkakati wa wizara.

Aidha, matumizi ya wizara yataelekezwa zaidi katika kuimarisha programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi, hifadhi ya jamii kwa wazee na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, maendeleo ya vijana, mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto, pamoja na kushajiisha usawa na uwiano wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kwa kipindi cha mwaka 2014/2015 imejipangia kutekeleza malengo makuu yafuatayo:

1. Kuimarisha hali za kiuchumi na kijamii za vijana, wanawake, watoto, wazee, makundi yanayoishi katika mazingira magumu na jamii kwa ujumla;

2. Kuhakikisha kuwa mapungufu ya sera na sheria katika masuala ya uwezeshaji na yanayohusu watoto, wanawake, vijana, wazee na makundi yanayoishi katika mazingira magumu yanafanyiwa kazi;

3. Kuimarisha ubora wa huduma na upatikanaji wa hifadhi ya jamii kwa watoto, wanawake, vijana, wazee na makundi yanayoishi katika mazingira magumu;

4. Kuhakikisha kuwa taarifa zinazohusu masuala ya wanawake, vijana, watoto, wazee, hifadhi ya jamii na uwezeshaji wananchi kiuchumi zinakusanywa na kutumiwa katika kuandaa na kuimarisha sera, mikakati na programu;

5. Kukuza uwelewa wa jamii juu ya dhana, misingi na kanuni za ushirika; na

6. Kuimarisha uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014,wizara ilipangiwa kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi Milioni Kumi (shs10,000,000) kutokana na usajili na huduma za ukaguzi wa vyama vya ushirika. Hadi

kufikia mwezi wa Mei 2014, jumla ya Shilingi Milioni Tano, laki Tisa na Elfu Thamanini na Tano (shs 5,985,000/=) zilikuwa zimekusanywa, sawa na asilimia 60 ya makadirio kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014, wizara ilitengewa Shilingi Bilioni Tatu, Milioni Mia Mbili Arobaini na Tisa, Laki Sita na Elfu Ishirini na Mbili (shs 3,249,622,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida, ikiwa ni pamoja na mishahara. Hadi kufikia mwezi wa Mei, 2014, fedha zilizotolewa ni Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne na Tisini na Tano, Laki Tatu na Hamsini Elfu (shs.2,495,350,000/=) ambayo ni sawa na asilimia 77 ya fedha zilizotengwa. Aidha, Wizara ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nane na Themanini (shs.1,880,000,000/=) kwa kazi za maendeleo. Fedha zilizotolewa kwa kazi hizo mpaka kufikia mwezi Mei, 2014 ni Shilingi Milioni Mia Tano Arobaini na Mbili, Laki Mbili na Elfu Tisini na Mbili (shs.542,292,000/=), ambazo ni sawa na asilimia 29 ya fedha zilizotengwa *(Angalia Kiambatanisho Namb. 1a na 1b).*

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya wizara hii yanatekelezwa kupitia Idara zake nane na Ofisi kuu Pemba kama zifuatazo:

1. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
2. Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
3. Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi;
4. Idara ya Ushirika;
5. Idara ya Mikopo;
6. Idara ya Ustawi wa Jamii,
7. Idara ya Maendeleo ya Vijana; na
8. Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto.
9. Ofisi Kuu Pemba inasimamia shughuli zote za wizara, ikiwemo majukumu ya idara hizi kwa Pemba.

Utekelezaji wa malengo ya Wizara kupitia Idara hizi kwa mwaka 2013/2014 na malengo kwa mwaka 2014/2015 ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, idara hii ilijipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia uingizwaji wa masuala ya jinsia na mtambuka katika mipango, bajeti, programu/miradi na sera za kisekta na wizara;
2. Kusimamia uandaaji wa tafiti mbili zinazohusu masuala ya jinsia na maendeleo ya vikundi vya wanawake;
3. Kuimarisha uratibu, uandaaji na ukusanyaji wa taarifa, ufuatiliaji na tathmini ya mipango, programu na bajeti ya wizara;
4. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuleta maendeleo na ustawi wa wanawake, vijana, wazee na watoto;
5. Kusimamia utekelezaji wa miradi ya wizara.

Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka 2013/2014:

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ni kusimamia uandaaji wa sera, ili kujenga mfumo mzuri wa utekelezaji wa shughuli inazozisimamia. Katika hili, Wizara tayari imekamilisha Sera ya Maendeleo ya Ushirika na Sera ya Hifadhi ya Jamii, ambazo zimeshapitishwa rasmi na ziko tayari kutumika. Sera hizi zitakuwa ndio dira na miongozo katika uendeshaji wa vyama vya ushirika na usimamiaji wa mipango ya hifadhi ya jamii Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, wizara pia imeandaa Rasimu ya Sera ya Jinsia ambayo ipo tayari kujadiliwa katika kikao cha Kamati ya Makatibu Wakuu. Sambamba na hilo, wizara inaandaa mpango wa utekelezaji wa sera hiyo. Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Vijana nayo imekamilika na matayarisho yanafanywa ili kuiwasilisha katika vikao vya maamuzi. Pia wizara imo katika hatua ya kutayarisha Sera ya Uwezeshaji, imefanya ufuatiliaji katika kamati 18 za shehia Pemba na 10 Unguja za kupinga vitendo cya udhalilishaji ili kutathmini utekelezaji wa shughuli zao na kupewa ushauri na maelekezo ya kuwasaidia kuimarisha kazi zao. Imesimamia uundwaji wa kamati 11 za shehia za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia katika Wilaya ya Chake Chake Pemba na kupewa maelekezo ya namna ya kusimamia shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wake ili uendane na mabadiliko yaliyofanywa kuhusiana na majukumu yake na kushughulikia changamoto mpya zilizojitokeza. Mpango Mkakati huo umekamilika na umetumika katika uandaaji wa Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imetayarisha na kuwasilisha kunakohusika ripoti mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji wa majukumu yake. Taarifa hizo ni pamoja na zinazohusu utekelezaji wa miradi inayosimamiwa na Wizara, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2005) na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara. Aidha, ziara za ufuatiliaji zimefanywa ili kuangalia utekelezaji wa programu za Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imo katika hatua ya kukusanya Taarifa za Hali ya Kijinsia (*Gender Profile*) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali. Kuwepo kwa taarifa hizo kutasaidia uandaaji wa Sera na Mipango ya Kitaifa inayozingatia masuala ya kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuimarisha uzingatiaji wa masuala mtambuka katika sera, mipango na program za wizara, mafunzo yametolewa kwa wajumbe wa Kamati ya Wizara inayoshughulikia masuala mtambuka kwa upande wa Unguja. Mafunzo hayo ni pamoja na yaliyohusu uzingatiaji wa masuala ya kijinsia katika bajeti, mipango, sera na programu na masuala ya uwezeshaji na ujasiriamali. Kwa upande wa Pemba, wafanyakazi na familia zao wamepatiwa mafunzo ya kujikinga na maambukizo ya virusi vya UKIMWI na vifo vitokanavyo na UKIMWI, pamoja na kuhimiza utendaji wa kazi kwa kuzingatia jinsia.

Mhe. Mwenyekiti, kamati 18 za Shehia Pemba na 10 Unguja za kupinga vitendo vya udhalilishaji zimefuatiliwa ili kutathmini utekelezaji wa shughuli zao na kupewa ushauri na maelekezo ya kuwasaidia kuimarisha kazi zao. Aidha, jumla ya vijana 120 kutoka Mikoa 3 ya Unguja na 80 kutoka Mikoa miwili ya Pemba walipatiwa mafunzo ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na kuepukana na mimba na ndoa za utotoni. Vile vile, Wizara imesimamia uundwaji wa kamati kumi na moja (11) za Shehia za kupambana na udhalilishaji wa kijinsia katika Wilaya ya Chake Chake, Pemba. Aidha, Kamati hizo zilipewa maelekezo na kujengewa uwezo wa kusimamia shughuli zao kwa kushirikiana na Masheha na Waratibu wa Wanawake na Watoto wa Shehia.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeendelea kutoa taarifa mbali mbali kupitia vyombo vya habari ili kuielewesha jamii juu ya shughuli inazozitekeleza. Jumla ya taarifa 17 za matukio mbali mbali ya Wizara zilirushwa hewani kupitia vyombo vya habari. Pia vipindi vitatu (3) vya redio na televisheni kwa ajili ya kushajiisha jamii kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia viliandaliwa na kurushwa hewani. Vile vile, makala mbili (2) zilizozungumzia masuala ya haki za wanawake na kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ziliandaliwa na kutolewa katika Gazeti la “Zanzibar Leo”.

Utekelezaji wa Programu zinazosimamiwa na Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia Idara ya Mipango, Sera na Utafiti katika kipindi cha mwaka 2013/2014 imesimamia utekelezaji wa Programu mbili zifuatazo:

Programu ya Jinsia Zanzibar

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu (*UNFPA*). Madhumuni ya programu hii ni kuisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzingatia masuala ya kijinsia katika sera, mipango na bajeti, pamoja na kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali na wananchi katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/2014, Wizara kupitia programu hii imetekeleza yafuatayo:

- Imetayarisha miongozo kwa viongozi wa dini mbili kuu, ya Kiislamu na ya Kikristo, kwa ajili ya kuwafundisha waumini wao juu ya masuala ya kupinga udhalilishaji wa kijinsia. Miongozo hii imeshafanyiwa majaribio na marekebisho na ipo tayari kwa kutumika.

- Imeandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Kuondoa Aina Zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (*CEDAW*) kwa upande wa Zanzibar. Taarifa hiyo inayozungumzia utekelezaji kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2011 hadi 2014, itajumuishwa na ile ya Tanzania Bara kwa ajili ya kuwasilishwa katika Mkutano wa Umoja wa Mataifa utakaofanyika mwezi Septemba 2014.

- Imezijengea uwezo Kamati za kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia za Mkokotoni, Mahonda na Kinyasini Unguja na Micheweni na Konde Pemba ili ziweze kufanya kazi zao kwa ufanisi. Jumla ya Wajumbe 140 wa kamati hizo wamepatiwa mafunzo ya ushauri nasaha, Sheria na taratibu za kukuza mwitiko dhidi ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia na ufuatiliaji wa kesi.

- Imefanya tathmini ya mapungufu yaliyopo katika Sheria ya Usajili wa Ndoa ya mwaka 1966 sura ya 91 na 92, ambapo tathmini hiyo iligundua kwamba Sheria hii imejikita zaidi katika masuala ya usajili na haikugusia masuala muhimu yanayohusu ndoa, ikiwemo suala la haki na wajibu wa wanandoa, umri wa kuingia katika ndoa, tafsiri ya ndoa na suala la matunzo ya watoto baada ya kuvunjika kwa ndoa. Aidha, ripoti ya tathmini hiyo ilieleza kuwa kuna umuhimu wa kuandaliwa Sheria maalum ya ndoa, lakini itanguliwe na uandaaji wa Sera ya Kuimarisha Familia.

- Imeandaa Muhtasari (*Fact Sheet)* juu ya hali halisi ya udhalilishaji wa kijinsia ambao utatumika kushajiisha jamii kuchukua hatua dhidi ya vitendo vya udhalilishaji. Vile vile, wizara imeandaa mchezo wa kuigiza, wenye sehemu 25, kwa ajili ya kuelimisha jamii juu ya athari ya ukatili wa kijinsia kupitia redio. Mbali na hayo, Wizara imetayarisha filamu ya ushuhuda wa vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar, ambayo itatumika katika programu za kuelimisha jamii juu ya athari za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Programu ya Kukuza usawa wa Kijinsia na Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi

Mhe. Mwenyekiti, programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano na Shirika la *UN- Women* kwa lengo la kusaidia jitihada za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Kupitia programu hii, wizara katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 imetekeleza yafuatayo:

- Imefanya utafiti wa kuvitambua vikundi vya uzalishaji na vya kiuchumi vya wanawake katika Wilaya zote 10 za Unguja na Pemba. Utafiti huu utaweza kutambua aina ya biashara zinazofanywa na kinamama, uimara wa vikundi vyao, mitaji waliyonayo ya kuendesha biashara zao na maeneo vilipo vikundi hivyo,

- Imetoa mafunzo ya kuvijengea uwezo vikundi vya wanawake vya Mkoa wa Kaskazini Unguja, jumla ya wanawake 60 wamenufaika na mafunzo hayo na kwa upande wa Pemba jumla ya wanawake 60 wa Wilaya ya Micheweni na Mkoani wamenufaika na mafunzo hayo. Mafunzo hayo yalihusu utengenezaji wa bidhaa, ufungashaji, ufugaji wa kuku wa kisasa na kienyeji, utengenezaji wa unga wa lishe, ulimaji wa mboga mboga, utengenezaji wa sabuni na utafutaji wa masoko.

- Pia kupitia mradi huu, watendaji wawili wa Wizara ilihudhuria mkutano wa 58 wa Tume ya Umoja wa Mataifa Juu ya Hadhi ya Wanawake, uliofanyika New York, Marekani ambapo ujumbe wa mwaka huu ulikuwa ni **'Changamoto na Mafanikio katika Kutekeleza Malengo ya Milenia kwa Wanawake na Watoto wa Kike'**. Mkutano huo uliweka azimio la kuweka lengo mahsusi linalohusu usawa wa kijinsia katika Ajenda ya Maendeleo ya Baada ya Mwaka 2015. Pamoja na mambo mengine mkazo uliwekwa katika kumuwezesha mwanamke kiuchumi na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Aidha, ilisisitizwa kuwa malengo mengine yote yaliyobaki yazingatie usawa wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kusimamia uingizaji wa masuala mtambuka, ikiwemo masuala ya jinsia katika sera, mipango, programu na bajeti za kisekta na Wizara;
2. Kusimamia uandaaji wa utafiti wa kuangalia athari za utalii na mmonyoko wa maadili kwa vijana;
3. Kusimamia uandaaji wa Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii, Sera ya Watoto, Sera ya Uwezeshaji na Sera ya Maendeleo ya Vijana;
4. Kuimarisha uandaaji, uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya mipango na programu za wizara;
5. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili kuleta maendeleo na ustawi wa wanawake, vijana, wazee, watoto na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi; na
6. Kuratibu utekelezaji wa programu na miradi inayosimamiwa na Wizara.

   Mhe. Mwenyekiti, ili Idara ya Mipango, Sera na Utafiti iweze kutekeleza malengo yake iliyojiwekea kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Elfu Sitini na Tano (shs 165,000,000/=) kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Mbili na Nne, Laki saba na Elfu Thalathini na Tano (shs 2,204,735,000/=) kwa Kazi za Maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2013/14, idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kusimamia shughuli za kila siku za Uendeshaji na Utumishi za wizara, ikiwemo Sheria na Kanuni za Utumishi Serikalini na kuhakikisha wafanyakazi wanafuata Sheria na Kanuni za Usimamizi wa fedha na manunuzi ya vifaa vya Ofisi;
2. Kuwajengea uwezo wafanyakazi wa wizara kwa kuwasaidia malipo ya ada ya masomo ya muda mrefu na muda mfupi kwa kuzingatia mahitaji ya wizara;
3. Kuimarisha utendaji kazi kwa kusimamia ununuzi wa vifaa muhimu vya kutendea kazi;
4. Kuimarisha wizara kwa kuajiri wafanyakazi wapya kumi na nane (18) Unguja na wanane (8) Pemba; na
5. Kuendelea kuviimarisha vitengo vya manunuzi, uhasibu na ukaguzi wa ndani.

Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Uendeshaji na Utumishi kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, katika kusimamia uendeshaji wa shughuli za kila siku, Wizara imeshughulikia upatikanaji na utunzaji wa vifaa mbali mbali vya Ofisi, huduma za mawasiliano na usafiri, pamoja na kuvifanyia matengenezo vyombo ya usafiri na vifaa vya ofisi Unguja na Pemba. Aidha, wizara imenunua vespa mbili (2) ili kuimarisha huduma za usafiri kwa ufuatiliaji wa shughuli za kazi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imeajiri wafanyakazi wapya 13 (4 wanaume na 9 wanawake) katika fani za Uchumi, Utawala, Katibu Muhtasi, Udereva, Ufundi, Ushoni na Upishi Unguja na Pemba. Nafasi hizi zimejazwa kutokana na kuachwa wazi na wafanyakazi waliostaafu kazi kisheria na wengine kufariki

dunia. Aidha, Wizara imepokea wafanyakazi wawili (2) kwa njia ya uhamisho kutoka taasisi nyengine za Serikali na wafanyakazi tisa (9) walipewa uhamisho wa kwenda kuendelea na kazi katika Wizara nyengine. Pia, wafanyakazi kumi (10) walistaafu kazi kisheria, wafanyakazi wawili (2) waliacha kazi kwa hiari yao na wafanyakazi watatu (3) walifariki dunia *(Angalia Kiambatanisho Namb.2a)*

Mhe. Mwenyekiti, wizara imewapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi 4, (2 Unguja na 2 Pemba) katika kada ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani, Uandishi wa Kumbukumbu, Habari na Mawasiliano. Pia, wizara imewasaidia ada ya masomo wafanyakazi 29 (Unguja 21 na Pemba 8) wanaochukua masomo ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali nchini Tanzania. Wafanyakazi hao wanasomea fani za Ustawi wa Jamii, Uchumi, Sheria, Maendeleo ya Jamii, Ushirika, Mipango na Uongozi, Uongozi wa Fedha na Ujasiriamali, Utunzaji Kumbukumbu na Ukatibu Muhutasi *(Angalia Kiambatanisho Namb. 2b)*.

Mhe. Mwenyekiti, wizara imefanya vikao kumi (10) vya Kamati Tendaji na vikao vitatu (3) vya Kamati ya Uongozi. Miongoni mwa yaliyojadiliwa katika vikao vya Kamati hizo ni pamoja na rasimu za Sera ya Hifadhi ya Jamii, Sera ya Maendeleo ya Vijana na Sera ya Maendeleo ya Ushirika, pamoja na taarifa za utekelezaji wa programu mbali mbali zinazosimamiwa na Wizara.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuendana na mabadiliko yaliyofanywa katika muundo wa wizara, Bodi ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi wa Ndani ya wizara zimeundwa upya. Bodi ya Zabuni imefanya vikao viwili (2) ambavyo, pamoja na mambo mengine, vilijadili na kupitisha Mpango wa Manunuzi kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2005 na Ripoti za Manunuzi. Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za Ndani pia imefanya vikao viwili (2) ambavyo vilipitia na kujadili Ripoti za Ukaguzi wa Ndani zilizowasilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara kupitia Kitengo cha Ukaguzi wa Hesabu za Ndani ilifanya ukaguzi wa mahesabu na matumizi ya Wizara katika Idara, Miradi na Programu zake mbali mbali Unguja na Pemba. Lengo ni kuhakikisha kuwa fedha na mali nyengine za Wizara zinasimamiwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha na Manunuzi za mwaka 2005.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2014/2015 Idara ya Uendeshaji na Utumishi imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kufanya tathmini ya mahitaji ya uwezo wa rasilimali watu katika Wizara;
2. Kuimarisha uwezo wa utendaji kwa kusimamia upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa wafanyakazi 10 (Unguja 8 na Pemba 2) na kuajiri wafanyakazi wapya 76 (Unguja 55 na Pemba 21);
3. Kuimarisha mfumo wa mawasiliano wa wizara kwa kununua mtambo na vifaa muhimu vya mawasiliano vitakavyowezesha kujiunga na mfumo wa serikali wa mtandao (*E–government*), pamoja na kuweka simu za mezani;
4. Kuimarisha utendaji kazi kwa kusimamia ununuzi wa vifaa mbalimbali vya ofisi;
5. Kuendelea kusimamia nidhamu, wajibu na upatikanaji wa haki, maslahi, fursa na motisha kwa wafanyakazi wa Wizara Unguja na Pemba; na
6. Kuimarisha Mfumo wa Habari na Uhusiano wa Wizara.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendeshaji na Utumishi iweze kutekeleza majukumu yake katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu na Sitini (Tshs. 360,000,000/=) kwa kazi za kawaida na jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba na Tano, Laki Moja na Elfu Sitini na Nne (Tshs. 1,705,164,000/=) kwa ajili ya Mishahara, Mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Posho za wafanyakazi Unguja.

IDARA YA UENDELEZAJI NA URATIBU WA PROGRAMU ZA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kujenga utamaduni wa ujasiriamali na kuimarisha uwezo wa wajasiriamali, hususan vijana, katika wilaya 10 za Zanzibar;

2. Kuimarisha usimamizi, huduma za ushauri, ufuatiliaji na tathmini shirikishi ya shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;

3. Kutanua soko la bidhaa za wajasiriamali wadogo wadogo; na

4. Kuijengea uwezo wa kiutendaji Idara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2013/2014:

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/2014, utekelezaji wa malengo kwa Idara hii ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Idara ilipanga kutoa mafunzo kwa awamu sita juu ya ujasiriamali kwa watu 250 (150 Unguja na 100 Pemba) hususan vijana, lakini kutokana na uhaba wa fedha imeweza kutoa mafunzo kwa vijana 50 kutoka Mikoa miwili ya Pemba. Mafunzo hayo yalikusudia kuimarisha utamaduni wa ujasiriamali kwa vijana ili waweze kujiajiri kwa kuanzisha biashara mbali mbali. Pamoja na mambo mengine, mafunzo hayo yamesaidia vijana kubuni mipango ya biashara kulingana na fursa zilizopo katika maeneo yao. Kati ya vijana waliopatiwa mafunzo, vijana 11 (7 wanawake na 4 wanaume) wameweza kujiajiri kwa kuanzisha shughuli za biashara, kilimo, ufugaji na ushoni.

- Idara imetoa mafunzo ya awamu 4 kwa wajasiriamali wadogo wadogo 120 (90 Unguja na 30 Pemba) baada ya kufanya utafiti mdogo wa kubaini mahitaji yao. Pia imewapatia mafunzo wanavikundi 30 wa Wilaya ya Magharibi katika vijiji vya Maungani, Kisauni na Bweleo. Baada ya mafunzo hayo, wanavikundi hao wameunganishwa na wataalamu mbali mbali kulingana na mahitaji na changamoto zinazowakabili, kama vile masoko, upatikanaji wa vifaa vya kilimo na upatikanaji wa mashine ya kutotolea vifaranga na mayai inayotengenezwa kwa kutumia teknolojia rahisi na rasilimali zilizopo nchini.

- Mafunzo ya awamu 4 juu ya Uandishi wa Mpango wa Biashara *(Business Plan)* yalitolewa kwa wajasiriamali 45 (30 Unguja na 15 Pemba). Kutokana na mafunzo hayo, jumla ya Mipango ya Biashara 15 ya wajasiriamali vijana kutoka Mikoa miwili ya Pemba imetayarishwa na kuwasilishwa katika Idara ya Mikopo kwa ajili ya kufanyiwa tathmini juu ya uwezekano wa kupatiwa fedha za mitaji kupitia njia ya mkopo. Pia Idara inatarajia kupokea Mipango ya Biashara 30 kutoka Mikoa mitatu ya Unguja kwa kuiwasilisha Idara ya Mikopo kama ilivyofanywa kwa upande wa Pemba.

- Jumla ya wajasiriamali wadogo wadogo 100 (wanawake 70 na wanaume 30) wameshiriki katika maonesho ya Wiki ya Uwezeshaji yaliyofanyika katika viwanja vya Makao Makuu ya Wizara Mwanakwerekwe na Kisonge. Maonesho hayo yamebainisha kwamba wajasiriamali wadogo wadogo wanahitaji kujengewa uwezo zaidi katika kuimarisha ubora wa bidhaa zao, viwango na vifungashio ambayo ndiyo changamoto kubwa inayowakabili katika kumudu ushindani wa soko la ndani na la Afrika ya Mashariki.

- Kupitia makongano *(clusters)*, Idara imefanya uchanganuzi wa masoko ya ndani ya wajasiriamali wadogo wadogo katika Mikoa mitatu ya Unguja, ili kubaini changamoto katika uzalishaji na uuzaji wa mazao/bidhaa zao. Katika uchanganuzi huo, Idara imeweza kujua aina mbali mbali za bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wadogo wadogo, ubora na wingi wa bidhaa hizo, mitaji na faida inayopatikana, maeneo ya uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hizo na changamoto zinazowakabili. Miongoni mwa changamoto zilizobainika ni pamoja na uhaba wa

bidhaa zinazozalishwa kulingana na mahitaji ya soko, kutokuwepo kwa uendelevu katika uzalishaji, kukosekana kwa vifungashio vya bidhaa za wajasiriamali na ubora unaokubalika wa bidhaa. Changamoto hizo zinaendelea kufanyiwa kazi na Wizara.

- Kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara na Viwanda, Wizara imeweza kuwasaidia wajasiriamali 50 kushiriki katika maonesho ya 14 ya Juakali/Nguvu kazi ambayo kwa mwaka 2013/2014 yalifanyika Nairobi, nchini Kenya.
- Katika kuratibu shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi, Wizara imefanya mikutano miwili ya Kamati za Uwezeshaji za Wilaya ya Kusini na Kaskazini 'A' Unguja. Pia imeandaa mikutano miwili na washirika wengine wa taasisi za Serikali ili kujadili utekelezaji wa programu na shughuli mbali mbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi wanazozitekeleza. Mikutano hiyo pia imewashirikisha Waratibu wa programu mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi, ikiwemo *TASAF;* Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji Thamani Bidhaa na Huduma za Kifedha Vijijini *(MIVARF);* na Programu ya Kukuza Mazingira ya Biashara. Aidha, mikutano hii imesaidia kubadilishana taarifa juu ya utekelezaji wa programu hizo na kupeana uzoefu juu ya mikakati iliyoleta mafanikio.

- Idara imefanya ziara 3 (2 Unguja na 1 Pemba) za ufuatiliaji wa vikundi vya kiuchumi na mjasiriamli mmoja mmoja, ambapo jumla ya vikundi 20 (10 Unguja na 10 Pemba) na wajasiriamali 20 (15 Unguja na 5 Pemba) walitembelewa na kupatiwa huduma za ushauri, ili kukuza biashara zao *(Angalia Kiambatanisho Namb. 3).* Ziara hizo zimesaidia kuona udhaifu na kubaini matatizo yanayovikabili vikundi na wajasiriamali hao. Aidha, mafunzo ya papo kwa papo yalitolewa ili kutatua baadhi ya changamoto zilizobainika.
- Katika kujenga uwezo wa Idara ili iweze kuyamudu vyema majukumu yake, Wizara imemgharamia mfanyakazi mmoja wa Idara hiyo kutoka Pemba, kushiriki katika mafunzo ya wiki mbili juu ya masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi huko Tanzania Bara.

Mhe. Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake ya kuwawezesha wananchi kiuchumi, Wizara pia imekuwa ikishirikiana na taasisi mbali mbali za Serikali na zisizo za Serikali. Wizara kwa kushirikiana na washirika wengine wa masuala haya imo katika maandalizi ya kuanzisha Kituo cha Kulelea Wajasiriamali katika Chuo cha Karume cha Sayansi na teknolojia, Mbweni. Kamati maalumu imeundwa kusimamia uanzishwaji wa kituo hicho. Kamati hiyo inahusisha wawakilishi kutoka Chuo Kikuu cha Taifa *(SUZA),* Jumuiya ya Wafanya Biashara, Viwanda na Wakulima, Chuo cha Karume, Mamlaka ya Vyuo vya Amali, Benki ya Watu wa Zanzibar, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Habari, Wizara ya Mawasiliano, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Shirika la Kazi Duniani. Kituo hicho kitakapokamilika kitatoa taaluma kwa vijana juu ya masuala ya ujasiriamali, ikiwemo kuwasaidia kuibua na kuendeleza mawazo yao ya biashara pamoja na kuwaunganisha na huduma za fedha na masoko.

Mhe. Spika, pia Wizara, kwa msaada wa Tume ya Sayansi na Teknolojia ya Tanzania *(COSTECH)* imepata Mtaalaamu wa kujitolea kutoka nchini Canada, ambaye atasaidia katika masuala ya uimarishaji wa makongano *(clusters)* ya wajasiriamali. Mtaalamu huyo, kwa kushirikiana na Chuo cha Karume cha Sayansi na Teknolojia, Mbweni ametengeneza mashine ya kukaushia mwani na matunda kwa kutumia nguvu ya jua. Lengo ni kuwasaidia wajasiriamali wadogo wadogo kuweza kutumia teknolojia ya nishati ya jua kwa kuhifadhi bidhaa zao zisiharibike.

Malengo ya Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2014/2015, Idara hii imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuandaa mafunzo ya ujasiriamali katika maeneo tofauti kwa vijana 200 wakiwemo wahitimu wa vyuo na vikundi vya kiuchumi;

2. Kuanzisha Mtandao wa Wajasiriamali utakaohusisha taasisi zinazotoa huduma za kifedha na huduma za biashara;
3. Kukuza mashirikiano na taasisi nyengine zinazohusika ili kuhakikisha upatikanaji wa masoko kwa bidhaa za wajasiriamali;
4. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi;
5. Kukamilisha uanzishaji wa Kituo cha Kutotoa Wajasiriamali *(Incubation Center)* Unguja; na
6. Kutoa huduma za kibiashara kwa wajasiriamali wadogo wadogo kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Spika, ili Idara ya Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Sitini na Moja, Laki Tano na Elfu Sabini na Tano (Tshs. 61,575,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA USHIRIKA

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2013/14, Idara ya Ushirika ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuongeza uelewa wa wanachama 3,000 juu ya wajibu, haki na ushiriki katika vyama vya ushirika;
2. Kusimamia utekelezaji wa sheria katika uendeshaji wa vyama vya ushirika 1,200;
3. Kuwezesha uanzishwaji wa vyama viwili vya ushirika vya uzalishaji vinavyohusisha vijana;
4. Kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa kuendeleza vyama vya ushirika;
5. Kuimarisha utendaji wa vyama vikuu 6 na Shirikisho la Vyama vya Ushirika *(CUZA);*
6. Kuimarisha mahusiano na washirika wa sekta ya ushirika; na
7. Kuimarisha mazingira ya kazi, ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vifaa.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Ushirika kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Ushirika katika mwaka 2013/2014 imetekeleza yafuatayo:-

- Imetoa mafunzo juu ya mbinu za ubunifu, ushindani, wajibu na haki za wanachama pamoja na dhana ya Ushirika kwa jumla kwa wanachama 2,372 (Wanawake 1,569 na Wanaume 803). Wanachama hao walitoka kwenye vyama vya ushirika 209 (Unguja 157 na Pemba 52). Kati ya vyama vilivyopatiwa mafunzo hayo, 67 ni *SACCOS* na 142 ni vyama vya uzalishaji na utoaji huduma. Mafunzo hayo yamesaidia kuongeza uelewa wa wanachama hao juu ya haki zao, na kwa kiasi fulani yametoa msukumo kwa wanachama kufuatilia shughuli za vyama vyao.

- Katika kusimamia utekelezaji wa sheria kwenye vyama vya ushirika, Wizara imefanya ufuatiliaji, ukaguzi wa kawaida na kutoa mafunzo ya vitendo kwa vyama vya ushirika 629 (360 Unguja na 269 Pemba). Hii ni miongoni mwa juhudi za kuhakikisha kuwa vyama vya ushirika vinatunza vitabu vya hesabu na kuweka kumbukumbu nyengine kwa usahihi, kwa mujibu wa Sheria na Katiba za vyama husika.

- Vyama vya ushirika 135 (99 Unguja na 36 Pemba) vimefanyiwa ukaguzi wa hesabu, ambapo kati yao 18 ni *SACCOS* na 117 ni vyama vya uzalishaji mali na utoaji huduma. Lengo la ukaguzi huo ni kutambua hali ya mahesabu ilivyo kwenye vyama hivyo na kutoa maoni na ushauri wa kitaalamu juu ya hali halisi ya fedha kwa vyama hivyo. Matokeo ya ukaguzi huo yameonesha ukuaji wa wastani wa mitaji kwa baadhi ya vyama vya ushirika. Hata hivyo, elimu zaidi inahitajika ili kuimarisha udhibiti wa rasilimali na kuleta tija kwenye vyama vya ushirika.

- Vyama viwili (2) vya Ushirika vya vijana wenye taaluma ya elimu ya juu vimeanzishwa, kimoja kinajishughulisha na kilimo cha mboga mboga na chengine kinashughulika na kutoa huduma za kitaalamu kwenye vyama vya ushirika. Vyama hivyo ni; *Zanzibar Professionals Cooperative (ZAPROCO)* chenye wanachama 21 (wanawake 10 na wanaume 11) kilichopo Dole, na Zanzibar Fresh Vegetables Production chenye wanachama 14 (Wanawake 10 na Wanaume 4) kilichopo Maungani, Wilaya ya Magharibi. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani *(ILO)* imepanga kuvijengea uwezo vyama hivyo kupitia programu za ajira kwa vijana, ili viwe mfano kwa vijana wengine kuwapa hamasa ya kujiajiri.

- Jumla ya vyama vya ushirika 41 (Unguja 34 na Pemba 7) vimepatiwa mafunzo shirikishi ya kuandaa mipango ya biashara. Miradi iliyoandikiwa mipango ya biashara inajumuisha ya kilimo cha mboga mboga, ushoni, ufugaji wa samaki, ufugaji kuku, ukaushaji samaki, usagaji wa nafaka, uvuvi, upandaji miti, ufugaji nyuki, ufyatuaji matofali, useremala, kazi za mikono na ufundi umeme. Vikundi hivyo vimeunganishwa na taasisi za kifedha ili viweze kupatiwa mikopo kwa utekelezaji wa mipango yao ya biashara.

- Juhudi za kuimarisha uendeshaji wa Vyama Vikuu na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Zanzibar *(CUZA)* zimeendelea. Ziara za ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu kwa mujibu wa Mipango Mikakati ya Vyama Vikuu hivyo na *CUZA* zimefanywa. Aidha, vikao viwili baina ya Mrajisi wa Vyama vya Ushirika na Bodi ya *CUZA* vimefanyika ili kujadili na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa lengo la kurekebisha kasoro za utendaji zilizobainika. Hata hivyo, Wizara inaendelea kutoa mafunzo na ushauri zaidi kwa vyama hivyo ili viweze kufanya shughuli zake ipasavyo.

- Wizara iliandaa maadhimisho ya Siku ya Ushirika Duniani, ambayo huadhimishwa Jumamosi ya mwanzo ya mwezi Julai kila mwaka. Maadhimisho hayo yalijumuisha mkutano wa wadau wa kujadili maendeleo na namna ya kukabiliana na changamoto kwenye vyama vya Ushirika. Aidha, Tamko Rasmi la Waziri kuhusiana na maadhimisho ya siku hiyo lilitolewa. Vile vile, kipindi maalum kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar *(ZBC - TV)* kiliandaliwa. Maadhimisho haya pia yalilenga kuwashajiisha wananchi juu ya umuhimu wa Sekta ya Ushirika kwa maendeleo ya watu, hasa wenye kipato cha chini.

- Ili kuimarisha mashirikiano na wahusika wengine wa masuala ya ushirika, watendaji wawili (2) wa Wizara walishiriki katika Mkutano uliofanyika Chuo Kikuu cha Ushirika na Biashara, Moshi. Mkutano huo ulijadili hali ya maendeleo ya ushirika nchini pamoja na changamoto za upatikanaji wa huduma za mikopo. Pia watendaji hao walibadilishana mawazo na uongozi wa Chuo Kikuu cha Ushirika juu ya uwezekano wa Chuo hicho kushirikiana na Vyuo vilivyopo Zanzibar ili kutoa mafunzo na elimu ya Ushirika.

Malengo ya Idara ya Ushirika kwa mwaka 2014/2015

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka 2014/ 2015, Idara ya Ushirika imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kukuza uwezo wa ushindani wa vyama vya ushirika 10 ili vitoe huduma kwenye soko la utalii ifikapo Juni 2015;
2. Kuongeza uelewa kwa wanachama na viongozi 3,000 juu ya maadili, kanuni za ushirika, na mbinu za utendaji bora kwenye vyama vya ushirika ifikapo Juni 2015;
3. Kusimamia utekelezaji wa sheria katika uendeshaji wa vyama vya ushirika 1,400 ifikapo Juni 2015;

4. Kuimarisha mashirikiano na washirika ili kubadilishana taarifa na kujifunza mambo mapya ya kuendeleza sekta ya ushirika ifikapo 2015;
5. Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya vyama vya ushirika ifikapo Juni 2015; na
6. Kuimarisha mazingira ya kazi ikiwemo mafunzo kwa wafanyakazi na upatikanaji wa vifaa.

Mhe. Spika, ili Idara ya Ushirika iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2014/15, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi Milioni Arobaini na Tisa, Laki Tisa na Elfu Thelathini na Nane (Tshs. 49,938,000/=) kwa matumizi ya kazi za kawaida.

IDARA YA MIKOPO

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014, Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kutoa mikopo 1,000 kwa vikundi vya kiuchumi na watu binafsi/mjasiriamali mmoja mmoja yenye thamani ya Tshs. 300,000,000/=;
2. Kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kutoka asilimia 85 hadi zaidi ya asilimia 95;
3. Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za mikopo; na
4. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa shughuli za mikopo nafuu hapa nchini.

Utekelezaji wa Malengo ya Idara ya Mikopo 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Idara ya Mikopo ilitekeleza yafuatayo:-

- Imetoa mikopo 550 (Unguja 328 na Pemba 222) kupitia Mfuko wa Kujitegemea, yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Mbili Tisini na Nne, Laki Nane na Elfu Sabini na Saba (Tshs. 294,877,000/=). Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni Mia Mbili Kumi na Moja, Laki Nane na Elfu Sabini na Saba (TShs. 211,877,000/=) zilitolewa kwa wakopaji wa Unguja na Shilingi Milioni Themanini na tatu (Tshs.83,000,000/=) zilitolewa kwa wakopaji wa Pemba. *(Angalia Kiambatanisho Namb. 4).*

  Aidha, Wizara imetoa mafunzo kwa wakopaji 550 kuhusiana na uwekaji wa kumbukumbu za hesabu, faida za kutumia huduma za kibenki kwa wakopaji, umuhimu wa kujiwekea akiba na utafutaji wa masoko. Mafunzo haya yalitolewa ili kuwawezesha wajasiriamali kuzitumia fedha za mikopo vizuri na kwa malengo yaliyokusudiwa, pamoja na kusimamia vizuri biashara zao.

  Idara imeendelea kufuatilia marejesho ya mikopo ya Mfuko wa JK/AK, ambapo jumla ya Shilingi Milioni Thelathini, Laki Sita Elfu Themanini, Mia Nne na Sabini na Nane (Tshs. 30,680,478/=) zimekusanywa katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014. (*Angalia Kiambatanisho Namb*. 5). Idara pia imefanya ziara za ufuatiliaji wa marejesho ya mikopo katika Wilaya zote za Unguja na Pemba. Ziara hizo zililenga kuangalia maendeleo ya miradi ya wakopaji na changamoto zao, pamoja na kuwashauri juu ya namna bora ya kuendesha biashara zao, ili waweze kupata tija na kulipa mikopo yao kama inavyotakiwa.

- Idara imeanzisha mtandao wa taasisi zinazotoa huduma za kifedha kwa wajasiriamali wadogo ili kubadilishana taarifa za wakopaji na kufuatilia kwa karibu mwenendo wa uchukuaji na urejeshaji mikopo. Mtandao huo umejumuisha taasisi mbalimbali za kifedha, zikiwemo *WEDTF; YOSEFO; CRDB;* CHANGAMOTO; Jumuiya ya Wafanyabiashara, Wenye Viwanda na Wakulima Zanzibar; na *SACCOS* mbalimbali za mijini na vijijini. Kupitia mtandao huo, imeripotiwa kuwa hadi kufikia mwezi wa Aprili 2014, Jumuiya ya *WEDTF* imetoa mikopo 196 yenye thamani ya Shilingi Milioni Sitini na Moja (Tshs. 61,000,000/=); *SACCOS* kubwa 16 zimetoa mikopo 216 yenye thamani ya Shilingi Milioni Arobaini na Mbili

(Tshs.42,000,000/=); na *CRDB* kupitia Mfuko wa Vijana imetoa mikopo kwa vikundi 116 yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Tano (Tshs.245,000,000/=).

Idara imefanya mikutano kadhaa na Mamlaka za Wilaya na Shehia kuhimiza urejeshwaji wa fedha za mkopo. Mikutano hii pia ilitumika kuwaelewesha washiriki juu ya madhumuni ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, pamoja na Muongozo wa uendeshaji wake, ikiwemo taratibu za uombaji na utoaji wa mikopo. Aidha, mikutano hiyo ilisaidia kuongezeka urejeshwaji wa fedha za mikopo, ambapo hadi kufikia mwezi wa Aprili 2014, jumla ya Shilingi Milioni Mia Moja na Kumi na Moja, Laki Moja, Elfu Tano na Mia Moja (T.shs 111,105,100/=) zimerejeshwa katika Mfuko wa Kujitegemea Unguja na Pemba. Kati ya fedha hizo, Shilingi Milioni Themanini na Tatu, Elfu Hamsini na Nane na Mia Sita (TShs. 83,058,600/-) zilirejeshwa kutoka kwa wakopaji wa Unguja na Shilingi Milioni Ishirini na Nane, Elfu Arobaini na Sita na Mia Tano (Tshs. 28,046,500/=) kutoka kwa wakopaji wa Pemba (*Angalia Kiambatanisho Namb. 6*).

- Ili kujifunza uzoefu wa taasisi nyengine katika masuala ya mikopo, Idara imefanya ziara za kujifunza kwa taasisi bora zinazotoa mikopo huko Tanzania Bara. Taasisi zilizotembelewa ni Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi *(National Economic Empowerment Council)* na *BLUE Finance* zilizoko Dar es Salaam. Pia ziara mbili kwa wafanyakazi wa Idara baina ya Unguja na Pemba zilifanyika, ambapo waliweza kujifunza na kubadilishana uzoefu katika uwekaji wa kumbukumbu za mikopo.

- Idara imeendelea kufuatilia ahadi za uchangiaji wa fedha zilizotolewa na taasisi, wafanyabiashara na wananchi mbali mbali kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. ambao ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, tarehe 21 Disemba, 2013. Katika uchangishaji huo, ahadi za jumla ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Ishirini na Tatu, Laki Nne na Elfu Tisini (Tshs. 1,023,490,000/=) zilitolewa. Hadi sasa jumla ya Shilingi Milioni Mia Tisa Sitini na Moja, Laki Nane na Elfu Tisini (Tshs. 961,890,000/=) fedha taslim zimekusanywa ambazo ni sawa na asilimia 94 ya ahadi zote. Zoezi la kufuatilia ahadi zilizobaki linaendelea. Naomba nichukue fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Rais ya Kusimamia Uchangiaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Haroun A. Suleiman, Waziri wa Nchi (Ofisi ya Rais) Kazi na Utumishi wa Umma, Kamati hii imefanya kazi kubwa na nzuri ya kupigiwa mfano.

  Aidha, nachukua fursa hii kutoa shukurani maalumu kwa taasisi, wafanyabiashara na wananchi mbali mbali ambao wamechangia fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko huu. Nataka niwaahidi kwamba Wizara yangu itasimamia vyema Mfuko huu, ili kuhakikisha unafikia malengo yake ya kuwawezesha wananchi wa Zanzibar wenye kipato cha chini kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu, ili waweze kujiajiri kwa shughuli za kiuchumi na kujikwamua kutoka kwenye umaskini.

- Ili kuimarisha utendaji, wafanyakazi watatu (Unguja mmoja na Pemba wawili) wamegharamiwa kuendelea na mafunzo ya muda mrefu katika fani ya mikopo na ujasiriamali, usimamizi wa masoko na usimamizi wa rasilimali watu. Mafunzo hayo yatasaidia kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye taaluma, jambo ambalo ni muhimu katika kuleta ufanisi kwenye utendaji wa shughuli za Idara.

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015, Idara hii imepanga kuendelea kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kutoa mikopo 1,000 yenye thamani ya Shilingi 500,000,000/= kupitia vikundi vya kiuchumi na mjasiriamali mmoja mmoja katika sekta za kiuchumi;
2. Kuongeza kiwango cha marejesho ya mikopo kutoka asilimia 85 hadi asilimia 95;
3. Kuanzisha fursa mpya za mikopo na kuwaelewesha wananchi juu ya Muongozo wa Uendeshaji wa Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi;
4. Kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wateja wa mikopo;
5. Kuendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kutunisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili uendelee kuwasaidia wajasiriamali wengi zaidi;
6. Kuimarisha mashirikiano na uratibu wa shughuli za mikopo nafuu hapa nchini; na
7. Kuimarisha uwezo wa watendaji ili kuongeza ufanisi wa kazi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Mikopo iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Thamanini na Nne, Laki Tisa na Elfu Arobaini (T.shs 84,940,000/=) kwa matumizi ya kawaida.

IDARA YA USTAWI WA JAMII

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Ustawi wa Jamii ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha Mfumo wa Hifadhi ya Mtoto;
2. Kuimarisha uratibu na kufuatilia masuala ya malezi na makuzi ya awali ya watoto kuanzia miaka 0-8;
3. Kuimarisha Hifadhi ya Wazee;
4. Kusimamia ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali kazini; na
5. Kuimarisha shughuli za kuwapatia wanajamii misaada ya kiustawi.

Utekelezaji wa Malengo kwa Idara ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2013/2014

Mhe. Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/204, Idara ya Ustawi wa Jamii imetekeleza shughuli zifuatazo:-

- Imekusanya taarifa za udhalilishaji wa watoto kutoka Wilaya za Unguja na Pemba na kuziingiza katika mfumo wa kuhifadhi taarifa. Aidha, vituo vyengine viwili vya Mkono kwa Mkono vimeanzishwa katika Hospitali za Wete na Micheweni kwa ajili ya kurahisisha ushughulikiaji wa kesi za udhalilishaji katika maeneo hayo. Pia, mkutano mmoja (1) umefanywa ili kuwakutanisha wafanyakazi wa Vituo vya Mkono kwa Mkono vya Hospitali ya Mnazimoja, Kivunge na Makunduchi kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kujadili mafanikio pamoja na changamoto zinazowakabili katika kutoa huduma hizo. Pamoja na hayo, Kitengo cha Hifadhi ya Mtoto cha Mkoa wa Kaskazini Unguja kimeimarishwa kwa kupatiwa vifaa vya kufanyia kazi, ikiwemo kompyuta, printa, fotokopi na samani. Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, jumla ya malalamiko 2,356 (2,258 Unguja na 98 Pemba) ya udhalilishaji wa watoto yaliripotiwa na kushughulikiwa katika vituo vya Mkono kwa Mkono *(Angalia Kiambatanisho Namb. 7a na 7b).*

- Kwa kushirikiana na Wajumbe wa Kamati ya Kitaifa ya Hifadhi ya Watoto, Idara imefuatilia kesi 20 za watoto waliodhalilishwa zilizoripotiwa katika kipindi cha miezi sita (Agosti - Januari). Aidha, Mkutano mmoja wa kuratibu na kujadili changamoto zinazozikabili Kamati za Hifadhi ya Mtoto za Wilaya zote za Unguja na Pemba umefanyika. Vile vile, familia 10 zimepatiwa msaada wa kisaikolojia, ushauri nasaha na kupatiwa rufaa kwenda vituo vya Mkono kwa Mkono kwa kupata huduma za afya. Kwa upande wa Pemba, kamati zimefuatilia

katika Vyombo vya Sheria jumla ya kesi 60 za udhalilishaji wa watoto. Pia, Idara imeandaa mikutano ya Kamati za Hifadhi ya Mtoto kwa Wilaya nne za Pemba na ya Kamati ya Kitaifa ya kushughulikia masuala ya Hifadhi ya Mtoto, ili kujadili changamoto, matatizo na jinsi ya kukiimarisha kitengo cha hifadhi ya mtoto Pemba.

- Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kutoka Mahkama mbali mbali Unguja, jumla ya kesi Themanini na Tano (85) za udhalilishaji zimeripotiwa katika kipindi cha Julai 2013 hadi Aprili 2014 Unguja; kati ya kesi hizo, kesi za kubakwa ni Sitini na Saba (67) ambapo kesi nne (4) zimeshatolewa uamuzi, kesi (mbili (2) zimefutwa, kesi mbili (2) zimehukumiwa kifungo na Kesi Sitini na Tatu (63) zinaendelea kusikilizwa. Kesi za kutorosha watoto ni tatu (3) ambazo zote zinaendelea kusikilizwa na kesi za kulawiti ni kumi na tano (15) ambapo kesi mbili (2) zimetolewa uamuzi wa kufutwa na kesi kumi na tatu (13) zinaendelea kusikilizwa. Kwa upande wa Pemba jumla ya kesi 24 zimeripotiwa kutoka Mahkama za Mkoa katika kipindi cha mwezi wa Julai, 2013 hadi Aprili, 2014. Kati ya hizo kesi za kubaka ni kumi na tatu (13), kulawiti tano (5), kutorosha nne (4) na shambulio la aibu mbili (2). Miongoni mwa hizo, kesi tatu (3) zote za kubaka zimeshatolewa hukumu.

- Katika kuimarisha ufuatiliaji wa masuala yanayohusu hifadhi ya watoto, hususan masuala ya ubakaji, Wizara imefanya mikutano miwili ya Kamati ya Hifadhi ya Mtoto inayohusisha Viongozi wa Juu (Mawaziri na watendaji wakuu wa Serikali kutoka Taasisi zinazohusika), ambayo ilijadili mikakati mbalimbali ya kuwalinda watoto dhidi ya udhalilishaji. Vile vile, Wizara imefanya mkutano wa kujadili Kitini cha Kufundishia Masuala ya Hifadhi ya Mtoto na pia kuwajengea uwezo Maafisa Ustawi, Maafisa Wanawake na Watoto na Masheha juu ya jinsi ya kuripoti kesi za udhalilishaji, Unguja na Pemba.

- Kamati za Shehia za kuhudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi katika Shehia mbili za Pemba (Kiuyu Kigongoni na Minungwini Wilaya ya Wete Pemba) zilifuatiliwa na kupatiwa mafunzo juu ya namna ya kuwatambua na kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Aidha, utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi katika maeneo hayo ulifanyika. Pia, ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa, Wizara kwa kushirikiana na *Measure Evaluation* imeandaa Mpango Kazi wa miaka mitatu wa ufuatiliaji na tathmini ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

- Idara imeendelea kuhudumia Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini yenye jumla ya watoto 38. Watoto hao walipatiwa huduma za chakula, afya, vifaa vya skuli na nguo. Aidha, Wizara imeendelea kutoa misaada ya kijamii kwa watu wasiojiweza na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi katika jamii, wakiwemo wazee 163 wanaoishi katika nyumba za wazee Sebleni na Welezo Unguja na Limbani na Makundeni Pemba. Pia, familia 75 Unguja na 55 Pemba zinazoishi katika mazingira magumu zaidi zimepatiwa misaada ya fedha za kujikimu.

- Idara imeanza kufanya utambuzi wa wazee wote wa Zanzibar ili kujua idadi yao halisi na kuweza kupanga mipango bora kwa mujibu wa mahitaji yao. Aidha, Idara iliandaa maadhimisho ya Siku ya Wazee duniani tarehe 01.10.2013 Unguja na Pemba. Katika maadhimisho hayo, Wizara ilisisitiza umuhimu wa jamii kutunza na kuwaenzi wazee, na kuwa jukumu la Serikali ni kuwahudumia wazee ambao hawana wa kuwahudumia kabisa. Pamoja na hayo, Wizara ilizika maiti nane (8) zisizokuwa na wenyewe zilizoripotiwa katika hospitali na maeneo mbalimbali.

- Idara inaendelea na kazi ya kupokea madai na kulipa fidia kwa wafanyakazi wanaopatwa na ajali wakiwa kazini, ambapo kwa mwaka 2013/14 jumla ya wafanyakazi 11 (10 Unguja na mmoja Pemba) walilipwa. Aidha, Wizara bado ina deni kubwa la fidia lililofikia TShs. 96,808,293/= kwa wafanyakazi 89 wa Unguja na Pemba. Fedha hizo zimeshapatikana na watu wote wanaodai madeni hayo wameanza kulipwa. *(Angalia Kiambatanisho 8a na 8b).*

Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Ustawi wa Jamii imejipangia kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuimarisha mfumo wa Hifadhi ya Mtoto ifikapo mwaka 2015;
2. Kuratibu na kufuatilia masuala ya malezi na makuzi ya watoto;
3. Kuimarisha Hifadhi ya Wazee ;
4. Kuendeleza utoaji wa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi ;
5. Kuimarisha Mfumo wa hifadhi ya Jamii ifikapo mwaka 2015; na
6. Kusimamia ulipaji wa fidia kwa watu wanaopatwa na ajali kazini.

Mhe. Spika, ili Idara ya Ustawi wa Jamii iweze kutekeleza vyema malengo yake kwa mwaka 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liiidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Mbili Tisini na Moja na Laki Tano (Tshs. 291,500,000/=) kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MAENDELEO YA VIJANA

Mhe. Spika, katika mwaka 2013/2014, Idara ya Maendeleo ya Vijana ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu uanzishwaji wa Baraza la Vijana;
2. Kuratibu Mpango wa Mikopo kwa Vijana na kuwahamasisha kujiunga na vyama vya ushirika na mikopo;
3. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mpango wa Elimu ya Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya Skuli;
4. Kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa ambapo kilele chake kiliidhinishwa tarehe 14/10/2013 Mkoani Iringa. Wakati wa mbio za mwenge jumla ya miradi ya

5. Kufanya uratibu, ufuatiliaji na uhamasishaji wa vikundi vya vijana;
6. Kuimarisha mashirikiano na uhusiano wa Taasisi za Vijana ndani na nje ya nchi; na
7. Kuendeleza na kuimarisha miundo mbinu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo cha rossela na mbogamboga kwa vijana Unguja na Pemba.

Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Maendeleo ya Vijana kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, katika kufanikisha malengo iliyojiwekea, Idara ya Maendeleo ya Vijana katika mwaka 2013/2014 imeweza kutekeleza yafuatayo:-

- Iliendelea na taratibu za Kisheria za kuanzisha Baraza la Vijana la Zanzibar. Sheria ya kuanzisha Baraza hilo tayari imepitishwa na Baraza lako Tukufu na mchakato wa kuandaa kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria hiyo unaendelea.

- Imeshiriki katika kuratibu Mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana Kitaifa, ambapo kilele chake kiliadhimishwa tarehe 14/10/2013 Mkoani Iringa. Jumla ya miradi ya maendeleo 1,229 yenye thamani ya Shilingi Bilioni Mia Moja Thamanini na Nne, Milioni Mia Tano

Thamanini na Saba, Laki Sita Sitini na Saba, Mia Sita Kumi na Tatu na Senti Arobaini (Tshs. 184,587,667,613.40/=) ilikaguliwa, kuzinduliwa au kuwekewa mawe ya msingi Tanzania nzima. Kati ya hiyo, miradi 78 ilikuwa ya Zanzibar, ambapo kati yao 38 ilikaguliwa, 21 iliwekewa mawe ya msingi na 19 ilizinduliwa. Aidha, jumla ya fedha taslimu kiasi cha Shilingi Milioni Sitini na Sita, Elfu Tisini na Nne, Mia Sita na Arobaini (Tshs.66,094,640/=) zilikusanywa wakati wa Mbio za Mwenge katika Mikoa ya Zanzibar, kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi iliyozinduliwa. *(Angalia Kiambatanisho Namb. 9 na 10).*

- Kupitia Idara hii, Wizara imeshirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya SMT katika kufanya maandalizi ya uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru, uliofanyika tarehe 02/05/2014 katika Wilaya ya Bukoba, Mkoani Kagera. Ujumbe Mkuu wa mwaka huu ni **"Katiba ni Sheria Kuu ya Nchi"**, chini ya kauli mbiu **"Jitokeze kupiga kura ya maoni tupate Katiba mpya iliyo bora"**. Sambamba na ujumbe huo mapambano dhidi ya UKIMWI, Dawa za Kulevya, Rushwa na Malaria umekuwa ni ujumbe wa kudumu unaoendelea kutolewa wakati wa Mbio za Mwenge.

- Idara iliendelea kuratibu utoaji na urejeshaji wa mikopo ya Mfuko wa Vijana, ambapo mikopo 116 imetolewa yenye thamani ya Shilingi Milioni Mia Mbili Arobaini na Tano (Tshs.245,000,000/=) Unguja na Pemba. Aidha, fedha zote zilizokopwa zimesharejeshwa. Hata hivyo, kulijitokeza changamoto ya ucheleweshaji wa marejesho ya mikopo kwa upande wa Pemba, hali iliyopelekea Wizara kwa kushirikiana na Benki ya *CRDB* kuandaa ziara maalumu, ambayo ilifanikisha kurejeshwa kwa fedha za mikopo iliyocheleweshwa, yenye thamani ya Shilingi Milioni Ishirini na Sita (Tshs. 26,000,000/=).

- Katika jitihada za kukuza ajira kwa vijana, Idara imendelea na juhudi za kuwahamasisha vijana Unguja na Pemba kujiunga katika vyama vya ushirika na kuanzisha miradi ya kiuchumi katika sekta za kilimo, uvuvi, ufugaji, biashara na ufundi wa aina mbali mbali. Kufuatia juhudi hizo, vikundi 30 vimeanzishwa katika Wilaya ya Chake Chake na viongozi wake kupatiwa mafunzo ya ujasiriamali. Aidha, mafunzo yalitolewa kwa vijana 60 (40 Unguja na 20 Pemba) katika nyanja za ukuzaji biashara, masoko, utawala na usimamizi wa miradi, ili kuimarisha uzalishaji katika vikundi vyao. Pia, jumla ya vikundi 103 vya Vijana vilitembelewa na kupewa ushauri na maelekezo ya jinsi ya kuendesha miradi yao *(Angalia Kiambatanisho Namb. 11).* Vile vile, kwa kushirikiana na SACCOS ya Vijana Pemba, jumla ya vikundi 55 vya ujasiriamali vya vijana vilihamasishwa juu ya umuhimu wa kujiunga na SACCOS hiyo ili waweze kupata mikopo yenye masharti nafuu, kwa lengo la kuweza kuimarisha na kuendeleza shughuli zao za uzalishaji *(Angalia Kiambatanisho Namb. 12).*

- Katika kuimarisha mashirikiano na uhusiano wa Taasisi za Vijana ndani na nje ya nchi, Vijana wanne (4) wameshiriki katika Mikutano ya Vijana huko Austria na Misri. Aidha, kwa kushirikiana na Shirika la UVIKIUTA, vijana wa Zanzibar kwa kushirikiana na vijana wa Tanzania Bara, walipatiwa mafunzo ya uongozi wa kambi za kimataifa za vijana, ambazo madhumuni yake ni kuhamasisha vijana juu ya uzalendo na kuipenda nchi yao, kubadilishana mawazo juu ya changamoto mbalimbali zinazowakabili vijana na namna ya kukabiliana nazo. Kupitia makambi haya, vijana hushiriki katika shughuli za ujenzi wa taifa katika miradi ya jamii kama vile ujenzi wa skuli, vituo vya afya na uhifadhi wa mazingira.

- Wizara kwa kushikiana na Shirika la Idadi ya Watu Duniani *(UNFPA)* na Tume ya UKIMWI Zanzibar, imeandaa Kitini na Muongozo wa Mafunzo ya Stadi za Maisha kwa Vijana. Kitini na Muongozo huo vimefanyiwa majaribio kwa maandalizi ya mwisho ya kutumika rasmi. Muongozo huu utasaidia kutoa elimu kwa vijana, itakayowasaidia kujitambua na kuepukana na changamoto wanazokabiliana nazo.

- Ili kuyaimarisha mashamba ya mauwa na mbogamboga ya vijana Tunguu, Unguja na Mbuzini, Pemba, Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Vijana, imeendelea na taratibu za uwekaji wa miundo mbinu. Hii ni pamoja na kuweka miundombinu ya umwagiliaji majii kwa kutumia mfumo wa "drip irrigation", pamoja na "green house" mbili kwa Unguja. Kwa upande wa Pemba, Wizara inaendelea na hatua za uimarishaji miundo mbinu, ambapo imeweza kumalizia utiaji wa milango na madirisha ya kibanda cha kuwekea pampu ya maji. Lengo kwa upande wa Pemba ni kuweka "green house" kama Tunguu. Kwa hivi sasa vijana wanalitumia shamba hilo la Mbuzini kwa kulima mpunga.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Maendeleo ya Vijana imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Vijana;
2) Kuratibu na kufuatilia uanzishwaji wa Baraza la Vijana;
3) Kuratibu mbio za Mwenge wa Uhuru na Wiki ya Vijana kitaifa;
4) Kuwahamasisha, kuwaandaa na kuwaunganisha vijana na fursa mbali mbali za kiuchumi zilizopo;
5) Kuratibu utekelezaji wa Kitini na Muongozo wa Stadi za Maisha kwa Vijana walio nje ya Skuli;
6) Kufanya ufuatiliaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii za vijana; na
7) Kuimarisha ushirikiano na taasisi zinazoshughulikia masuala ya vijana ndani na nje ya nchi.

Mhe. Spika, ili Idara ya Vijana iweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Sabini na Tatu, Laki Tano na Elfu Thelathini na Tatu (Tshs. 73,533,000/=) kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO

Mhe. Spika, kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2013/2014, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na kusimamia haki za wanawake na watoto;
2. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mtoto;
3. Kuimarisha uratibu wa shughuli za kiuchumi na maendeleo ya wanawake na watoto;
4. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa mambo yanayohusu wanawake na watoto.

Utekelezaji wa malengo ya Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto kwa mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, utekelezaji wa malengo ya Idara hii kwa mwaka 2013/2014 ulikuwa kama ifuatavyo:-

- Katika kuratibu na kusimamia, haki za wanawake na watoto, Kamati ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto imeanzishwa. Kamati hiyo imejumuisha wawakilishi 30 kutoka katika taasisi za Serikali na zisizo za Serikali. Tayari Kamati hiyo imeanza kazi na imekuwa ikiendesha mikutano ya kujadili masuala mbali mbali yanayohusu hali na ustawi wa watoto wa Zanzibar**.**
- Wizara kupitia Idara hii, imetayarisha nyenzo za mawasiliano za masuala ya udhalilishaji wa watoto na kuzifanyia mapitio kwa kuwashirikisha wadau wa masuala ya watoto wakiwemo wanafunzi, walimu na wazazi wa Mkoa wa Kaskazini Unguja. Pia, Wizara imetayarisha Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao utasaidia upatikanaji wa taarifa na takwimu zinazohusu haki za watoto.

- Idara imeendelea kuyapokea, kuyashughulikia na kuyapatia ufumbuzi malalamiko yanayohusu wanawake, ambapo kwa mwaka 2013/2014 jumla ya malalamiko 119 (Unguja24 na Pemba 95) yalipokelewa na kupatiwa ushauri na maelekezo yanayofaa. Malalamiko hayo yalihusu kupigwa, kupewa ujauzito, kubakwa, kutelekezwa na mume, kuunguzwa moto, madai ya fedha na madai ya nyumba *(Angalia Kiambatanisho Namb.13a, 13b).*

- Idara iliratibu maandaalizi ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo huadhimishwa kila mwaka ifikapo mwezi wa Machi. Kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka 2014 ilikuwa ni **"ONGOZA MABADILIKO KWA MAENDELEO YA WANAWAKE"**. Kwa upande wa Zanzibar, maadhimisho hayo yalihusisha shughuli mbali mbali zikiwemo: Kuandaa vipindi vya redio na Televisheni; Kufanya usafi wa mazingira katika nyumba za wazee Sebleni; Kuendesha makongamano katika Wilaya za Kusini na Mjini; Maonesho ya kazi za Sayansi kwa wanafunzi wanawake; na Kufanya uhamasishaji wa upimaji na uchangiaji wa damu salama. Siku ya Kilele (tarehe 08 Machi, 2014), kuliendeshwa Kongamano la Wanawake, ambapo washiriki walipata fursa ya kujadiliana juu ya hali ya Wanawake katika nyanja za kuchumi, kisiasa, kijamii na afya, pamoja na udhalilishaji wa kijinsia.

- Katika kupiga vita vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake, Umoja wa Mataifa umeweka siku 16 maalum (kuanzia tarehe 25 Novemba hadi tarehe 10 Disemba ya kila mwaka) kwa nchi wanachama kufanya kampeni na kuhamasisha jamii juu ya kupambana na vitendo hivyo. Kwa Unguja, kampeni hiyo iliendeshwa kwa kuandaa kongamano la siku moja lililowashirikisha wadau kutoka taasisi za Serikali na zisizo za Serikali. Kwa upande wa Pemba, Wizara ilishirikiana na *SOS* kuandaa maandamano na mkutano wa hadhara iliyohusisha, pamoja na mambo mengine, mabango yenye ujumbe wa kupinga udhalilishaji, michezo ya kuigiza na hotuba za viongozi. Kwa mwaka 2014, kampeni hii iliendeleza ujumbe unaosema **"AMANI YA DUNIA HUANZA NYUMBANI; TUPINGANE NA VITENDO VYA UTUMIAJI WA NGUVU DHIDI YA WANAWAKE NA WATOTO"**.

- Idara imeratibu uanzishwaji wa Mabaraza ya Watoto 38 ya Shehia (Unguja 29 na Pemba 9) ili kuinua ushiriki wa watoto katika mambo yanayowahusu. Kwa Unguja Mabaraza hayo yameanzishwa katika Wilaya za Kaskazini 'B' (8), Kaskazini 'A' (1), Mjini (10) na Kati (10) na kwa Pemba yameanzishwa katika Wilaya za Wete (3) na Mkoani (6). Mabaraza haya yanasaidia watoto kujua haki zao na kusaidia kuripoti matukio mbali mbali yanayohusu watoto. Mabaraza mawili ya watoto ya Wilaya ya Magharibi katika maeneo ya Mwanakwerekwe na Welezo yamekaguliwa ili kuangalia utendaji wao. Hali ya Mabaraza ya Watoto imeonesha kuwa yamekuwa yakikosa ushirikianao kutoka kwa viongozi, wakiwemo Madiwani, Wabunge na Wawakilishi katika maeneo yao. Aidha, kwa upande wa Pemba Mabaraza kumi na moja (11) yametembelewa kuangalia utendaji wake, ambapo ilibainika kuwa yanaendelea vizuri, watoto wanasaidiana na wanatoa taarifa juu ya mambo yanayohusu watoto yanayotokezea katika shehia zao.

- Katika Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mtoto, Idara imeendesha mafunzo juu ya ushughulikiaji wa masuala ya watoto wanaokinzana na Sheria. Mafunzo hayo yalitolewa kwa watendaji 53 kutoka taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazoshughulikia masuala ya watoto. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoto wanaokinzana na sheria wanashughulikiwa katika ngazi ya jamii, badala ya utaratibu wa kimahkama uliopo sasa, ikizingatiwa suala zima la kulinda haki zao za msingi kama ilivyoelekezwa katika Mkataba wa Haki za Mtoto.

- Idara pia imesimamia uandaaji wa Mkakati wa Haki za Mtoto (2013-2018) pamoja na Mpango wa Utekelezaji kwa mwaka 2014. Uandaaji wa Mkakati huo pamoja na Mpango wake wa

utekelezaji ulishirikisha taasisi nyengine zinazohusika, zikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka, Mahkama, Vyuo vya Mafunzo, Polisi, na Taasisi zisizo za Serikali. Aidha, Wizara imeandaa kanuni kwa ajili ya uendeshaji wa Mahkama ya Watoto kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki za watoto.

- **K**wa kushirikiana na *UNICEF*, Wizara imo katika hatua za kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Masuala ya Haki za Kisheria za Mtoto *(Child Justice Monitoring and Evaluation Framework).* Mfumo huu, pamoja na mambo mengine, utawezesha Wizara kufahamu kesi za watoto zilizopo na hatua zilizofikiwa katika Mahkama, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Polisi. Aidha, utawezesha kujua kama mfumo wa sheria unazingatia ipasavyo masuala ya haki za watoto, kama yalivyoainishwa katika Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watoto na Mkataba wa Afrika kuhusu haki za Watoto.

- Kupitia Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto, juhudi za kuviimarisha vikundi vya kiuchumi vya wanawake zimeendelezwa. Jumla ya vikundi 70 vilitembelewa kwa lengo la kutathmini mahitaji na maendeleo yao, pamoja na kuona changamoto zinazowakabili ili kuwapatia ushauri unaofaa kwa ajili ya kuimarisha shughuli zao za kiuchumi *(Angalia Kiambatanisho Namb. 14).* Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko imeviwezesha vikundi 49 vya wajasiriamali wanawake (42 Unguja na 7 Pemba) kushiriki katika Maonesho ya 36 ya Sabasaba, kwa lengo la kutangaza biashara zao. Vile vile, mafunzo ya ujasiriamali na namna ya kutafuta masoko yametolewa kwa Waratibu wa Shehia 99 wa shughuli za wanawake na watoto katika Wilaya za Kaskakazini A, Magharibi na Kati Unguja, ili waweze kutoa mafunzo kwa vikundi vilivyopo katika maeneo yao. Kwa upande wa Pemba, tathmini ya vikundi vya ujasiriamali vya wanawake imefanywa katika Shehia 33 za Mkoa wa Kaskazini (21 Wete na 11 Micheweni) kwa lengo la kupata taarifa sahihi za vikundi hivyo. Taarifa hizo zitatumika katika kuandaa mipango ya kuviimarisha vikundi hivyo. *(Angalia Kiambatanisho Namb. 15).*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

1. Kuratibu na kusimamia haki za wanawake na watoto;
2. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mtoto;
3. Kuimarisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za kiuchumi, kijamii na maendeleo ya wanawake na watoto;
4. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Mabaraza ya Watoto;
5. Kuimarisha mashirikiano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa mambo yanayohusu wanawake na watoto; na
6. Kuratibu na kusimamia mapambano dhidi ya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Spika, ili Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto iweze kutekeleza malengo yake kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Sitini, Laki Saba na Elfu Sitini na Tatu (Tshs. 60,763,000/=) kwa kazi za kawaida na Shilingi Milioni Mia Moja Tisini na Tano na Laki Sita (Tshs.195,600,000/=) kwa kazi za Maendeleo.

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba inasimamia shughuli zote za Wizara kwa upande wa Pemba, ikiwemo utekelezaji wa majukumu ya Idara mbali mbali za Wizara. Hivyo, utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2013/2014 pamoja na malengo kwa mwaka 2014/2015 kwa Ofisi hii, ni kama ilivyoainishwa katika Idara husika, ambazo maelezo yake yamehusisha pia na Pemba.

Mhe. Spika, ili Ofisi Kuu Pemba iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, naliomba Baraza lako Tukufu liidhinishe jumla ya Shilingi Milioni Mia Tatu Thelathini na Nane, Laki Tano na Elfu Hamsini (Tshs. 338,550,000/=) kwa Kazi za Kawaida na Shilingi Milioni Mia Nne Hamsini na Thelathini na Sita Elfu (Tshs. 450,036,000/=) kwa ajili ya mishahara, mchango wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na maposho ya wafanyakazi.

HITIMISHO

Mhe. Spika, tunatambua na kuthamini sana michango ya Washirika wa Maendeleo katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Napenda nichukue nafasi hii adhimu, kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya zanzibar, kuwashukuru sana washirika wetu wa maendeleo kwa mashirikiano waliyotupa katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana, wanawake, watoto, wazee na wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Washirika hao ni pamoja na nchi wahisani, ikiwemo Umoja wa Ulaya, India na Jamhuri ya Watu wa China na Mashirika ya Kimataifa, ikiwemo *UNFPA, UNICEF, UNESCO, UNDP, ILO, SAVE THE CHILDREN, FHI,* Tunajali Program, CHAI, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, pamoja na Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na Jumuiya ya Madola.

Mhe. Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Wizara pia ilishirikiana na Wizara na taasisi nyengine za Serikali pamoja na zisizo za Serikali, ikiwemo sekta binafsi. Napenda kuchukua fursa hii kuzishukuru taasisi hizo kwa mashirikiano waliyotupa na naziomba tuendelee kushirikiana, ili kwa pamoja tuweze kufikia malengo tuliyopanga kwa maslahi ya wananchi na Taifa letu kwa jumla.

Mhe. Spika, natoa shukrani maalum kwa Ofisi za Mikoa, Wilaya na Shehia kwa mchango wao katika usimamizi na ufuatiliaji wa masuala mbali mbali yanayohusu Wizara kwenye maeneo yao, ikiwa pamoja na masuala ya kupiga vita udhalilishaji wa wanawake na watoto. Pia natoa shukrani kwa taasisi za kiraia ambazo zimechangia katika juhudi za Serikali za kuimarisha ustawi na maendeleo ya vijana, wanawake, watoto, wazee na wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Taasisi hizo ni pamoja na ZAYEDESA, *ZACA*, ZAIADA, ZAWDO, ZAFELA, ZAWCO, ZAMWASO, ZANGOC, ZLSC, COWPZ, PIRO, UVIKIUTA, UWT, ACTION AID, WEDTF, TAWLA, TAMWA, CHANGAMOTO, PRIDE, TMC na TGNP. Shukurani zangu pia ziende kwa taasisi za kifedha, ikiwemo BOT, PBZ, CRDB, FBME, na Benki ya Posta kwa mashirikiano yao mazuri kwa Wizara, hususan kwenye program za uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, vyombo vya habari navyo vimetoa mchango mkubwa katika utekelezaji wa shughuli zetu, ikiwemo kutangaza matukio mbali mbali yaliyohusu Wizara, pamoja na kuelimisha jamii juu ya masuala ambayo Wizara inayafanyia kazi, ikiwemo programu za kupinga vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Hivyo, nachukuwa fursa hii kuwapongeza viongozi na watendaji wa vyombo hivyo vya habari, vikiwermo redio, televisheni na magazeti kwa mashirikiano yao kwa Wizara.

Mhe. Spika, yote ambayo nimeyaeleza yametekelezwa kwa shirikiano mkubwa wa Watendaji Wakuu na Wafanyakazi wote wa Wizara. Napenda kuwashukuru na kuwapongeza Wafanyakazi wote wa Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kuanzia Katibu Mkuu Nd. Asha Ali Abdulla, Manaibu Katibu Wakuu Nd. Ali Khamis Juma na Nd. Msham Abdalla Khamis, Wakurugenzi, Ofisa Mdhamini pamoja na Maafisa wafanyakazi wa ngazi zote kwa kufanya kazi kwa umakini na juhudi kubwa. Mashirikiano haya yamepelekea kutekeleza malengo na majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, nawaomba waendeleze umoja, mashirikiano, mshikamano, upendo na nidhamu ili tuweze kufanikisha vyema malengo yetu kwa mwaka wa fedha unaokuja na itakayofuata.

Mhe. Spika, Ili Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto iweze kutekeleza malengo na majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kwa heshima na taadhima nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yako wapokee, wajadili, watupe ushauri na maelekezo na hatimae wapitishe na kuidhinisha matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Saba, Milioni Mia Tano

Sabini, Laki Sita na Elfu Sabini (Tshs. 7,570,670,000/=). Kati ya hizo, Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Moja Hamsini na Tano na Laki Mbili (Tshs. 2,155,200,000/=) ni kwa ajili ya mishahara, michango ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na maposho maalum kwa wafanyakazi; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Nne Thamanini na Tano na Laki Nane (Tshs. 1,485,800,000/=) ni kwa matumizi mengineyo; Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Tano na Elfu Ishirini na Nne (Tshs. 1,524,000,000/=) ni kwa kazi za Maendeleo na Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne na Tano, Laki Sita na Elfu Sabiini (Tshs. 2,405,670,000/=) ni fedha zilizoahadiwa kutolewa na Washirika wa Maendeleo *(Angalia Kiambatanisho Namb. 16).* Pia naomba idhini ya kukusanya mapato ya Shilingi Milioni Kumi (Tshs. 10,000,000/=) kupitia usajili na ukaguzi wa vyama vya ushirika kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

VIAMBATANISHO

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI

Kiambatanisho Nam 1a

MCHANGANUO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA 2013/2014

FUNGU	IDARA	MAKADIRIO YA 2013/2014			KILICHOPATIKANA JULAI, 2013 - MEI, 2014			ASILIMIA YA M/MENGINEO	ASILIMIA YA FEDHA ZOTE
		JUMLA	MISHAHARA	M/MENGINEO	JUMLA	MISHAHARA	M/MENGINEO		
03	**A/KUU PEMBA**	472,008,000	212,008,000	260,000,000	427,987,950	289,503,950	138,484,000	53	91
04	**M/S/UTAFITI**	318,446,000	98,446,000	220,000,000	187,033,639	91,166,277	95,867,362	44	59
05/01	**W/WATOTO**	220,568,000	103,568,000	117,000,000	123,040,838	90,668,038	32,372,800	28	56
05/02	**MIKOPO**	296,284,000	98,110,000	198,174,000	187,785,816	107,391,333	80,394,483	41	63
07	**M/VIJANA**	272,557,000	75,557,000	197,000,000	132,458,132	79,889,222	52,568,910	27	49
09	**UWEZESHAJI**	158,180,000	71,209,000	86,971,000	85,714,193	54,626,111	31,088,082	36	54
1101	**U/JAMII**	687,825,000	347,825,000	340,000,000	564,751,491	351,128,605	213,622,886	63	82
10	**USHIRIKA**	234,767,000	178,890,000	55,877,000	192,888,994	164,947,494	27,941,500	50	82
12	**U/UENDESHAJI**	588,987,000	368,987,000	220,000,000	593,688,947	443,389,796	150,299,151	68	101
JUMLA:		**3,249,622,000**	**1,554,600,000**	**1,695,022,000**	**2,495,350,000**	**1,672,710,826**	**822,639,174**	**49**	**77**

Kiambatanisho Nam 1b

MCHANGANUO WA FEDHA ZA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

FUNGU	IDARA	MAKADIRIO YA 2013/2014			KILICHOPATIKANA JULAI, 2013 - MEI, 2014			ASILIMIA YA FEDHA ZOTE
		JUMLA	SERIKALI	WAHISANI	JUMLA	SERIKALI	WAHISANI	
03	**A/KUU PEMBA**	-	-	-		-	-	-
04	**M/S/UTAFITI**	401,200,000	10,000,000	391,200,000	177,475,000	-	177,475,000	44
05/01	**W/WATOTO**	958,800,000	150,000,000	808,800,000	104,629,000	40,000,000	64,629,000	11
05/02	**MIKOPO**	-		-	-	-	-	-
07	**M/VIJANA**	-	-	-	-	-	-	-
09	**UWEZESHAJI**	-	-	-	-	-	-	-
1101	**U/JAMII**	520,000,000	360,000,000	160,000,000	260,188,000	100,000,000	160,188,000	50
1102	**U/JAMII-PBA**	-			-			-
10	**USHIRIKA**	-	-	-		-	-	-
12	**U/UENDESHAJI**	-	-	-	-	-	-	-
JUMLA:		**1,880,000,000**	**520,000,000**	**1,360,000,000**	**542,292,000**	**140,000,000**	**402,292,000**	**29**

Kiambatanisho Namb. 2a

AJIRA MPYA, UHAMISHO, WALIOFARIKI DUNIA NA WALIOACHA KAZI UNGUJA NA PEMBA 2014/2015

AINA	UNGUJA			PEMBA			JUMLA KUU		
	W/KE	W/ME	JUMLA	W/KE	W/ ME	JUMLA	W/KE	W/ME	JUMLA
AJIRA MPYA	4	9	**13**	0	0	**0**	4	9	**13**
AJIRA KWA NJIA YA UHAMISHO	1	1	**2**	0	0	**0**	1	1	**2**
WALIOHAMISHWA TAASISI NYENGINE ZA SMZ	8	1	**9**	0	0	**0**	8	1	**9**
WALIFARIKI DUNIA	2	1	**3**	0	0	**0**	2	1	**3**
WALIOSTAAFU KISHERIA	5	4	**9**	0	1	**1**	0	1	**10**
WALIOACHA KAZI	2	0	**2**	0	0	**0**	2	0	**2**
JUMLA KUU	**22**	**16**	**38**	**0**	**1**	**1**	**17**	**13**	**39**

Kiambatisho Namb. 2b

MAFUNZO YA MUDA MREFU NA MFUPI KWA WAFANYAKAZI KWA MWAKA 2013/2014

AINA YA MAFUNZO	UNGUJA			PEMBA			JUMLA KUU
	W/KE	W/ME	JUMLA	W/KE	W/ME	JUMLA	
MUDA MREFU	12	9	**21**	6	2	**8**	**29**
MUDA MFUPI	2	-	**2**	1	1	**2**	**4**
JUMLA	**14**	**9**	**23**	**7**	**3**	**10**	**33**

Kiambatanisho Namb. 3

VIKUNDI VYA WAJASIRIAMALI VILIVYOFANYIWA UFUATILIAJI NA KUPATIWA USHAURI UNGUJA NA PEMBA KWA MWAKA 2013/2014

UNGUJA

NO	JINA LA KIKUNDI	AINA YA BIASHARA
1	Hand craft making	Utengenezaji wa mabakuli na maua kwa kutumia mifuko ya Plastiki
2	ZAYDAT & BASMA	Sabuni za Viuongo na Madawa
3	Mosquito Net	Ushonaji Vyandarua na Mapazia
4	Tujitegemee	Utengenezaji wa Viatu vya ngozi
5	Jambo Spice	Viungo
6	Man Group	Utengenezaji wa madawa ya kiasili
7	Kheri liwe	Uvuvi na usarifu wa dagaa
8	Hatwendi kwa chuki	Usarifu wa mazao ya Kilimo
9	Tusijitenge	Utengenezaji wa Vyakula vikavu
10	Vijana Tuwe Mbele	Mikufu ya kalenda za karatasi

PEMBA

NO	JINA LA KIKUNDI	AINA YA BIASHARA
1	Jiendeleze kwa maisha bora	Utengenezaji wa mazulia
2	JUKUNUM	Uzalishaji wa Asali
3	Haturudi Nyuma	Utengenezaji wa makawa mikoba, Mikeka na sabuni
4	Kichakaa Si Shangi	Uzalishaji wa Chumvi
5	Tusishindwe	Utengenezaji wa Sabuni
6	Tushikamane	Utengenezaji wa Sabuni
7	Nia Njema	Utengenezaji wa Asali Mishumaa na chakula cha Lishe
8	Gando women development Association	Utengenezaji wa Viungo na bidhaa za kutumia unga wa muhogo
9	Juama	Utengenezaji wa Madawa Sabuni na ufumaji
10	Umaskini kujitakia	Utengenezaji wa makawa na Vipepeo

Kiambatanisho Namb. 4

UTOAJI WA MIKOPO KUPITIA MFUKO WA KUJITEGEMEA JULAI,2013 HADI MACHI,2014

NA	WILAYA	JINSIA		JUMLA	VIKUNDI	FEDHA
		W'KE	W'ME			
1	MJINI	28	30	58	7	37,500,000.00
2	MAGHARIBI	53	41	94	14	57,177,000.00
3	KASKAZINI "A"	19	29	48	7	32,300,000.00
4	KASKAZINI "B"	43	32	75	13	32,850,000.00
5	KUSINI	19	12	31	6	28,000,000.00
6	KATI	10	12	22	6	24,050,000.00
	JUMLA NDOGO	**172**	**156**	**328**	**53**	**211,877,000.00**
7	MKOANI	11	11	22	3	18,000,000.00
8	CHAKE CHAKE	40	80	120	17	25,500,000.00
9	WETE	20	20	40	4	19,400,000.00
10	MICHEWENI	20	20	40	9	20,100,000.00
	JUMLA NDOGO	**91**	**131**	**222**	**33**	**83,000,000.00**
	JUMLA KUU	**263**	**287**	**550**	**86**	**294,877,000.00**

Kiambatanisho Namb. 5

UTOAJI NA UREJESHAJI WA MIKOPO KUPITIA MFUKO WA JK/AK JULAI 2013 HADI FEBRUARI 2014.

UNGUJA						
MKOA	**WILAYA**	**IDADI YA MIKOPO**	**FEDHA ZILIZOKOPWA**	**FEDHA ZILIZOLIPWA HADI MACHI,2014**	**DENI LILILOSALIA HADI MACHI.2104**	**MALIPO KUANZIA JULAI,2013 HADI MACHI,2014**
KASKAZINI						
	KASKAZINI "A"	58	103,800,000.00	73,537,740.00	30,262,260.00	682,740.00
	KASKAZINI "B"	59	166,388,575.00	88,510,912.00	77,877,663.00	494,694.00
JUMLA		**117**	**270,188,575.00**	**162,048,652.00**	**108,139,923.00**	**1,177,434.00**
KUSINI						
	KATI	23	53,700,000.00	31,006,827.00	22,693,173.00	879,916.00
	KUSINI	84	139,200,000.00	92,531,585.00	46,668,415.00	3,458,283.00
JUMLA		**107**	**192,900,000.00**	**123,538,412.00**	**69,361,588.00**	**4,338,199.00**
M/MAGHARIBI						
	MAGHARIBI	159	392,770,000.00	216,572,225.00	176,197,775.00	4,288,656.00
	MJINI	153	219,406,256.00	118,591,786.00	100,814,470.00	7,510,854.00
JUMLA		**312**	**612,176,256.00**	**335,164,011.00**	**277,012,245.00**	**11,799,510.00**

JUMLA NDOGO	**536**	**1,075,264,831.00**	**620,751,075.00**	**454,513,756.00**	**17,315,143.00**
PEMBA					
KASKAZINI					
WETE	47	104,270,000.00	41,661,126.00	62,608,874.00	1,049,219.00
MICHEWENI	49	84,500,000.00	35,625,490.00	48,874,510.00	3,538,212.00
JUMLA	**96**	**188,770,000.00**	**77,286,616.00**	**111,483,384.00**	**4,587,431.00**
KUSINI					
MKOANI	41	62,600,000.00	46,909,043.00	15,690,957.00	1,737,901.00
CHAKE CHAKE	83	226,850,000.00	129,960,992.00	96,889,008.00	7,040,003.00
JUMLA	**124**	**289,450,000.00**	**176,870,035.00**	**112,579,965.00**	**8,777,904.00**
JUMLA NDOGO	**220**	**478,220,000.00**	**254,156,651.00**	**224,063,349.00**	**13,365,335.00**
JUMLA KUU	**756**	**1,553,484,831.00**	**874,907,726.00**	**678,577,105.00**	**30,680,478.00**

Kiambatanisho Namb. 6 MAREJESHO YA FEDHA ZA MKOPO KUPITIA MFUKO WA KUJITEGEMEA JULAI,2013 - MACHI,2014

WILAYA	JULAI	AUG	SEPT	OKT	NOV	DEC	JAN	FEB	MACH	APRIL	JUMLA

MJINI	1,561,000	2,559,000	2,502,000	2,077,000	824,000	2,858,700	1,664,000	1,847,000	2,070,250	2,951,500	**20,914,450**
M/GH	1,792,500	3,149,500	2,228,500	1,784,000	1,171,000	666,000	1,341,200	2,218,500	3,270,250	1,938,500	**19,559,950**
KASK/A	1,264,400	1,068,500	1,688,500	1,134,000	1,186,000	749,500	1,542,500	1,873,000	1,212,000	1,772,000	**13,490,400**
KASK/B	702,500	792,000	865,000	625,000	420,500	502,000	385,000	705,600	968,000	720,000	**6,685,600**
KUSINI	1,615,000	1,404,500	1,185,500	1,153,000	1,051,000	2,345,500	1,815,500	1,115,000	1,222,500	980,000	**13,887,500**
KATI	860,000	998,500	953,700	958,500	512,000	516,500	662,500	1,294,000	786,500	978,500	**8,520,700**
MKOANI	441,000	505,000	307,000	714,000	335,000	400,000	527,000	600,000	510,000	490,000	**4,829,000**
CHAKE	1,157,500	1,649,500	817,500	1,292,500	1,226,000	720,000	1,246,500	814,000	900,000	1,265,000	**11,088,500**
WETE	772,000	1,156,000	1,215,000	1,101,500	602,000	115,000	1,416,500	486,000	566,000	729,000	**8,159,000**
MICHEW	260,000	597,000	461,000	705,000	455,000	150,000	615,000	327,000	50,000	350,000	**3,970,000**
JUMLA	**10,425,900**	**13,879,500**	**12,223,700**	**11,544,500**	**7,782,500**	**9,023,200**	**11,215,700**	**11,280,100**	**11,555,500**	**12,174,500**	**111,105,100**

Kiambatanisho 7a

RIPOTI YA UDHALILISHAJI UNGUJA JULAI 2013 -MACHI 2014

SNO	AINA YA UDHALILISHAJI	W/WAKE	W/UME	JUMLA
1.	**KUBAKWA**	12	0	12
2.	**KULAWITIWA**	2	1	3
3.	**MIMBA**	2	0	2
4.	**KUKASHFIWA**	2	0	2
	JUMLA	**18**	**1**	**19**

RIPOTI YA KITENGO CHA ONE STOP CENTER –UNGUJA,JULAI 2013-MACHI 2014

AINA YA TUKIO	CHINI YA 18	ZAIDI YA 18	M/KE	M/MME	JUMLA
KUBAKWA	331	17	501	0	849
KULAWITIWA	25	1	4	36	66
MIMBA	127	26	225	0	378
KUTOROSHWA	20	3	20	0	43
KUKASHIFU	280	28	418	0	726
SHAKA YA KULAWITIWA	33	0	111	33	177
JUMLA	**816**	**75**	**1279**	**69**	**2239**

Kiambatanisho 7b

RIPOTI YA KITENGO CHA ONE STOP CENTER –PEMBA, JULAI 2013-MACHI 2014

PEMBA

		KUSINI				**KASKAZINI**				**WATOTO**		**WATU WAZIMA**		**KESI/POLISI**	**KESI MHAKAMANI**	**MAELEZO**
SHUGHULI	**IDADI YA KESI**	**CHAKE CHAKE**		**MKOANI**		**WETE**		**MICHEWENI**								
		ME	**KE**	**ME**	**KE**	**ME**	**KE**	**ME**	**KE**	**ME**	**KE**	**ME**	**KE**			
Kubaka	43	-	31	-	4	-	4	-	4	-	43	-	-	43	3	17 MIMBA ZA UTOTONI
Kulawiti	6	5	-	-	-	-	-	1	-	6	-	-	-	6	2	
Kutorosha	23	1	19	-	1	-	2	-	-	1	12	-	10	23	3	
Shambulio la kuumiza mwili	7	1	6	-	-	-	-	-	-	1	2	-	4	7	2	
Shambulio la aibu	4	1	3	-	-	-	-	-	-	1	3	-	-	4	-	
Kumpa mimba msichana asiyepata kuolewa	15	-	14	-	-	-	1	-	-	-	-	5	10	15	-	
JUMLA	**98**	**8**	**73**	**-**	**5**	-	**7**	1	**4**	**9**	**60**	**5**	**24**	**98**	**10**	

Kiambatanisho Nam. 8a

WADENI WA FIDIA UNGUJA NA PEMBA

ENEO	WATU	DENI
Unguja	41	31,617,537
Pemba	48	65,190,756
Jumla	89	96,808,293

Kiambatanisho Nam. 8b

MALIPO YA FIDIA JULY 2013-MARCH 2014 UNGUJA NA PEMBA

ENEO	Idadi ya waliolipwa	Kiasi kilicholipwa
Unguja	10	4,000,000
Pemba	1	608,646
Jumla	11	4,608,646

Kiambatanisho Nam: 9

MIRADI ILIYOPITIWA NA MWENGE

MKOA WA MJINI MAGHARIBI

	JINA LA MRADI	**PAHALA**
1.	Uzinduzi wa maji safi na salama	Amani kwa Bopar
2.	Kutembelea kituo cha afya	Mpendae
3.	Uzinduzi wa programm ya uhifadhi maeneo yaliyoathirika kimazingira.	Kwahani Uwanja wa Farasi.
4.	Kutembelea mradi wa utengenezaji wa gati.	Malindi.
5.	Kutembelea mradi wa uimarishaji Polisi Jamii.	Malindi.
6.	Kutembelea na kuhamasisha wananchi Saccoss Bank.	Kikwajuni.
7.	Kutembelea historia ya Magofu.	Maruhubi.
8.	Kutembelea kazi za mikono kikundi cha Tusifarikiane.	Miembeni
9.	Uzinduzi wa Barabara ya kifusi.	Nyamazi.
10.	Uzinduzi wa kisima cha maji safi na salama.	Dimani.
11.	Uwekaji jiwe la msingi Kituo cha afya.	Kianga.
12.	Kutembelea mradi wa mbogamboga	Kombeni.
13.	Kutembelea vikundi vya ushirika.	Bweleo.

MKOA WA KASKAZINI UNGUJA

	JINA LA MRADI	**PAHALA**
1.	Ujenzi wa Hospitali	Pwani mchangani
2.	Upimaji wa afya kwa hiari	Matemwe.
3.	Ujenzi wa skuli.	Mfuru matonga.
4.	Upandaji miti kuhifadhi vyanzo vya maji.	Kiweshange.
5.	Ujenzi wa skuli ya awali	Kibuyuni.
6.	Elimu ya mapambano dhidi ya Dawa za kulevya.	Mkwajuni.
7.	Ujenzi wa kituo cha kuhifadhia mitihani.	Mkwajuni.
8.	Utoaji wa mikopo.	Mkokotoni.
9.	Ufugaji kuku.	Makoba.
10.	Upandaji miti.	Mafufuni.
11.	Ujenzi wa banda la skuli ya msingi.	Pangeni
12.	Ujenzi wa banda la kinu cha kusagia nafaka.	Kilombero.

MKOA WA KUSINI UNGUJA

	JINA LA MRADI	**PAHALA**
1.	Chuo cha Wajasiriamali Vijana	Dunga Jumba la Mawe
2.	Vikundi vya Kinamama Weza	K/Mwembeshauri
3.	Ujenzi wa Banda la Madrasa	Pongwe Mwera
4.	Kisima cha Umwagiliaji maji	Koani
5.	Banda la mitihani	Michavi
6.	Kituo cha Afya	Paje
7.	Chumba cha Komputa	Jambiani
8.	Chumba cha Komputer na Maktaba	Mtende
9.	Ushirika wa Migomba na mazao	Mzuri – Makundichi
10.	Ushirika wa kupanda miti	Kiongoni – Makunduchi

MIRADI NA THAMANI YA FEDHA KIMKOA

	JINA LA MRADI	PAHALA ULIPO	SHUGHULI	THAMA
1	Mradi wa uvuvi bwawa la samaki	Chokocho	Ukaguzi na uzinduzi	75,000,00
2	Mradi wa upandaji miti kwa ajili ya kuhifadhi mazingira	JKU Chokocho	Ukaguzi na uzinduzi	-
3	Mradi wa kilimo cha migomba	Chokocho	Kuweka jiwe la kumbu kumbu	10,000,00
4	Ujenzi wa uwanja wa mikutano ya kijamii	Chokocho	Uzinduzi	17,500,00
5	Ujenzi wa skuli ya msingi	Chokocho	Uwekaji wa jiwe la msingi	13,000,00
6	Ujenzi wa nyumba bora	Kandarani	Uwekaji wa jiwe la msingi	
	WILAYA YA MKOANI			
7	Mafunzo ya UKIMWI na Madawa ya kulevya	Skuli ya Mkanyageni	Ukaguzi na ufunguzi wa mafunzo	S/N
8	Ujenzi wa bara bara Shidi/Mwambuni	Shidi	Ukaguzi na uzinduzi	14,000,00
9	Mradi wa maji safi Mashuleni	Makombeni	Ukaguzi na uzinduzi	15,000,00
10	Mradi wa bio gas	Mahuduthi	Ukaguzi na uzinduzi wa nishati mbadala kwa hifadhi ya mazingira, ukaguzi wa ng'ombe wa maziwa na migomba ya majaribio.	14,000,00
11	Mradi wa Kompyuta	Skuli ya Mkanyageni	Ukaguzi na uzinduzi	25,000,00
12	Ujenzi wa kituo cha afya	Tasini - Kiwani	Uzinduzi wa kituo cha huduma za mama na watoto	9,663,000
13	Ujenzi wa Mnara wa kumbu kumbu	Kiwani	Uzinduzi wa mnara na upandaji wa mti wa kumbu kumbu	-
WILAYA YA CHAKE CHAKE				
1	Mradi wa ujenzi wa bara bara	Kilindi	Uwekaji wa jiwe la msingi	-
2	Mradi wa hifadhi ya mazingira	Kilindi	Ukaguzi wa miti ya hifadhi ya mazingira	40,995,13
3	Mradi wa ujenzi wa skuli	Kilindi	Uwekaji wa jiwe la msingi na upandaji wa miti ya kumbu kumbu	42,038,20
4	Ujenzi wa nyumba bora	Mitamani	Uwekaji wa jiwe la msingi	8,067,320
5	Mradi wa ufugaji kuku	Chanjaani	Ukaguzi wa shughuli za ushirika	11,000,00
6	Mradi wa kilimo cha migomba	Tibirinzi	Ukaguzi wa shughuli za ushirika wa wajasiriamali na uzinduzi wa kisanduku cha maoni ya kupinga rushwa	-

7	ZAPHA+	Wara	Ukaguzi wa shughuli za upigaji vita UKIMWI na Dawa za kulevya	-
8	Mradi wa SACCO ya vijana	Chachani	Ukaguzi na uzinduzi wa SACCOS pamoja na kukabidhi mikopo kwa baadhi ya wanachama wa SACCOS hiyo	-
9	Mradi wa maji safi	Wesha	Ukaguzi na uzinduzi wa mradi	16,000,00
10	Mradi wa ukaushaji wa madagaa	Ndagoni	Ukaguzi wa shughuli za ukaushaji wa madagaa	36,000,00
11	Mradi wa ujenzi wa kituo cha afya	Ndagoni	Uwekaji wa jiwe la msingi na utoaji wa chanjo ya matone ya vitamin A pamoja na upandaji wa miti.	65,375,00
12	Huduma ya upimaji wa VVU	Madungu Sekondari	Ukaguzi wa huduma ya ushauri nasaha na upimaji wa hiari wa VVU na UKIMWI CVCT	-
WILAYA YA MICHEWENI				
1	Ushirika wa jiendeleze B	Wingwi Njuguni	Ukaguzi wa shughuli za ushirika	-
2	Mradi wa kilimo cha mahindi	Mziwanda	Ukaguzi wa shamba la kilimo cha mahindi	-
3	Utoaji wa mafunzo ya UKIMWI ZANGOC	Mjini Wingwi	Ukaguzi na ufungaji wa mafunzo ya UKIMWI na Madawa ya kulevya	-
4	Mradi wa kuhifadhi mazingira	Mkwaju mgoro	Upandaji wa miti ya kuhifadhia mazingira	-
5	Ushirika wa wajasiriamali Hirimu nifasi	Majenzi Micheweni	Uwekaji wa jiwe la msingi katika ofisi ya ushirika na ukaguzi wa shughuli za wanaushirika	13,000,00
6	Mradi wa ujenzi wa daraja	Chanjaani Konde	Ukaguzi na uzinduzi wa daraja la bara bara ya Konde - Msuka	300,000,0
7	Mradi wa kituo cha huduma za mifugo	Konde	Ukaguzi na uzinduzi wa kituo cha huduma za mifugo	-
8	Kituo cha afya	Konde	Utoaji wa chanjo za Vitamin A kwa watoto	-
9	Ujenzi wa skuli	Mgogoni	Uwekaji wa jiwe la msingi	29,000,00
10	Ujenzi wa nyumba bora	Kinyasini	Uwekaji wa jiwe la msingi	-

WILAYA YA WETE				
1	Mradi wa upandaji wa miti katika shamba la misitu	Kiungoni	Ukaguzi wa shamba	-
2	Ujenzi wa nyumba bora	Mchanga mdogo	Uwekaji wa jiwe la msingi	15,000,00
3	Mradi wa ufugaji ng'ombe wa maziwa	Kisiwani	Ukaguzi wa ofisi ya shughuli za wanaushirika	5,555,000
4	Mradi wa ujenzi wa daraja	Mkarafuu mmoja	Ukaguzi na ufunguzi wa daraja hilo	44,418,45
5	Mradi wa ujenzi wa skuli	Mzambarauni	Ufunguzi wa madarasa 3 ya kusomea	18,853,00
6	Nyumba za kubadilisha tabia (Soba houses)	Limbani	Ukaguzi na ufungaji wa mafunzo ya vijana walioacha kutumia madawa ya kulevya	-
7	Ujenzi wa kituo cha mafunzo ya amali	Minyunyweni Ukunjwi	Ukaguzi na uwekaji wa jiwe la msingi	51,133,52
8	Mradi wa utengenezaji majiko sanifu	Ukunjwi	Ukaguzi wa shughuli za wanakikundi	-

MIRADI ILIYOSAIDIWA KWA MICHANGO YA MWENGE MKOA WA KUSINI UNGUJA

No.	**JINA LA MRADI**	**PAHALA**	Kiasi
1.	Chuo cha Wajasiriamali Vijana	Dunga Jumba la Mawe	1,050,0
2.	Vikundi vya Kinamama Weza	K/Mwembeshauri	500,00
3.	Ujenzi wa Banda la Madrasa	Pongwe - Mwera	350,00
4.	Kisima cha Umwagiliaji maji	Koani	350,00
5.	Banda la mitihani	Michavi	350,00
6.	Kituo cha Afya	Paje	
7.	Chumba cha Komputer na Maktaba	Mtende	300,00
8.	Ushirika wa Migomba	Mzuri – Makundichi	300,00
9.	Ushirika wa kupanda miti	Kiongon -Makunduchi	300,00
10.	Ushirika wa kina mama	Kizimkazi- kunguni	300,00

SNO	JINA LA MRADI	PAHALA ULIPO	SHUGHULI	MSAA
1	Nyumba bora	Mitambani	Kiongozi alizawadia miradi hio	
2	ZAPHA+	Wara	“	
3	Mifugo	Chanjaani	“	
4	Migomba	Tibirinzi	“	
5	Madagaa	Ndagoni	“	
	Skuli ya Kilindi	Kilinidi	“	
6	Vikundi (4) Wajasiriamali	Kilindi	“	
7	Skuli ya Madungu	Madungu Sekondari	“	
	VIKUNDI VYA SANAA			
1	Utenzi		Kiongozi alisaidia vikundi hivyo vya sanaa	
2	Brass Band			
3	Awali group			
4	Sururu group			
5	Taarab			
6	Halaiki			
7	Rusha roho			

FEDHA ZILIZOCHANGWA KWA AJILI YA MWENGE WA UHURU 2013

	MKOA	
	Mkoa wa Mjini Magharibi	**16,070,850**
	Mkoa wa Kaskazini Unguja	**16,746,340**
	Mkoa wa Kusini Unguja	**7,362,450**
	Mkoa wa Kaskazini Pemba	**11,350,000**
	Mkoa wa Kusini Pemba	**14,565,000**
	JUMLA	**66,094,640**

Kiambatanisho Nam. 10

ORADHA YA MIRADI ILIYOCHANGIWA KWA FEDHA ZA MICHANGO YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2013 MKOA WA MJINI MAGHARIBI

S/NO	JINA LA MRADI	MAHALA	KIWANGO CHA FEDHA
1.	Uzinduzi wa program ya uhifadhi wa maeneo yaliyoathirika kimazingira	Kwahani Uwanja wa Farasi	1,142,616/-
2.	Kikundi cha tusifarikiane cha kina mama	MuembeShauri	200,000/-
3.	Kikundi cha Polisi Jamii	Malindi	1,142,616/-
4.	Skuli ya Msingi	Migombani	2,179,500/-
5.	Skuli ya Sekondary	Muembe Ladu	300,000/-
6.	Mradi wa Magofu	Maruhubi	571,700/-
7.	Kamati ya watoto wanaoishi katika Mazingira magumu	M/Makumbi	571,700/-
8.	Kituo Cha Afya	Kwawazee	571,700/-
9.	Kikundi cha Tushikamane kina mama	Migombani	571,700/-
10.	Kituo cha Wajasiriamali	Karakana	571,700/-
11.	Mradi wa TAWABINA Sober house	Meli nne uzi	300,000/-
12.	Ushirika wa watu wenye ulemavu	Magogono na Kinuni	300,000/-
13.	Kikundi cha Mazingira cha upandaji miti	Bububu	300,000/-
14.	Skuli ya kijuto upele	Kijuto upele	900,000/-
15.	Skuli ya Dimani	Dimani	300,000/-
16.	Skuli ya M/Kwerekwe ‘E’	M/Kewerekwe	400,000/-
17.	Ushirika wa kina mama wa kupika na kushona	Taveta	600,000/-
18.	Ukumbi wa Mkutano	Wilaya ya Magharibi	600,000/-
19.	Watoto wanaoishin katika Mazingira magumu	Kijuto Upele	300,000/-
20.	Watoto wanaoishi katika Mazingira magumu	M/Kwerekwe	300,000/-
21.	Skuli ya M/Kwerekwe ‘C’	M/Kwerekwe	300,000/-
22.	Kituo cha Afya	Kiyanga	900,000/-
23.	Kikundi cha Ushirika	Kiyanga	300,000/-
24.	Kikundi cha Ushirika	Kwarara	300,000/-
25.	Kikundi cha nia safi ni njia	Bweleo	300,000/-
26.	Wastara Coorperative ushoni	Bweleo	300,000/-

27.	Ushirika wa nia safi	Bweleo	300,000/-

Vikundi vilivyohitaji mkakati maalum ili viweze kurejesha mikopo yao ni:-

1- Sivibaya – Chake Chake

2- Takawani – Chumvi Cooperative Society – Shengejuu

3- Jiendeleze – Wingi

4- Kidutani –Sizini (Uchongaji)

5- Uchozini Cooperative Society – Wete

6- Tupendane – Piki

7-Tundwa Cooperative Piki

8- Mambo Pujini

9-Kumbuka – Wajibu Wako

10- Tajirika and Metal Works –Mkoani

11- Creative Saccos – Mkoani

Kiambatanisho Nam. 11

VIKUNDI VYA VIJANA VILIVYOTEMBELEWA

S/NO	JINA LA KIKUNDI	AINA YA MRADI	ENEO KI
	WILAYA YA CHAKE CHAKE		
1	Sayari		Wawi Viji
2	Mungu tupe SACCOS	Kuweka na Kukopa	Chachani
3	Tawakal cooperative society	Uchongaji	Kichungw
4	Sivibaya	Uchongaji	Chake cha
5	Ujuzi cooperative	Kilimo na Uvuvi	Tundauwa
6	Kumbuka wajibu wako	U/Ngo'mbe	Matale
7	Mambo 1	Uchongaji	Pujini
8	Yaleo kali	kuweka na kukopa	chake Cha
9	Zena Yahya Othman	U/Sabuni	Madungu
10	Soko la Jumapili	uuzaji wa bidhaa za Wajasiriamali	Chake Ch
11	Nia safi tailoring	Ushonaji	Chake Ch
12	Uchumi Imara	K/Mboga mboga	Chake Ch
13	Tuonane SACCOs	kuweka na kukopa	Chake Ch
	WILAYA YA MKOANI		
14	Tajirika cooperative	Uchomaji vitu vya vyuma	Uweleni
15	Kidutani cooperative	Mgahawa Chokostiq	Kendwa
16	Mtaka Youth	Kilimo na U/mazingira	Nanguji
17	Utandawazi	K/Mboga mboga	Chokocho
18	Bora Imani	Uvuvi	Chokocho
19	Creative	kuweka na kukopa	Mkoani
20	Ufugaji wa nyuki cooperative	Ufugaji nyuki	Kiwani
21	Juhudi	Kilimo	Kiwani
22	Upandaji wa mikoko cooperative	U/Mazingira	Kiwani
23	Ushonaji cooperative	Ushonaji/Vitalu	Mkoani
24	Jambo Group	K/Mboga mboga	Mkoani

25	ZAPHA+	U/Sabuni	Mkoani
26	JUWAMA	Mafuta/U/Sabuni,	Mkoani
27	Mola Tupe Kheri	vyakula vikavu	mkoani
28	Juhudi Zetu	U/sabuni	Mkoani
	WILAYA YA MICHEWENI		
29	Jitihada	U/Mwani	Wingwi
30	Kinazini cooperative	Kilimo	Wingwi
31	Uhai hustiri mambo	Kilimo	Shumba y
32	Kidutani	U/Mbuzi	Sizini
33	Nia Njema	U/Mazingira	Michewen
34	Umoja Ni Nguvu	U/Sabuni	Michewen
35	Safinia	Uatikaji wa vitalu	Michewen
36	Letu Ni Moja	U/Mazingira	Michewen
37	Safina	Uvuvi	Michewen
38	Zinangatia	Usukaji Kamba	Michewen
39	Jiendeleze A	Uchongaji	Wingwi
	WILAYA YA WETE		
40	Takawani cooperative	U/Chumvi	Shengejuu
41	Imara cooperative	U/kuku	Chwale
42	Hatuyumbi	U/chumvi	Shengejuu
43	Hatunachuki	Kilimo na Ufugaji	Mtambwe
44	Sisi wanamaendeleo	U/Kuku	Bahanasa
45	Istiqama	Kilimo	Chwale
46	Maendeleo	Ufugaji Kilimo	Chwale
47	Tunaweza	Kilimo	Maziwani
48	Lion of development	Ufugaji Kuku	Pandani
49	Jumuiya ya Uvuvi, Kilimo na Ufugaji wa Samaki	Kilimo, Uvuvi, Ufugaji wa Samaki	Gando
50	Nguvu zetu	Kilimo	Gando
51	Uchozini Cooperative	B/ndogo ndogo	Jadida

52	Tundwa Cooperative	U/kuku na Kilimo	Piki
53	Tupendane	Kilimo	Kinyikani
54	Hatuwi sawa	U/ng'ombe na Uvuvi	Mpamban
55	Elimu ya msingi	Uvuvi na U/Mihogo	Mpamban
56	Tufanye kazi	Kilimo cha Mwani	Kojani
57	Mungu ni Mwema	K/mboga mboga	Kitambuu
58	Wazo letu	U/Chumvi	Pembeni
59	Starehe gharama	Uvuvi	Kojani
60	Mambo waa	Uchongaji	Pembeni
61	Annur SACCOS	Kuweka/kukopa	Piki
62	Tuwe imara	Ufugaji, Kilimo	Piki
63	Haviliki	U/Miti	Mjini Ole
64	MKIPI miliki	U/Sabuni	Mzambara
65	Jambo nia	K/Minazi, K/Migomba	Kambini
66	Kwanini tusiweze	Kilimo na U/kuku	Hindi – K
67	Tutawezana	U/Kuku	Kambini
68	Kutoa ni moyo	U/Mashuka	Hindi – K
69	Kitunze kidumu	Kilimo, U/Nyuki, U/miti na ufinyanzi	Hindi – K
70	Umoja wetu	U/Nyuki, U/Kuku na Migomba	Kambini
71	Kibwe kiti	U/samaki, Chunvi, Kilimo na U/sabuni	Kambini
72	Penye nia	k/mboga mboga na Ufugaji	Hindi – K
73	Jumuiya ya mazingira Kambini (JUMAKA)	U/Nyuki, U/Miti	Kambini
74	Tuamke	Kilimo, U/Nyuki na U/Majiko	Kambini
75	Juhudi zao	U/Chumvi	Mchinjiba
76	Kichakaa si shangi	Samaki na U/Chumvi	Kiuyu mir
77	Matumaini B	K/mboga,K/Kukopa U/Ng'ombe	Kiuyu Kig
78	Matumaini A	B/ndogondogo na U/Kuku	Kiuyu Kig
79	Bee Reconciliation Co. Society	U/Nyuki	Kiuyu Kig
80	Minungwini Social Welfare Organization	U/mazingira na Kusaidia Jamii	Kiuyu Mir
81	Maendeleo Yetu	Ushonaji na U/Mikoba	Kiuyu Kig

82	Hatutaki Shari	U/Kuku	Kiuyu Kig
83	Gongo Maji Cooperative	Ushonaji na B/ndogo ndogo	Ole – Mih
84	Maumbile	Mboga mboga na B/ndogo ndogo	Ole – Kizi
85	Juhudi endelevu	Mboga mboga, K/Mivinje	Ole – Gon
86	Wezesheni tuweze	U/kuku na K/mboga mboga.	Ole – Jonv
87	Tumekubali	Ufugaji wa Kuku	Ole – Jonv
88	Mbuyuni cooperative society	Kilimo/migomba	Ole – Mbu
89	Tushirikiane	Ufugaji Kuku	Ole – Rah
90	Tunda jema co. society	U/Mbuzi, U/Sabuni na B/Ndogo ndogo	Ole – Mih
91	Haturudi nyuma	K/Muhogo. Mboga mboga na U/Mashuka	Vumba –
92	Maisha ni siri	U/Ng'ombe na K/mboga mboga	Kinyikani
93	Umoja ni nguvu	K/migomba U/mikoba	Kinyikani
94	Jikomboe	K/mboga mboga, Ufugaji, U/sabuni na Upandaji miti	Kinyikani
95	Jiwezeshe	K/muhogo na U/mbuzi	Kinyikani
96	Bora juhudi zetu	Ushonaji	Kinyikani
97	Mungu Tupe Kheri	Kuweka Na Kukopa	Wete
98	Mola Tujaalie	Kuweka Na Kukopa	Wete
99	Riziki Mtoaji Mola	Kuweka Na Kukopa	Wete
100	Nia Njema	Asali Na Sabuni	Wete
101	Gando Women Development	Sabuni Za Aina Zote	Gando
102	Gando Youth Act	Usindikaji Matunda	Gando
103	Gando Cassava Production	Usindikaji Muhogo	Gando

Kimbatanisho Nam. 12

VIKUNDI VYA UJASIRIAMALI VYA VIJANA VILIVYOHAMASISHWA KUJIUNGA NA SACCOS YA VIJANA

SN	VIKUNDI VILIVYOSHAJIISHWA KUJIUNGA NA SACCOS YA VIJANA	MAENEO VILIOPO	SHUGHU
	WILAYA YA WETE		
01	Hatunachuki	Mtambwe Kusini	Klimo na
02	Sisi wana maendeleo	Bahanasa – Piki	Ufugaji w
03	Istiqama	Chwale	Kilimo
04	Maendeleo	Chwale	Ufugaji/K
05	Tunaweza	Maziwani	Kilimo
06	Uhai hustiri mambo	Shumba ya vyamboni	Kilimo
07	Wazo letu	Pembeni	U/Chumv
08	Starehe Gharama	Kojani	Uvuvi
09	Mambo waa	Pembeni	Uchongaj
10	Kidutani	Sizini	U/Mbuzi
11	Annur SACCOS	Piki	Kuweka n
12	Tuwe imara	Shengejuu	Ufugaji, K
13	Haviliki	Mjini Ole	Upandaji
14	MKIPI miliki	Mzambarautakao	Utengene
15	Nguvu zetu	Gando	Kilimo
16	Jumuiya ya Utunzaji wa mazingira	Gando	Kuhifadhi
17	Lion of development	Pandani	Ufugaji w
18	Tawakal salt	Shengejuu	U/chumvi
19	Hatuyumbi Masota	Shengejuu	U/Chumv
	WILAYA YA MICHEWENI		
20	Safina	Finya	Uvuvi
21	Jitihada	Wingwi	Upandaji
22	Kujali wakati	Wingwi	U/Mwani/
23	Jiendeleze “B”	Wingwi	Kusokota

24	Jiendeleze “A”	Wingwi	Uchongaj
25	Mvivu halisi	Wingwi	Uchongaj
26	Hirimu nifasi	Micheweni	Utengene
	WILAYA YA CHAKE CHAKE		
27	Juhudi ni uwezo	Chonga	Kilimo
28	Nia njema	Pujini dodo	Kilimo
29	Zindukeni	Ndagoni	Uvuvi
30	Vijana Vikunguni	Nga’mbwa	Kilimo/U
31	Nia njema cooperative	Shungi	Ufugaji/K
32	Tuwe imara	Madungu	Biashara
33	Mungu atosha	Mkoroshoni	Kilimo ch
34	Samjuu	Madungu	Biashara
35	Mwanzo Mgumu	Chachani	Ufumaji
36	Lenge Maendeleo	Msingini	Ushonaji
37	Kheri Lawama	Wesha	Kilimo
38	Tunaweza Harakati	Tibirinzi	Ushonaji,
39	Tuwe Imara	Madungu	Ufumaji
40	Tukijaaliwa	Ziwani	Ufugaji w
41	Sayari	Wawi Vijijini	Ufugaji, F
42	Mungu tupe SACCOS	Chachani	kuweka n
43	Tawakal Cooperative Society	Kichungwani	Uchongaj
44	Ujuzi Cooperative	Tundauwa	Kilimo na
	WILAYA YA MKOANI		
45	Creative society	Uweleni	Kuweka
46	Badria	Uweleni	Biashara
47	Matumaini Cooperative	Uweleni	U/sabuni
48	Mwanzo Mgumu	Mkoani	Biashara
49	Tajirika Cooperative	Uweleni	Uchomaji
50	Kitandu Cooperative	Kendwa	Kilimo ch

51	Mtaka Youth	Nanguji	Kilimo na
52	Utandawazi	Chokocho	Kilimo ch
53	Bora Imani	Chokocho	Uvuvi
54	Wengi Wape	Mbuguani	Kilimo
55	Ugomvi Wa Ndugu	Wambaa	Uvuvi.

Kiambatanisho Nam. 13a

MALALAMIKO YA WANAWAKE UNGUJA NA PEMBA

UNGUJA

S/N	**AINA YA LALAMIKO**	**WILAYA**						**JUMLA**	**HATUA ZILIZOFIKIA**
		MJIN	**MAG**	**KAS "A"**	**KAS "B"**	**KAT**	**KUS**		
1.	Kupigwa	1	3	1	1		-	6	Ziko Polisi kwa hatua za kupatiwa ufumbuzi
2.	Huduma za Ujauzito	1	2	-	-	-	-	3	Kashauriwa kwenda Mahkama ya Kadhi kwa kupata ufumbuzi wa kisheria
3	Kuunguzwa moto	1						1	Mtuhumiwa yupo rumande kwa hatua zaidi za kisheria
4.	Kubakwa	1	1	-	-	1	1	4	Kashauriwa kwenda Mahkamani
5.	Kutelekezwa na Mume	-	4	1	-	-	-	5	Ipo mahkama ya Kadhi kwa hatua za kisheria
6.	Madai ya fedha		2	-	-	1	-	3	Malalamiko yote yamepatiwa ufumbuzi
7.	Madai ya nyumba	1	-	-	-	-	-	1	Kashauriwa kwenda Mahkamani
	JUMLA KUU							**24**	

Kiambatanisho Nam 13b

PEMBA

S/NO:	TUKIO	WETE	CHAKE	MICHEWENI	MKOANI	JUMLA	MAELEZO
1	Madai ya mahari	3	12	2	3	19	Malalamiko Kadhi.
2	Migogoro ya ndoa	15	36	-	6	57	35 yamepati 22 yamepele
3	Kupigwa	3	4	1	1	9	Ziko Polisi
4	Shambulio la aibu	1	2	-	-	3	2 ziko Polisi
5	Mvutano wa malezi	-	1	-	-	1	Suluhu imep
6	Kutoroshwa	-	-	-	1	1	Iko Polisi
7	Kupewa mimba	-	-	-	1	1	Iko PolisiI
8	Kutishiwa amani na kuibiwa	1	-	-	-	1	Iko Polisi
9	Madai ya nyumba	1	-	1	-	2	Kesi ziko kw
10	Mimba	1				1	Polisi
	JUMLA KUU	**25**	**55**	**4**	**12**	**95**	

Kiambatanisho Nam. 14

VIKUNDI VILIVYOTEMBELEWA UNGUJA - KIWILAYA WILAYA YA KASKAZINI "A"

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1.	Kuomba popote	Kilimo cha mboga mboga	Potoa
2.	Inna llaha maaswabirina	Muweka na kukopeshana	Potoa
3.	Twande nao	Mashine ya kusagia nafaka	Mkokotoni
4.	Hatujigawi	Kilimo cha muhogo	"
5.	Nasiye tufikiriwe	Kilimo cha mpunga	"
6.	Maskini hanuni	Kilimo cha mboga mboga	Chaani kubwa
7.	Chaani kubwa saccos	Kuweka na kukopa biashara ndogo ndogo	"
8.	Juhudi njema	Mboga mboga	"
9.	Kina mama imara	Mgahawa,Ususi na Biashara ndogo ndogo.	Nungwi
10	Ungalipo	Ufugaji ng'ombe wa maziwa	M/shauri
11.	Tupendane	Ufugaji kuku na mayai	Mshauri
12.	Tusife moyo	Upishi wa sabuni ya Mchai chai,Mdalasini, Mkarafuu na Mrihani.	Kidoti.
13.	Kina mama Jam	Upishi wa Jam	Gamba
14.	Hisani njema	Kilimo cha mboga mboga	Chutama
15.	Potoa SACCOS	Ushonaji nguo na kilimo	Kilindi.

WILAYA YA KASKAZINI "B"

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1.	Uendelee	Ukulima wa muhogo, matikiti na viazi vitamu.	Kilombero
2.	Yakwao	Kilimo cha Mananasi	Donge Vijibweni.
3.	Ususi endelevu	Usukaji wa mikoba, mikeka,	Pangeni
4	Hatuna pingamizi	Upishi wa sabuni , utengenezaji wa batiki	Upenja
5	Mgambo mpya	Ufugaji kuku wa kienyeji	Mgambo
6	Hatuna chuki	Uvunjaji kokoto , kuweka na kukopa	Mgambo
7.	Muwanda SACOSS	Upandaji miti na mashine ya kukobolea mpunga	Muwanda
8	Mtatuona hivihivi	Kilimo cha mbogamboga	Donge Mnyimbi
9	Sisi kwa sisi	Ufugaji wa ngombe wa maziwa	Donge Mnyimbi

WILAYA YA MAGHARIBI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1.	Asaakheri	Kilimo cha mboga mboga na kazi za mikono	
2.	Busara	Mapambo, mikoba, mazulia, vipochi	
3.	Wanawake tunaweza	Tie &die, ufugaji wa kuku, mboga mboga na kukopeshana.	
4.	Tupendane		
5.	Hatufi moyo	Kukopeshana bidhaa na fedha	Mw/Kwerekwe
6.	Neema haichewezi	Utengenezaji wa sabuni za chokaa na za maji,mikoba achari,madomet na batiki	Pangawe
7.	Wema Cooperative	Kushona nguo,kufuma,kupika sabuni,ususi wa sabuni,ususi wa mikoba,kokopeshana vombo.	Pangawe
8.	Tufaha	Ususi wa kili,achari,ufumaji wa mashuka ,usarifu wa ubuyu.	Mtofaani
9.	Family Group	Utengenezaji wa madometi achari za embe na kushona.	Mtofaani
10.	Maendeleo kwa wote	Mikoba,sabuni,madometi,biashara za vyakula,kukopesha pesa,vyombo na nguo	K/Upele
11.	Tusitupane	Kuweka na kukopa	Kwarara
12.	Hatutaki majungu	Kuweka na kukopa	K/Upele
13.	Kitunze kidumu silk	Kuweka na kukopa	MW/Kwerekwe

WILAYA YA KATI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1	Chaza mali	Utengenezaji wa mikoba, vitu vya mapambo.	Kikungwi
2	Tumeamua	Utengenezaji wa mikoba,	U/Ukuu kae pwani
3	Tumeridhika	Kilimo cha miti ya mivinje	Uroa
4	Nasisi twaja	Kilimo cha mboga mboga	Uroa
5	Sisi tuwe mbele	Kilimo cha mboga mboga	Mpapa
6.	Hatuna pangu	Kilimo cha mboga mboga	Mpapa
7	Kinamama mbele	Kilimo cha Halizeti	Mpapa
8	Mvivu hendi	Kilimo cha miti ya mivinje	Bambi

9	Tusiweze tunanini	Biashara ndogo ndogo, kuweka na kukopa, kutengeneza chumvi na sabuni	Bambi
10	Nia njema	Kazi za mikono, kuweka na kukopa, biashara ndogo ndogo	Bambi
11	Wema popote	Kilimo cha mboga mboga na biashara ndogo ndogo	Bambi
12	Ubaguzi hatutaki	Kilimo cha mboga mboga	Bambi
13	Tumeamua	Usafi wa mazingira na kilimo cha mboga mboga	Umbuji
14	Tuaminiane	Kuweka na kukopa, biashara ndogo ndogo	Gana
15	Tushirikiane	Kuweka na kukopa, biashara ndogo ndogo	Gana

WILAYA YA MJINI

S/N	**JINA LA KIKUNDI**	**SHUGHULI**	**SHEHIA**
1	Uwami	Kusuka mashuka	Migombani
2	Hatutaki shari	Kusuka mikoba	Migombani
3	Kinamama imara	Mafuta ya kiungo	Mkele
4	Riziki ni chanzo cha chuki	Kukopeshana bidhaa	Chumbuni
5	Tunamuomba Mungu	Biashara ndogo ndogo	Chumbuni
6	Nia Safi	Kushona nguo	Karakana
7	Mungu tujaalie	Biashara ndogo ndogo	Karakana
8	Ukubwa jaa	Kukopeshana bidhaa	Karakana

WILAYA YA KUSINI

S/N	JINA LA KIKUNDI	SHUGHULI	SHEHIA
1.	Daima tupendane	Kushona kufuma na kusuka madomet	Tasani
2.	Tunajaribu	Kilimo cha migomba	Tasani
3.	Mnarani	Kilimo cha mboga mboga	Tasani
4.	Juhudi zetu	Kilimo cha mboga mboga,	Tasani
5.	Tuwe n moyo	Kilimo cha viazi vikuu	Nganani
6.	Hatuyumbi	Kilimo cha mivinje	Nganani
7.	Bihimoyo	Kilimo cha migomba	Nganani
8.	Kisimba	Kiklimo cha muhogo na viazi vikuu	Muyuni A”
9.	Tusikerane	Kilimo cha muhogo na viazi	Muyuni A”
10.	Tupendane	Ufugaji wa kuku,	Muyuni A”

Kiambatanisho Namb. 15

SHEHIA ZILIVYOFANYIWA TATHMINI KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE

S/N	JINA LA SHEHIA	WILAYA
01	Pandani	Wete
02	Shengejuu	,,
03	Pembeni	,,
04	Bopwe	,,
05	Chwale	,,
06	Junguni	,,
07	Mtambwe Kaskazini	,,
08	Kiungoni	,,
09	Kambini	,,
10	Kinyikani	,,
11	Mzambarauni	,,
12	Piki	,,
13	Mchanga mdogo	,,
14	Ole	,,

15	Kisiwani	,,
16	Kizimbani	,,
17	Utaani	
18	Limbani	
19	Jadida	
20	Selemu	
21	Kipangani	
22	Mapofu	Micheweni
23	Mgogoni	,,
24	Sizini	,,
25	Tumbe Mashariki	,,
26	Kwale Gongo	,,
27	Kijichame	,,
28	Mtemani	,,
29	Njuguni	,,
30	Chanjaani	,,
31	Kidodi Wingwi	,,
32	Mpakani	,,

Kiambatanisho Nam 16

MCHANGANUO WA MATUMIZI YA FEDHA ZA KAWAIDA KWA MWAKA 2014/2015

FUNGU	IDARA	MAKADIRIO YA 2014/2015				
		JUMLA	MISHAHARA	M/MENGINEO	WAHISANI	FEDHA ZA MAENDELEO
03	A/KUU PEMBA	788,586,000	450,036,000	338,550,000	-	-
04	M/S/UTAFITI	2,494,329,000	124,594,000	165,000,000	1,604,735,000	600,000,000
05/01	W/WATOTO	382,540,000	126,177,000	60,763,000	195,600,000	-
05/02	MIKOPO	191,727,000	106,787,000	84,940,000	-	-
07	M/VIJANA	1,045,139,000	97,606,000	73,533,000	-	874,000,000
09	UWEZESHAJI	135,671,000	74,096,000	61,575,000	-	-
1101	U/JAMII	891,916,000	186,643,000	49,938,000	605,335,000	50,000,000
10	USHIRIKA	744,644,000	453,144,000	291,500,000	-	-
12	U/UENDESHAJI	896,118,000	536,117,000	360,001,000	-	-
JUMLA:		**7,570,670,000**	**2,155,200,000**	**1,485,800,000**	**2,405,670,000**	**1,524,000,000**

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa ni zamu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, karibu.

Mhe. Farida Amour Mohammed (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto): Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wanawake na Watoto naomba kusoma hotuba ya maoni ya Kamatiya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na makadirio na mapato na matumizi ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka 2014/2015.

Utangulizi

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na ardhi kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena leo hii katika mkutano wa bajeti kwa lengo la kuendelea kuwatumikia wananchi wetu na kufanya mapitio ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara mbali mbali za serikali kwa lengo la kuwaletea wananchi maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na makadirio ya bajeti ya wizara hii kwa mwaka 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Waziri na watendaji wake wote kwa mashirikiano yao makubwa wanayotupatia katika kazi zetu za Kamati ikiwemo na kazi hii muhimu ya kupitia na kujadili bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, aidha nachukua fursa hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yangu kwa michango na maoni yao waliyotoa wakati wa kujadili na kupitia bajeti hii. Naomba niwatambue kwa kuwataja kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar	Makamu Mwenyekiti
3.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
4. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Mjumbe
5. Mhe. Farida Amour Mohammed	Mjumbe
6. Mhe. Abdi Mosi Kombo	Mjumbe
7. Mhe. Ali Salum Haji	Mjumbe
8. Ndg. Asha Said Mohammed	Katibu
9.Ndg. Maryam Rashid Ali	Katibu.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Ustawi wa Jamii ni kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka kama ambavyo Kanuni ya 112 (e) Toleo la mwaka 2012 linavyoelekeza.

Aidha, Kanuni ya 95 (1) nayo inaelekeza kuwa fungu lolote la makadirio na matumizi lazima lipelekwe katika Kamati husika kufikiriwa kabla ya kupelekwa kwenye Kamati ya Matumizi. Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu kunukuu Kanuni hiyo ifuatavyo.

"Kabla ya Kamati ya Matumizi haijashughulikia fungu lolote la makadirio ya matumizi, fungu hilo kwanza litapelekwa kwenye Kamati inayohusika likafikiriwe na halitoletwa kwenye Kamati ya Matumizi ya Baraza Zima mpaka Mwenyekiti wa Kamati wa iliyopelekwa kazi kufikiria fungu hilo, atakapomuarifu Spika kwamba kamati yake imemaliza kulifikiria fungu hilo".

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu ilifikiria fungu Nam. 28 la makadirio ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto mnamo tarehe 8/05/2014 na ikafanya uchambuzi wa fungu hilo kwa umakini mkubwa na kuishauri serikali na wizara kwa kadri kamati ilivyoona inafaa. Na baada ya kukamilisha kazi hiyo ilimpa taarifa Mhe. Spika, kama kanuni zetu zinavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo mfupi, sasa naomba nianze kutoa maoni ya Kamati juu makadirio ya wizara kwa mwaka 2014/2015, kwa kuangalia maeneo mbali mbali ambayo kamati yangu imeona kuna haja kuyaingiza katika hotuba hii na kuyatolea ufafanuzi na ushauri kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake.

Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti 2013/2014:

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ilitengewa jumla ya shilingi bilioni tatu, milioni mia mbili arobaini na tisa, laki tisa na ishirini na mbili elfu (3,249,922,000). Hadi kufikia Mei, 2014 wizara ilipatiwa shilingi bilioni mbili, milioni ishirini na nne laki tisa na hamsini na tisa elfu(2,024,959,000) kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 62 ya bajeti yote ya wizara iliyotengwa kwa matumizi ya kazi za kawaida kwa 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, uingizwaji wa fedha za matumizi za kazi za kawaida kwa wizara hii ulikuwa si mbaya ukilinganisha na Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya ambazo pia kamati yangu imekuwa ikizisimamia wizara hizo. Ingawaje kamati imebaini kuwa mabadiliko ya muundo ya wizara za serikali uliofanywa katika mwaka wa fedha 2013/2014, ulipelekea wizara hii kuongezwa idara tatu zilizotoka katika Wizara ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Idara hizo zilikuwa ni Idara ya Mikopo, Idara ya Ushirika na Idara ya Uendeshaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

Kamati ilikubaliana na mabadiliko hayo kwa kufikiria kuwa kuongezwa kwa idara hizo katika wizara hii kungepelekea idara kufanya kazi kwa pamoja na wizara, na ile dhamira iliyokusudiwa ya kuziunganisha na wizara ingefikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli hali ilikuwa tofauti na vile Kamati yangu ilivyofikiria na napenda kuchukua nafasi hii kulieleza Baraza lako tukufu, kwamba Idara zilizoongezwa katika wizara hii, hazikupelekwa na bajeti zao na hivyo ilikuwa kama ni mzigo kwa wizara na ilipelekea ugumu mkubwa katika kutekeleza shughuli zao. Kutokana na hali ilivyojitokeza, Kamati inaiomba serikali pindi watakapokuwa wanafanya mabadiliko yeyote ya muundo wa wizara zake izingatie pia suala la kuhamisha fedha za bajeti ili majukumu yaliyopangwa na Idara hizo yaendelee kutekelezwa kama yalivyokusudiwa katika upitishwaji wa bajeti.

Kuhusu Deni la Fidia ya Wafanyakazi Walioumia Kazini

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imekuwa ikilifuatilia deni la fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini kwa kipindi kirefu ambapo deni hilo linajumuisha jumla ya wafanyakazi 71 na lenye thamani ya Tshs milioni 92,844,586/= (Unguja shilingi 32,560,064/= na Pemba Shilingi 60,284,522/=). Deni la fidia kwa wafanyakazi walioumia kazini limekuwa linasimamiwa na Idara ya Ustawi wa Jamii na limekuwa ni mzigo mkubwa kwa Idara hiyo, kwa sababu ni kubwa sana na Idara haiwezi kulilipa kutokana na uchache wa fedha za bajeti za Idara.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilifanya jitihada za makusudi ya kuiondolea Idara mzigo huo na ilifanya kikao kilichowakutanisha kwa pamoja Kamati yangu, Wizara ya Uwezeshaji,Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto na Wizara ya Fedha, ambapo lengo la kikao lilikuwa ni kujadili namna ya kulipa na kumaliza kabisa deni hilo ili wafanyakazi walioumia kazini wapatiwe fedha zao, ambapo kikao hicho kiliamua kuwa deni hilo litalipwa na Wizara ya Fedha baada ya taratibu za kuhakiki upya deni hilo.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu ilipokuwa inaendelea na kazi zake za kwa kipindi chake cha mwisho niliulizia tena deni hilo katika Wizara na majibu waliyopewa na Wizara hii, ni kuwa wameahidiwa na Wizara ya Fedha kwamba deni linaendelea kufanyiwa kazi na Wizara ya Fedha italipa malipo hayo kabla ya kuisha bajeti ya mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inakumbushia ahadi hiyo na naomba kupatiwa mchanganuo wa malipo, yaliyofanyika katika deni hilo wakati Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho ya hotuba yake ili Kamati yangu iweze kujua hatua iliyofikiwa na pia ikiwa imeshindikana kulipwa deni hilo Kamati inaomba kupatiwa sababu za msingi

zilizopelekea hali hiyo, kwani Wizara ya Fedha imekuwa ikitoa ahadi mara nyingi kulipa deni hilo, lakini Kamati bado haijaona utekelezaji wake.

Kuhusu Suala la Udhalilishaji Kijinsia

Mhe. Mwenyekiti, udhalilishaji wa kijinsia bado umekuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu kutokana na kuongezeka kwa vitendo hivyo siku hadi siku, bado kesi nyingi zimekuwa zikiripotiwa katika vituo mbali mbali vya polisi, lakini kesi hizo zimekuwa zikizorota, hazisongi mbele na katika hali hiyo kesi hukosa kutolewa hukumu kwa wakati na kupelekea kuongezeka kwa vitendo hivyo dhidi ya wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto imekuwa ikichukua jitihada kubwa katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji nchini kwa kuunda Kamati za Shehia za kupambana na vitendo vya udhalilishaji Unguja na Pemba, kuimarisha Vituo vya Mkono kwa Mkono,kufanya mapitio kwa baadhi ya sera na sheria zinazohusiana na masuala ya jinsia pamoja na kuielimisha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inaziona jitihada zinazochukuliwa na wizara hii, inathamini sana mchango wa wizara katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia, lakini kwa upande mwengine Kamati inasikitishwa sana na hali ya Mahakama zetu kwani kumekuwa na kesi za muda mrefu ambazo hazijapatiwa ufumbuzi na hatimae kufutwa. Hivyo, Kamati inaitaka serikali kuziunga mkono jitihada za wizara na kuhakikisha kuwa kesi zilizorundikana Mahakamani zinafuatiliwa na kutolewa hukumu kwa wakati kwani kuendelea kuzorotesha kesi kunapelekea waathiriwa wa vitendo hivyo kukosa haki zao, kuwaachia athari katika maisha yao hasa hasa za kisaikolojia na pia kuipa nafasi jamii kuendeleza vitendo hivyo.

Kuhusu Kilimo cha *Rosella* na mboga mboga kwa Vijana wa Tunguu

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha kilimo hicho kwa upande wa Unguja na Pemba ambapo kupitia kilimo cha *Rosella* na mboga mboga vijana wetu wameweza kupata ajira na kujiongezea kipato. Katika kufanikisha kilimo hicho, Wizara imekuwa ikilihudumia shamba la Vijana wa Tunguu kwa kulipia gharama mbali mbali ikiwemo za miundombinu ya maji, gharama za mafuta ya kuendeshea jenereta na gharama za mafunzo ambazo zimetumika katika kuwaendeleza vijana hao kwa kuwapeleka kujifunza zaidi Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu imeona mafanikio yaliyopo katika shamba la Tunguu na inaiomba wizara kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kujipatia taaluma zaidi wa kuendeleza shamba hilo, pamoja na kulitumia kama ni kituo cha mafunzo kwa vijana wengine watakaopendelea kujiunga na kilimo cha aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, Kamati yangu inaiomba wizara kuelekeza nguvu zake sasa katika shamba la vijana la Mbuzini liliopo Pemba, kwani kwa sasa vijana waliopo katika shamba la Tunguu wapo katika mazingira mazuri, wameshapata mafunzo ya kutosha na kilichobaki ni wizara kuwashajihisha vijana hao kujitegemea wenyewe na kuondokana na dhana ya utegemezi wa kila kitu kwa wizara.

Kuhusu Suala la Uwezeshaji na Ujasiri amali

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaipongeza wizara kwa kuweza kuwapatia mafunzo Wajasiriamali waliopo Unguja na Pemba mafunzo ambayo yameweza kuimarisha bidhaa zao na kuzipa thamani bidhaa hizo katika soko. Aidha, Kamati imefurahishwa na hatua zinazochukuliwa na Wizara hii, ambazo zina azma ya kuanzisha kituo cha kutotolea wajasiriamali *Incubation centres* kwa lengo la kufundisha na kuwalea wajasiriamali ili waweze kuwa na ujuzi katika fani hiyo na hatimae kujiajiri wenyewe kupitia vikundi vya ushirika au mtu mmoja mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati inaitaka jamii pindi kituo hicho kitakapokuwa tayari kukitumia ipasavyo na kuyatumia mafunzo wanayopatiwa na wizara katika kutengeneza bidhaa zao ili ziweze kuwa na viwango vizuri na zipate ushindani katika soko la biashara za ndani na nje ya nchi na hatimae kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yangu inampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuanzisha Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambao ulizinduliwa Rasmi tarehe 4/6/2014 na Makamu wa Pili wa Rais, mfuko huu muhimu kwa kuwaendeleza Wajasiriamali utasimamiwa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa jamii, Vijana Wanawake na Watoto. Kamati inachukua nafasi hii kuishauri wizara kutoa elimu ya kina kwa wananchi kuhusiana na mfuko huu, aidha, kusimamia vyema katika kuhakikisha kuwa wananchi watakaonufaika na mfuko huo kupitia mikopo wanarudisha mikopo hiyo kwa wakati ili iweze kuwanufaisha na wengine. (*Makofi)*

Kuhusu Jengo la Idara ya Ushirika

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ilipokuwa inafanya kazi zake kwa vipindi tofauti imekuwa ikikagua jengo la Idara ya Ushirika na kubaini kuwa bado Idara wanatumia jengo chakavu na halitoshelezi kwa mahitaji ya Idara. Aidha, Kamati ilipokuwa inahoji kuhusiana na hali hiyo, iliarifiwa kuwa tayari Idara imepatiwa jengo jengine katika eneo la Migombani kwa ajili ya Ofisi, jengo ambalo linahitaji matengenezo makubwa kabla ya kuhamiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati imebaini kuwa katika mwaka wa fedha ulioisha hakukuwa na marekebisho ya msingi yaliyofanyiwa jengo hilo hali iliyopelekea wafanyakazi wa Idara kuendelea kubakia katika jengo bovu. Kamati yangu hairidhishwi na hali ya jengo, kwani mfanyakazi yeyote anahitaji mazingira yaliyo salama kwa ajili ya kufanya kazi zake kwani mazingira yasiyo salama yanaweza kumletea athari mfanyakazi na pindi anapopata ajali kazini, inachukua muda mrefu kupata fidia zake, kama Kamati yangu ilivyokuwa inashuhudia deni la wafanyakazi 71 walioumia kazini kuendelea kuchukua muda mrefu bila ya kulipwa.

Mhe. Mwenyekiti, kila mmoja wetu anafahamu kuwa kinga ni bora kuliko tiba. Hivyo, Kamati inaitaka serikali kuipatia Idara fedha za matengenezo katika bajeti ya mwaka huu ili Idara iweze kufanya matengenezo ya jengo lake na wafanyakazi waweze kufanya kazi zao katika mazingira mazuri na yenye usalama.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumalizia hotuba hii kwa kusema kwamba utekelezaji katika wizara yeyote unahitaji nyezo na rasilimali ikiwemo fedha, wataalamu, vitendea kazi nakadhalika ili majukumu yaweze kutekelezwa kwa ufanisi. Hivyo, Kamati inaisisitiza Wizara ya Fedha kuipatia wizara hii bajeti yake yote kama itakavyopitishwa na Baraza la Wawakilishi kwani bila ya nyenzo wizara itashindwa kufanya majukumu yake.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua tena fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Wajumbe wa Baraza hili tukufu, pamoja na watendaji mbali mbali kwa utulivu na usikivu wao katika kipindi chote nilichokuwa nawasilisha hotuba ya maoni ya Kamati, aidha, nawaomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waijadili, washauri na wakosoe kwa lengo la kuboresha na hatimae waipitishe bajeti ya wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi binafsi na kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Farida Amour Mohammed, kwa niaba ya Mwenyekiti kwa uwasilishaji wako. Mpaka sasa Waheshimiwa Wajumbe, nina mchangiaji mmoja tu na tunamkaribisha mchangiaji huyo ambaye ni Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wale wengine ambao wanataka kuchangia, basi tunawaomba walete maombi yao.Karibu Mhe. Makame Mshimba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze kuchangia kwa kuanza kutoa taaluma ambayo niliyopewa na Mwenyezi Mungu mwenyewe na kwa kupitia kwa wataalamu ambao na wao wamepewa akili na Mwenyezi Mungu mwenyewe *Subhanahu Wataallah.*

Mhe. Mwenyekiti, nina masikitiko makubwa sana kwa wizara hii, ambayo ina walengwa muhimu sana katika nchi na ni wajengaji nchi wamo katika wizara hii. Leo nilifikiria, sina haja ya kukutoa thamani, lakini ilikuwa *full suit* iendelee kama ilivyokuwa Makatibu wanawake wawili, ilikuwa na Mwenyekiti awepo mwanamke hapo juu, ingekuwa raha zaidi, lakini sawa hakuna tatizo, hiyo imo lazima kwa kinamama na kinababa na wao wawepo, ili waweze kuchangia maendeleo kwa pamoja, nalo hilo nimeliona kwa upande mwengine. Naona hiyo haki niitowe kwa kukupa haki yako kuwa unawaongoza vizuri kinamama, sifa hiyo naomba nikugaie na wewe.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na kero dogo sana. Mhe. Waziri usione tabu kukuambia nakuzuilia fungu, nakutolea shilingi. Bora nilizuie fungu la Mipango na Utafiti. Naomba nilizuie na sababu zangu ninazo na *Hansard* zangu ninazo. Usinune mama ndio tumo katika utekelezaji wa maendeleo ya bajeti.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana nilichangia suala la benki ya kina mama. Nilizungumzia sana benki hii ya kinamama tuwatafutie benki yao. Wenzetu Bara tayari wameshafikia malengo makubwa sana na hiyo benki tayari ipo, kina mama ni watu tabu na ni lazima tuwatatulie vitu vya kuwalainishia ili wasiwe watu wa tabu. Nilisema sana kuhusu suala la benki ya akinamama. Kinamama wanahangaika, wako wengi na hatujawatendea haki, niseme ukweli *kililahi taalah,* kinamama hatujawatendea haki na ndio maana nikawa na uchungu mkubwa sana, wamenizaa na wamenilea, kwa nini mimi nisiwatetee.

Mhe. Mwenyekiti, katika hii *Hansard* yangu ina Mhe. Wanu Hafidh na yeye alichangia, alitia nyama katika suala la benki ya kinamama, kwa sababu ndio mkombozi, lakini mpaka leo tunaona tabu gani. Haidhuru tuna mfuko wa uwezeshaji, ni pesa ndogo na mwishowe zinaishia katikati, wengine wanakuwa hawarejeshi, lakini benki ina sheria, sasa unapokuwa na sheria ndio kina mama wanapopata kuelimika kwa mujibu wa sheria. Hii mifuko haina sheria, kama ziko sheria zake, basi hazina nguvu ya kumuezesha mtu aogope aone zirejeshwe zile fedha kwa haraka sana. Kama ipo sheria, basi naomba sana Mhe. Waziri uje kuieleza sheria ya kumueleza mtu ili aelewe zile fedha anazopewa sio za kula tasi tu, lakini benki zina sheria zake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Waziri aje kunipa jibu zuri sana kuhusu suala la benki, si hivyo nitashirikiana nao kina mama kuandamana kabisa, kwa sababu hiki kitu sio masihara, usiseme aaah! linauma sana, kinamama wanapata tabu, wanataka kujiendesha. Kama nchi za wenzetu sasa hivi, leo ukipiga hesabu kinamama, nani mwenye uwezo wa kujenga nyumba kinamama hapa, hawana uwezo. Je, ni wangapi wanafanya biashara kinamama? Njoo niambie, kama sio matajiri tu kama kina Mhe. Raza niambie ni wangapi? Hakuna kwa sababu hawana sehemu ya kwenda kukopea, kwa sababu benki yao ikiwepo itakuwa mkopo nafuu na sheria nafuu, tofauti na hizi benki nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, Mhe. Waziri mimi naomba sana kwa hili silinyamazii nimeshachoka, naomba kunukuu sasa. mwaka jana nilipiga kelele sana kuhusu suala la benki ya kinamama. Kinamama walinipa hongera baada ya kusikia mimi nawatetea kuhusu suala la benki, wametoa hongera kubwa na leo watazidi kupiga vigelegele mitaani huko. Kwa hivyo, mimi naomba sana, niko *serious* na hili suala mimi sikubaliani nalo, kwa sababu suala hili linaondoa udhalilishaji kwa kinamama, na kubakwa kinamama kama utaiweza hii benki.

Mhe. Spika, natoa ushauri wangu kwa kuwa hii wizara yako mara nyingi sana ina mambo ya ubakaji, mambo ya kudhalilishwa kinamama, mambo ya vijana kukosa ajira na mengineyo, lakini kuna chombo ambacho najaribu kuwatafutia wana sheria kama wapo wajaribu kunisaidia chombo hicho. Kweli Idara ya Kazi kipo na Idara ya Kazi yenyewe ipo, lakini inavyoonesha asilimia kubwa sana wanapata tabu kinamama kwa chombo kama hiki, kupata haki zao katika sehemu wanazofukuzwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kinamama wanafukuzwa kazi ovyo ovyo kwenye makazi, hawatendewi haki, hawafuatiliwi haki zao na sasa hivi wako nje kibao, sijui kama sio chini ya 5 au 6 wananisubiri mimi nitoke nje, lakini wewe mwenye wizara ndio mwenye uchungu, ni lazima uwe na chombo cha sheria. Suala hili naomba sana jamani msione tabu kuwatafuta wanasheria, chombo hiki kitakusaidia wewe kupambana na hao kama ikiwa *labour* wamefanya vizuri au wamefanya vibaya, wewe unaingia kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama kipo utaniambia kwa nini kisifanyekazi, nitazidi kung'ang'ania shilingi mbili nitowe nyengine. Kama kipo, kwa sababu gani hakitekelezi kazi yake, kama huna, basi mimi nitakusaidia watafute wanasheria ili waweze kukitengeneza hiki chombo, kwa sababu ni chombo muhimu sana ambacho kitawasaidia vijana kunyanyaswa, kitawasaidia kinamama hata zile kero za kufukuzwa ovyo ovyo kwenye makazi, idadi inazidi siku hadi siku ya kufukuzwa.

Mhe. Mwenyekiti, Makampuni yapo mengi ya *security,* hatimaye kinamama maskini ya Mungu wanakwenda kujiunga, lakini wanafukuzwa na pesa zao hawapewi, wanadhalilika maskini, Mhe. Waziri, wizara yako iko wapi? Naomba sana Mhe. Waziri, tatua kitengo hicho kwa mujibu wa sheria, watafute wanasheria ili waweze kukusaidia kushughulikia matatizo hayo, kwa sababu *labour* nasema bado haijafika asilimia ya kuweza kuwatetea wananchi,

hawana nguvu, kwa sababu watu wengine maafisa ni walaji wanawadhalilisha hao wanyonge, namba inazidi badala namba kupungua kwa sababu serikali inatoa mwanya kwa Makampuni ili watowe ajira na waweze kuondoa mzigo serikalini na kuweka kwenye sekta za binafsi, lakini ni moja katika chaka moja baya sana la udhalilishaji ndani ya nchi yao. Mimi kitu kinachonisikitisha ni ndani ya nchi yao mtu anakuja anawadhalilisha, sheria zipo na mawizara yapo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio maana nikasema nitowe wasia wa kusema kuwa Juzi nimshukuru Mhe. Rais ambaye alikuambieni sana na nina wasia mmoja mzuri sana. Nadhani ni wasio mzuri wa kuwa lazima wachaguliwe mawaziri wenye macho ya kuona mbali na sio chini ya pua tu, kama walivyo wengine kati ya hao mawaziri, nani watajijua wenyewe. Kwa hivyo, naomba wasia huo nao tuutekeleze, kwa sababu sasa hivi mawaziri tunatakiwa tuone mbali na tuone mbali kwa sababu kuwathamini wale wananchi wetu sio tuone hapa tu. Sasa na huo wasia wangu nakupeni mawaziri chukueni bure tu, wala hautaki *expert* ili tukamilishe katika kujenga serikali nzuri ya Dkt. Ali Mohammed Shein, mwenyewe anakusikilizeni mnavyofanya vitu vyake huku bila ya kufuata ushauri uliokuwa wa kuaminika.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee kwa haraka haraka, lakini naona leo hawako wengine nikusaidie kazi, ukurasa huu wa 22, Idara ya Uwezeshaji, kifungu hiki kinanisikitisha sana tunatanua masoko bila ya wajasiriamali wadogo, masoko hayo yako wapi, mpaka leo tuko *weak*, masoko yao yako wapi?

Mhe. Mwenyekiti, kwenye majimbo watu wanatengeneza maachari, watu wanatengeneza bidhaa nyingi tu, biashara zimekuwa zinadoda, halafu leo tunasema hapa tuna utanuzi huu, mwaka karne ya ngapi bado tuna utanuzi tu, mimi sikubaliani nacho kifungu hichi, hatuko *serious* tunadanganya tu kwenye mapepa kama haya tunasema na nyinyi, mimi jamani kwa kweli inanisikitisha sana, hebu tuwe wakweli, Mhe. Waziri, tugeuke sasa, tugeuke tumalizie hii karne ya mwisho ya kuendelea kwenye uchaguzi, vijana sasa tunawataka kwenye uchaguzi tunataka chama chetu kishinde na sisi ndio wenyewe, tulioshika, kwa nini tushindwe kuwatengenezea neema? Kwa nini tushindwe kuwafuatilia kuwatafutia masoko?

Mhe. Mwenyekiti, masoko yapo ndani na nje, lakini kuya-*organize* tu, muhusika yule kupita kwenda kuyafuatilia, anakuwa anashindwa, hapa mimi nakuomba sana jitahidi sana kwa suala hili, tunaandika vizuri, sisi wataalamu wa kuandika vizuri wa vitabu, lakini sio wataalamu watekelezaji, ndio tatizo lenyewe kubwa hilo, sisi misingi yetu inakuwa mibovu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kuunda hakuna anayetukuta hapa Zanzibar, lazima sisi nambari *one* bwana, tuna uhodari wa kuunda *East Africa* nzima, tunaunda mambo mangapi, tunaunda sisi hapa, lakini tunashindwa kulinda hiyo, mimi sikubaliani nalo. Naomba sana vyama vya ushirika tunavyo vingi sana katika ukurasa huu na maafisa wanajitahidi kwenda kutoa taaluma, lakini hatimae wanakwambia nini kinachoendelea hakipo. Kwa hivyo, naomba sana tuwe na mageuzi ambayo yaliyokuwa na mwamko sana.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, ukurasa wa 36 masuala ya mkopo, mikopo kweli imetolewa nakubaliana nae, lakini jinsi ya taaluma ya urejeshaji tulifanya haraka katika kutoa mikopo, naomba sana mara hii itakapotoka mikopo tujaribu kutafuta njia ambazo zilizokuwa na taaluma nzuri, kwanza tuwafundishe watu wetu, tuwape somo la utafutaji wa soko, ndio madai tuweze kumpa mtu kwa sababu kuna biashara nyengine hazikubaliki kwa jamii, hazinunuliki hazina wingi wa watu, kuzipenda nalo hili ningeomba tutoe taaluma ili mtu ajue mkopo huu anapouchukua ajue kuurejesha kwa time inayokubalika. Naomba sana kwa hilo tujaribu sana kutoa taaluma kwa watu wetu ili mikopo hiyo isipate kuzunguka na nipate kurudi sio kila siku pale kwa pale tu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuendelea hapa, niingie katika *data* zako kidogo, naomba ukurasa wa 78 hili suala linanisikitisha sana tena linanitia huruma sana suala la kubakwa kwa watoto, namba hii ilikuwa zamani wakikamatwa vitangi wakitangaziwa, lakini hivi sasa sijasikia hata mmoja kwamba kakamatwa kitangi akatangaziwa. Naomba sana usione tabu kwa sababu sasa hivi hali halisi haipo nzuri sana na hasa katika chombo chetu kile cha jamii, mimi sijapata kukifahamu, naona nafungua mpira tu, nilikijaribu kwa Mhe. Abubakari akanirushia mpira akanambia hahusikia, lakini hapa sijui mtanambiaje, nani muhusika wa chombo hichi.

Mhe. Mwenyekiti, na hapa hatuko *serious*, hebu nawaombeni sana Waheshimiwa Wawakilishi hili suala tuling'ang'anieni ili tumsaidie mama huyu, tuwe makini na suala hili na kuna masuala mengine yanakuwa ya ukweli katika utendaji wa ile shutuma yenyewe, sasa hapa naomba sana kuwa tuwe wataalamu ili tuweze kujua hili la *fake*

na hili suala ambalo la kweli. Watu wanatenda kile kitengo vitoto vidogo na hasa vijanadume namba zinazidi kupanda na hao ndugu zetu wanaojitia mashehe wa vyuoni tumesikia ile kesi iliyokuwa inamdhalilisha yule mtoto, kwa kweli haileti sura.

Mhe. Mwenyekiti, ningekuwa na uwezo wa sheria na mimi basi ningetoa sheria kali sana, basi sidhani kama mtu mwengine angeweza kuthubutu kufanya kitendo kama hicho, lakini kwa kuwa ukitoa sheria kali sana, sheria ya mambo ya haki za binaadamu, dunia itakukemeya wewe, lakini sheria hiyo hata binadamu haioni kwamba yule mtoto naye kanyimwa haki yake ya kuweza kuishi duniani.

Mhe. Mwenyekiti, kinamama wanadhalilishwa sana hasa kwenye mitandao na sheria hii Mhe. Waziri, sijui mpaka sasa hivi umemchukulia hatua gani? Kinamama wanadhalilishwa na kina baba kwenye mtandao kwa kweli hili suala linasikitisha na linatoa imani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi namuomba sana Mhe. Waziri, hili si jambo la kufumbia macho kwa sababu binaadam tumeekeana kwa kukubaliana na kufichiana siri, lakini leo inakuja kuwa mmoja anafichua siri za kumdhalilisha mtu kwenye mtandao, Mhe. Waziri, ni jambo ambalo linasikitisha, ni jambo ambalo linatia uchungu kuwaona watoto wetu wanadhalilishwa kwenye mitandao, maneno mengine huwezi kusema utajiuliza kweli mwanangu anafanya kitendo hichi unalia machazi. Mhe. Waziri, nakuomba sana, ni jambo linaloumiza ndani ya nafsi, kwa nini tusitiwe adabu sisi akina baba?

Mhe. Mwenyekiti: Unadakika tano za ziada.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekikti, nipe hata kumi kwa suala la hapa niache niogolee, linaumiza sana, hili suala sisi tuna watoto, mimi na wewe tumeisha, lakini sisi tuna watoto wetu, hakuna mtu anayefurahi kuona mwanawe katolewa kwenye mtandano pengine wewe unafikiri vizuri vile, ni lazima hapa tuweke kitu cha msingi kabisa, ni jambo ambalo hamuendi kwenye mitandao, hamfuatilii kwenye mitandao ukishaona, basi umekwisha, sasa nimekwisha nini, mimi ndio maana nikasema leo nitakuwa mkali sana kwenye Wizara yako, nakufanyia ukali kutokana na marekebisho, tatizo wewe mama mimi naomba sana hili suala.

Mhe. Mwenyekikti, hili suala naliomba sana, Waheshimiwa wenye sheria wapo kama Mhe. Abubakar na Mhe. Mwanasheria Mkuu, naomba sana Mhe. Abubakar na Mwanasheria Mkuu tuleteeni sheria kali, kila siku ukifungua mtandao unakuta mtoto si kwa hiyari yake masikini ya Mungu, kwa sababu kuna vitu vya kisasa, mwanamme ndio unayejua anaweka kamera zake, wewe utaona mtu yupo kwenye *labtop* anachezea, kumbe muongo ameshaseti vitu vyake, jamani inasikitisha sana, hili linasikitisha sana sana, sikubaliani nalo kabisa.

Mhe. Mwenyekikti, hapa mimi nakuwa mchungu, sitounga mkono kwa asilimia yoyote, isipokuwa unakuja hapa Mhe. Waziri, unatafuta wanasheria wako, wanaokujua, unakuja unaniletea kitu tayari umeshaanda sheria kali za kuweza kuwadhibiti, hao watu tumechoka nao, watu wanaotiwa maneno na matusi, wanadhalilishwa matusi viongozi na mambo chungu nzima, kwa nini tustahamili kiasi hicho? Naomba sana hili jambo ulifanyie kazi kwa uaminifu kabisa, kwa sababu si vizuri na si uungwana kumkashifu mtu ambaye hakuwa na maridhaa yake mwenyewe ya kuweza kutoa.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa hili suala kama nilivyosema kuwa hichi chombo cha *DNA* niambiwe nani muhusika, si hivyo, vyengine vyovyote ukiwa wewe huna fungu, tulifanya harambee ngapi? Mfano tulifanya harambee za maji na harambee ya meli, kwa nini tushindwe kufanya harambee hiyo ya kupata chombo hicho ambacho kitatoa uhakika wa sheria? Kwa nini tushindwe hivo tuseme hatuko *serious* na jambo hilo na wakati watoto wetu wanadhalilika kama sio wangu mimi, ni wako wewe? Kama si asubuhi, ni mchana, basi mimi naomba sana nalo hili Mhe. Waziri, tulifanyie harambee kwa sababu najua ni *expensive* sana, chombo hicho si mchezo, lakini umoja wa Mataifa wapo tunaweza kwenda kuwaomba wenye haki zao za kutusaidia wapo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nizungumze la mwisho na la pili, vijana wetu wa *Scout*, nililisema sana suala hili, lakini naona bado lingali liko *very weak* sana katika utendaji wake, nakuomba sana Mhe.Waziri, hili bado ulilikamata mara ile nilikusifu sana lakini na mara hii naomba sana Mheshimiwa ulikamate sana kuweza kufanikisha ili wananchi wetu wale vijana wapate kujisikia, *Scout* ni moja katika chama kinachofundisha watu maadili mazuri, kinakusanya watoto waliokuwa hawataki kusoma, kinakusanya watoto wanaoashiria katika kuingia dimbwi baya

sasa, kwa nini kitu kama hicho hatuwezi tukakisaidia? Serikali ikasema sasa tupo makini kabisa katika kukisaidia, kama kuna hiyo Kamati ambayo imeundwa kwa kuifanya ifuatilie *Scout*, naomba sana lifuatilie.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho kwa vijana nataka kukuaga, vijana wako wengi na sasa hawana ajira, naomba sana umeonyesha hapa una mfuko mzuri sana na mfuko huu umewawezesha wananchi kiuchumi umeshazinduliwa rasmi, mimi nataka hapa mwenyewe usingojee mezani na kweli sijui umefanya ziara ngapi? Hebu na hili nataka uje kunambia katika *Departments* zako zote umefanya ziara ngapi Unguja na Pemba? Nataka nijue nalo hilo, kwa sababu hilo ni moja ambalo Mhe. Rais atapata vipimo vya kujua vipi mawaziri wao wanapotafuta matatizo kwa Idara zake ili kuweza kuleta maelezo yaliyokuwa sahihi. Naomba nalo hili uje kunijibu Mhe. Waziri, ili nikwachilie fungu lako uje kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wafuatiliwe kule sehemu za jimbo la Kitope wameshajiweka vizuri vijana wanakungojeeni na kinamama wameshajiweka vizuri kwa njia ya visanduku wanakungojeeni ili muwasaidie kuwawezesha, isiwe mjini tu na hili mimi sikubali, nataka uje unambie Jimbo la Kitope una asilimia mia kwa mia kwa mikopo uliyowapa, kwa sababu mna watu wameshapata mafunzo mazuri, nataka twenda ziara mimi na wewe kule ukaonyeshe *paylor* tena nakuhakikishia ukitaka ufanikiwe mfuko wako, njoo kule wale watu wameshasomeshwa bwana, wale watu wana taaluma nzuri. Ahsante sana.

Mhe.Mwenyekiti: Kabla hatujamkaribisha Mheshimiwa mwengine, ningependa niseme kitu kimoja ambacho Mhe. Mshimba alikuwa amekizungumza juu ya ujio wa Mwenyekiti, ambapo leo anasema kulikuwa kuna akinamama hapa wako chini na akinamama pia walikuwa wanatuongoza katika kuingia ndani na ilikuwa tulipanga Mwenyekiti Mgeni pia akae kwenye kiti hichi kwa siku ya leo, lakini kutokana na jukumu lile la Wizara ya Afya ambayo kesho tunataka tufanye majumuisho yake, imebidi sasa hivi akakae na Kamati baadae ili hoja ya Wizara hii iende leo na kesho asubuhi tufanye majumuisho na jioni tuweze kufanya majumuisho ya Wizara ya afya. Kwa hivyo, hiyo ndio inasababisha tuweze kuendelea na utaratibu huu, sasa tunamkaribisha Mhe. Moh'd Haji Khalid ili aendelee kuchangia na baadae bado huku kuna nafasi moja tu ya Mhe. Asha ambaye amekwenda juu kuungana na Kamati ya Mhe. Mgeni, kama kuna mwengine tunaomba atuletee maombi yake.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi asubuhi hii kupata nafasi ya kutoa yangu machache kuhusu Wizara hii ya Mhe. Zainab, nimpongeze Mhe. Zainab kwa jinsi alivyowasilisha ripoti yake kwa ufasaha na kwa *speed*, kwa kweli alikuwa kama charahani, *speed* yake anavyokwenda mbiyo, umri wake na *speed* yake haikubaliani, mtu anayesikiliza nje huko, atadhani ni mtoto mdogo, kumbe ni bibi mkubwa. Kwa hivyo, nampongeza kwa hatua yake hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika nimpongeze yeye na watendaji wake wanaomuwezesha na kumuandalia ripoti hii nzuri ambayo ameleta mbele yetu, baada ya hayo, nimeanza kinyume nyume nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha leo asubuhi kukutana hapa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi mpangilio ulipo hivi sasa kwako wewe na Makatibu ni sahihi kwa sababu umezingatia jinsia zote mbili, isingekuwa vyema kama wangelikuwa wote ni wa jinsia moja tu. Kwa hivyo, kuwepo kwako ni mpango sahihi kuliko kama angekuwapo Mhe. Mgeni, kwa sababu ingelikuwa wanawake wametawala peke yao, kumbe kwa sababu wanadai haki sawa. Kwa hivyo, na sisi tuwe haki sawa. Kwa hivyo, kukaa wewe umerekebisha mambo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo mfupi, mimi mazungumzo yangu yatakuwa mafupi sana na yatakwenda kwenye hivi viambatanisho tu, ndio nitakavyozungumzia mimi, nitaanza kwenye ukurasa wa 74 unaozungumzia utoaji wa mikopo kupitia mfuko wa kujitegemea. Kwenye ukurasa huu zimeorodheshwa wilaya zote za Unguja na Pemba na watu waliochukua mikopo nimetizama Wilaya yangu ya Mkoani kwenye jinsia wanawake wapo 11, wanaume 11 na vikundi 3, hivi ndivyo vilivyopata mikopo, lakini nikiangalia wilaya nyengine zote kidogo watu waliopata mikopo ni ya juu na hii Wilaya ya Mkoani kwa lugha yangu niseme ni ya mwisho. Ningependa tujaalie watu wa Mkoani hawajahamasika au hawana taarifa rasmi kwa mkopo huu na kama hawajahamasika ningeomba wahamasishwe ili na wao wajiunge kutafuta mikopo hii ambayo itaweza kuendeleza katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, kama tuko nyuma wenyewe tu, basi ningeomba wenzangu wa Wilaya ya Mkoani mikopo hii ipo tujitokezeni tuiombe ili nasi tuende sambamba na wilaya nyengine, mimi hapa naona aibu kabisa kuwa ni watu 22 tu na vikundi vitatu tu, ndio vilivyoomba mikopo hii, wakati ambao tupo watu wengi na viko vikundi vingi, lakini bado tumejificha hatujajitokeza. Kwa hivyo, ombi langu kama ni ukosefu wa taaluma, ningeomba Wizara ituongezee

taaluma sisi watu wa Mkoani ili tuweze kuungana na wenzetu katika kutafuta mikopo hii, kama ni kujiweka nyuma sisi wenyewe tusikae nyuma tujitokeze tuwe mbele na tuweze kuwapita hao waliokwisha tangulia mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi sasa nije katika ukurasa wa 78, mimi nimesema nitakuwa nachangia hivi viambatanisho peke yake, ukurasa wa 78 na 79 unaonyesha udhalilishaji unaofanyika kwa vijana wetu, lakini 78 niuwache tujadili zaidi ukurasa wa 79.

Mhe. Mwenyekiti, kulingana na taarifa iliyoko hapa, hali ni mbaya tena mbaya sana, kwa mfano vijana chini ya umri wa miaka 18 waliobakwa kwa Unguja peke yake na ambao wametambuliwa wapo wengine bado hawakutambuliwa, lakini wale waliotambuliwa ni 331, zaidi ya miaka 18 ni 17 na wanawake, ina maana hawa watu wazima ni 501. Hali hii ni mbaya haileti sura nzuri kwa nchi yetu na kuna haja ya kupiga vita kwa nguvu zetu zote.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii tuikemee, tuikatae, tuichukie na tusiikubali, wale watakaobainika na ikathibitika, basi hatua kali za kisheria dhidi yao zichukuliwe. Vitendo hivi vya ubakaji bahati mbaya vinafanywa na watu wa rika zote, ni jambo lisilofurahisha ukamkuta mtu wa umri wa miaka 50 kwenda juu nae kuwa yumo katika orodha ya wabakaji ni jambo baya, lakini vijana wadogo kama waliotajwa hapa chini ya miaka 18 na hawa wenye miaka 18, miaka 18 naweka kando nichukulie hawa zaidi ya miaka 18, wengine 18 hadi 25 ambao umri huu unaweza kuwa ni *genders age*, ni umri wa hatari, ni umri wa *teenagers* ni umri wa hatari.

Mhe. Mwenyekiti, mtu anapovuka katika umri huu baina ya miaka 18 mpaka 25 na 30 kama hajafanya kitendo kibaya huenda Mwenyezi Mungu akamuongoa asifanye tena, ndio maana umri huu unaitwa ni *dangerous age*. Kama hajalewa si rahisi tena kuingia katika ulevi, kama hajaiba si rahisi tena kuwa mwizi na kadhalika na kadhalika. Sasa umri huu ni umri wa hatari na kulingana na tabia za nchi yetu ilivyo, hivi sasa ukiacha hawa watoto wadogo ambao hawavutii kwa chochote, lakini hawa kuanzia miaka 14 kwenda juu wa kike na wa kiume, moja linaloshawishi ni namna ya mavazi yao. Mavazi kwa kima fulani kwa vijana ambao madhubuti, bado viwiliwili vyao vinavutia kujiingiza katika vitendo hivyo vibovu, vibaya na visivyokubalika.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa kuwa haya mavazi ni moja ya chanzo cha maovu haya na sisi ndio wazazi tunayempa mtoto wetu kikanzu hicho ambacho chamfanya mwenzake mwengine aliyevaa suruali inayoning'inia amfate. Ningeomba tuweke sheria angalau mavazi ya heshima, huenda pengine yakasaidia kidogo na pia kuna sheria ngumu ya watu watakaobainika wamefanya vitendo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, hicho ni kitendo kimoja tu cha ubakaji, kuna kitendo kibaya zaidi cha kulawiti. Vitendo hivi navyo vinaongezeka siku hadi siku ambacho ndio kibaya zaidi kuliko kile cha mwanzo. Jinsi vinavyoendelea na dunia inavyoendelea, hofu yangu watu hawa wasije wakaunda Jumuiya hatimaye na wao wakaomba wasajiliwe kutambulika rasmi. Kulingana na hali ilivyo na wito wa kidunia ambao hauzingatii lolote kwa kutegemea ile haki za mwanaadamu kwa kuonekana kuwa ni haki yao, lakini kwa hapa kwetu kuna haki nyengine si haki kuzifanya kuwa ni haki, ni kwenda kinyume na haki. Haki ya watu hawa wakija wakaomba kwamba na wao watambuliwe kisheria, kwa kweli naomba Mwenyezi Mungu mimi humu niwe simo tena kuja kuthibitisha kuwa watu wanaolawitiana watambuliwe kisheria. Tunakoelekea jambo linaelekea huko.

Mhe. Mwenyekiti, wapo waliopewa mimba chini ya miaka 18 kwa Unguja peke yake wapo 127 waliotambuliwa. Sasa mimba ipo pengine msichana kasema kuwa ni bwana X, lakini Mahakamani tunasema hakuna ushahidi. Wanasheria katika dunia ni watu wa aina peke yao, kwa sababu wao wanalolichunguza ni nani kajieleza vyema. Mtu anaweza akashtaki na hatimaye aliyeshtaki shtaka likamgeukia, ikawa mkosa yeye kulingana alivyojieleza. Kwa sababu hawa wanasheria ni wataalamu kwa kupanga hivi na lile mpaka likaelekea vile zaidi ya waliokuwa mawakili, kwa sababu wanataka washinde kesi, lakini mimi ninahisi kijana kapewa mimba kamtaja bwana X na kila anapohojiwa, habadilishi kusema ana bwana Y na bwana P, lakini kila anapohojiwa ni X, X, X. Kwa sababu vitendo hivi mara nyingi havifanyiki hadharani ushahidi wa kuja mtu akasema nimewaona ni mgumu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa, una dakika tano ya ziada.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Mwenyekiti, zinanitosha kwa sababu mimi nilisema sitaki nizungumze sana, ushahidi wa kusema mtu kuwa nimewaona ni mgumu. Sasa yule mtendwa na mtenda wangetosha kujadiliana kama bado ana akili zake timamu yule mtoto wa kike, bila kupata ushahidi wowote yeye mtendwa na mtendaji washindane Mahakamani na pengine yule mtoto anaweza akashinda kwa kutoa vielelezo, walikuwa wapi, siku gani

na walifanyaje, lakini katika ushahidi mwengine ni huo wa kitaalamu ambacho hicho chombo bado hakijakuwepo. Je, kwa sababu chombo hiki hatunacho ndio watoto wetu wanaodhalilishwa wasipate haki kwa kukosekana hiki chombo? Je, itakuwa kafanya haki juu ya vitendo hivi viovu vinavyofanyika?

Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo ambalo lazima sisi kama watunga sheria niiombe Wizara hii itengeneze Mswada wa Sheria utakaoletwa hapa juu ya vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Vyenginevyo, tutafikia pahala ambapo hatukutegemea kufikia.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitabu hiki Mhe. Waziri, alizungumzia viambatisho hivi ukurasa wa 70, ajira mpya. Hapa kuna ajira mpya, uhamisho kwa waliofariki dunia na walioacha kazi Unguja na Pemba. Ajira mpya Unguja kuna wanawake nafikiri ndio wanawake 4, wanaume 9, wote ni 13, Pemba Wanawake 0, Wanaume 0, Jumla 0, wanawake 4, wanaume 9, jumla 13. Nimuulize tu swali dogo Mhe. Waziri, hiyo Ofisi yako ya Pemba kwa kipindi hicho ilikuwa haina haja ya kuongeza ajira kwa vijana wako? Baada ya hayo machache, mimi nitamuunga mkono Mhe. Waziri, kwa asilimia 99.99, hiyo *point* moja ninaweka ya kibinaadamu. Ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Pili, napenda kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri kuwa kuisoma kwa ufasaha kabisa, nampongeza Katibu Mkuu wake, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo wanayoifanya na pia, nawapongeza kwa kazi kubwa ya kumsaidia Mhe. Waziri ili kufanikisha majukumu yake ya kila siku.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia katika maeneo 3; Eneo la kwanza suala zima la udhalilishaji, pili, fedha zilizochangwa kwa ajili ya michango ya mwenge na tatu, suala la vikundi mbali mbali ambavyo vimeainishwa humu vilivyotembelewa na watendaji katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 78, kiambatanisho namba 7(a) kimeeleza ripoti ya uzalishaji kwa masuala mbali mbali ya kubaka, kulawitiwa na katika ukurasa wa 79, wameeleza suala zima la kituo cha *One Stop Centre* ambapo wameeleza takwimu, hapa suala la kubakwa watoto chini ya miaka 18 kwa kipindi hiki cha Julai/Machi ni watoto 331 na zaidi ya miaka 18 wameeleza waliobakwa ni 501, jumla ni 849.

Mhe. Mwenyekiti, hali hii si nzuri, hii idadi ni kubwa na hii ndio iliyojitokeza kuna wengine wanapata matokeo hayo, lakini hawajitokezi wanasuluhishwa huko huko mitaani. Wanakaa wanaitana tu wazee wanamaliza, lakini hawa ndio waliojitokeza hali hii. Kwa hivyo, hili swali ni kubwa. Naiomba wizara izidi kujitahidi ili kuhakikisha kwamba vitendo kama hivi vya kuwanyanyasa watoto wetu chini ya miaka 18 wafanye matendo ambayo bado umri wao hawajawaruhusu kufanywa, naomba Mhe. Waziri, afanye mikakati ya makusudi ili aweze kulipunguza zaidi tukio hili, kwa sababu ni tukio si zuri na linawadhalilisha watoto wetu, linawaharibu hata kisaikolojia na wanashindwa hata kupata muelekeo mzima wa maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika fedha zilizochangiwa na mchango wa mwenge.Hapa napenda niwapongeze tu Wakuu wa Mikoa wote ambao wamefanya michango hii na zimetajwa hapa zile gharama ambazo zimekwenda katika shughuli mbali mbali za maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, katika *page* ya 92, imeelezwa Mikoa mbali mbali hapa ambayo imeainishwa kutokana na fedha ambazo zimechangiwa na Mwenge na fedha hizi zimeoneshwa kwamba zimeenda katika shughuli mbali mbali za maendeleo katika majimbo na shehia zetu na katika Mkoa wa Mjini Magharibi imeelezwa kiasi cha 16,070,850, Mkoa wa Kaskazini wameeleza hapa 16,746,340, Mkoa wa Kusini pia 7,362,450, Kaskazini Pemba 11,350,000 na Mkoa wa Kusini Pemba 14,565,000.

Mhe. Mwenyekiti, hizi pesa zimechangwa na wananchi au na wafanyabiashara mbali mbali ili kuendeleza mwenge, lakini mwenge huo huo pesa zile zile zinasaidia wananchi kwa shughuli mbali mbali za kijamii, lakini katika ripoti yake Mhe. Waziri, katika Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini, ndio walioeleza mchanganuo mzima wa hizi pesa ambazo zimeenda katika miradi mbali mbali katika majimbo na shehia. Ni Mkoa wa Mjini Magharibi ambao umeeleza katika kitabu hiki ni miradi karibu 27, fedha hizi zimepelekwa katika majibu ili kuendeleza miradi hiyo. Katika Mkoa wa Kusini imeelezwa ni miradi 10, lakini hii Mikoa mengine haijaeleza mchanganuo wa miradi ambayo fedha hizi zimepelekwa na katika kitabu kimeonesha kama pesa zimetolewa katika Mikoa hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hapa nilikuwa naomba Mhe. Waziri hii Mikoa mengine ni Mikoa 5, lakini Mikoa 2 tu ambayo imeeleza mchanganuo huo. Je, fedha hizo walizotengewa humu ambazo zimeainishwa hii Mikoa iliyobaki 3, tuna uhakika zimefika kwa walengwa katika shughuli mbali mbali za miradi ya wananchi, nilikuwa naomba nipate maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, hapa nitakwenda katika hivi vikundi mbali mbali ambavyo vimo katika majimbo yetu, vikundi ambavyo vijana wetu wamejikusanya wanafanya shughuli mbali mbali za maendeleo na wameeleza katika ripoti vikundi walivyotembelea ni 103 mbali mbali katika jamii. Vikundi ni vingi, lakini pia, vikundi hivi vinahitaji *support* ili waweze kuendeleza shughuli mbali mbali na kujipatia kipato katika maisha yao. Pia, zinasaidia vijana wetu kujishughulisha na kupunguza tatizo zima la ajira.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hapa kuna *page* hii ya 94 wameeleza hapa kama kuna vikundi vilivyohitaji mikakati maalum ili uweze kurejesha mikopo yao na vikundi vyenyewe vimetajwa hapa. Sivibaya/Chake Chake cha kwanza, cha pili Takawani/Chumvi, cha tatu Jiendeleze/Wingwi, cha nne Kidutani kiko Sizini hiki, cha tano Uchozini hiki kiko Wete, cha sita Tupendane kiko Piki, Tundwa *Cooperative* nacho hiki kiko Piki, cha nane Mambo/Pujini, tisa Tarijika/Mkoani na cha kumi ni *Creative-SACCOS*. Sasa hapa Mhe. Waziri, nilikuwa naomba anieleze kwa nini vikundi hivi viweke mikakati maalum ili viweze kurejesha mikopo? Vina matatizo au vikipewa mikope havikopesheki, vikikopeshwa pengine vinakuwa havirejeshi mikopo, nilikuwa naomba nipate maelezo maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu vikundi vyengine vimeeleza, lakini hivi vinahitaji mikakati maalum na kama ni hivyo, huku kuna vikundi vingi tu ambavyo vimeorodheshwa humu na hivi pia vinahitaji *support* kuendeleza katika shughuli zao.Vikundi kama hivi vimeoredheshwa na vilitakiwa viwekewe mikakati maalum, labda hayo maelezo nikipata naweza nikaridhi, lakini kama vitakuwa vina matatizo havikopesheki, basi tuangalie vikundi vyengine ambavyo vyenye kukopesheka.

Mhe. Mwenyekiti, halafu nilikuwa nitoe angalizo, humu tumeeleza vikundi mbali mbali vimo, lakini kuna vyengine ni vikundi vya zamani kabisa ambavyo vinaendeleza shughuli zao, lakini *support* hawapati na vina uwezo mzuri wa kufanya shughuli mbali mbali za kujiendeleza. Naomba nimpe tahadhari Mhe. Waziri pakizuka mfuko kama huu ambao wa kuwawezesha vijana wetu kujiendeleza na kufanya shughuli mbali mbali na vikundi vinaibuka na vyengine vinaibuka leo, vyengine kesho, lakini tutavisahau vile vikundi ambavyo vina miaka nenda miaka rudi, lakini viko *active* hivyo kutokana na kutokosa *support* vinashindwa kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri, aviangalie vikundi ambavyo ni vya muda mrefu ambavyo vipo na wamejishughulisha tangu zamani wanashindwa kupata misaada kama hii. Kuliko kuviangalia vile ambavyo vinaibuka tu vimesikia mfuko, basi vinaundwa hapo hapo na hivyo, pengine ndiyo vinapewa kipaumbele zaidi. Tuviangalie vile vikundi ambavyo vipo miaka mingi na vinafanya kazi vizuri, lakini vinashindwa kupata *support*. Baada ya kusema hayo, naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru asubuhi hii ya leo kunipa fursa na mimi kuwa jamii ya wachangiaji wa hotuba hii ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto zote ziko kwake yeye. Kwa hiyo, nashukuru na mimi kunipatia fursa hii kuchangia hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi nataka nigusie kidogo hapo alipomalizia mchangiaji aliyekaa kitako Mhe. Marina kuhusu suala hili la ubakaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nikiri kama idadi hii ya watoto 300 ni kubwa sana, na ni kubwa yakutisha, hasa ukizingatia utaona kama hiki kitendo cha ubakaji kwa Zanzibar kimekithiri na kikubwa sana. Pia, ni kweli kabisa kama hili suala linatakiwa hasa lifanyiwe ufumbuzi ili lipungue au ikiwezekana liondoke kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema pamoja na hali hii ya ubakaji, lakini jamani na sisi wazee wa watoto kidogo tunachangia hili suala kuendelea kuwepo. Nikisema tunachangia, nina maana yangu nasema kwa sababu ni ukweli kama kuna haki za binadamu, lakini haki za binadamu zimekuwa kubwa mpaka zimekithiri kwa sababu watoto wetu tunawapa uhuru mkubwa zaidi na huo uhuru mkubwa tunaowapa ndiyo unaochangia zaidi kuwa watoto wabakwe. Kwa sababu kuna watoto wanaobakwa wadogo, lakini kuna wakubwa na wao wanabakwa.

Mhe. Mwenyekiti, huu ubakaji mimi nasema mpaka mtu mzima anabakwa, kwa sababu kubaka kwa mimi ninavyoelewa ni kumshika mtu kwa nguvu bila ya ridhaa yake, ndiyo najua maana ya kubaka. Kwa hiyo, hata mtu mzima anabakwa, kama utamkuta mtu kwenye mapori anatafuta kuni bila ya ridhaa yake ukamshika kwa nguvu, basi umeshambaka.

Mhe. Mwenyekiti, hii sheria yetu ya ubakaji pia nasema kuna sehemu moja ambayo nayo ina mapungufu tunaifanya kama ni ya kubaka na pengine inakuwa si kubaka, kwa sababu kama watu wamekubaliana kwa ridhaa yao, si kubaka. Mimi nasema kubaka ni mtu anayeshikwa kwa nguvu, lakini watu wanaokwenda wakaambiana maneno wenyewe wakakubaliana, si kubaka.

Mhe. Mwenyekiti, wazee tunachangia kwa sababu watoto tunawapa uhuru mkubwa, haiwezekani nyumbani unamuona mtoto wako anavaa nguo za kimaajabu baba na mama mtu yupo, wewe baba unahimiza mtoto aende akashone nguo za maajabu, anakuja humwambii kitu, hivyo mtu huyo akitoka akienda nje akikuta vijana wako kwenye maskani yao anapita na nguo za maajabu, vijana lazima anawashughulisha, akiwashughulisha watu watamtega na wakimtega mwisho watambaka, lakini wazee tupo watoto tunawaachia uhuru ambao umekuwa mkubwa mpaka umekithiri. Jamani watoto wetu tunawalea sisi wenyewe, hivi kwa sababu zamani ilikuwa masuala ya kubaka yalikuwa hayako kama hivi na Zanzibar ni hii haijabadilika, Unguja na Pemba ni hii hii na watu wake ni wale wale waliopo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi watu wamekithiri kubaka kwa sababu ya matamanio, watu wanawatamanisha kwa sababbu ya maajabu ya nguo na watoto tunawapa uhuru mkubwa, mtoto anatoka nyumbani anarudi saa nne, saa tano, saa sita, haambiwi chochote au unamuona mtoto anakuja asubuhi amejipamba hata mama yake hajajipamba kama anaavyojipamba mtoto. Wewe unamuacha mtoto wako anatoka anaenda na shughuli zake, halafu watu wasibakwe, watabakwa watu kwa namna hii. Lazima kama ni hivyo, tuweke sheria, lakini na hawa watoto wetu tuwawekee sheria kwa sababu mambo yamekithiri, watoto tunawapa uhuru mno, haiwezekani mtoto anakuja nyumbani, hata akija anatoka na simu ya shilingi milioni mbili, wewe mama husemi kitu chochote na baba pia husemi, akenda huku lazima atabakwa tu. Mtoto ameshachukua simu ya watu lazima atabakwa tu, kwa maana hiyo, nasema malezi yetu lazima turudi na malezi yetu ya zamani tabia tutazozichukua hizi si tabia nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, wewe umepewa jukumu la wanawake na watoto. Kwa hiyo, wewe unatakiwa ukemee wazee wenzako, uwaelekeze wazee wenzako kwamba turudi tuwalee watoto kama tulivyokuwa tukiwalea zamani. Zamani kwanza ilikuwa hakuna mtoto wako ilikuwa mtoto yule ni wako wewe, lakini na mzee wa mwenzako anakusaidia ulezi. Sasa hivi hakuna mtu yeyote anayemsaidia ulezi mtoto wa mwenzake na hii yote ni tabia yetu tunayoifanya kwa sababu mtu hawezi kumkemea mtoto wa mwenzake.

Mhe. Mwenyekiti, zamani ilikuwa mtoto wa mwenzako anakukemea, mimi nathubutu kusema kama hapana hapa sehemu moja mzee anaweza kutoka na mzigo aende zake nyumbani akamkuta mtoto njiani akampokea. Zamani ilikuwa ukitoka na mzigo haufiki nyumbani wanaunyanyua watoto kumi, lakini sasa hivi hakuna mtoto anayemsaidia mtu. Jamani malezi tumeyaacha malezi yetu, silka yetu ya Zanzibar tumeiacha lazima tujirudi jamani na kama tukikubali kujirudi na Mwenyezi Mungu atatusaidia. Mwenyezi Mungu hawezi kutusaidia bila ya kujirudi, kwa sababu Mwenyezi Mungu anasema hawezi kubadilisha kitu mpaka muanze kubadilika, nyinyi wenyewe muanze kubadilika, basi na Mwenyezi Mungu atawabadilishia.

Mhe. Mwenyekiti, lakini siyo bwana tumebadilika tumeacha tabia zetu, tumeacha mila zetu tufanye nini, vijana wetu lazima waharibike. Leo kuna kesi 300 za kubaka jamani kesi 300 ni nyingi kweli kweli msifanye masihara. Kwa hiyo, mambo haya ya vitendo vya kubaka vinaongezeka kutokana na hali tunavyoiacha tumeacha wazi hatuna kizuizi. Jamani tusifanye hivi tujirudini. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni moja.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninalotaka kulizugumzia kama ninavyozungumza kama wewe umepewa uwezeshaji wananchi kiuchumi. Kwanza nataka nikulaumu ikiwa nitalolisema ndilo nitakulaumu, sina uhakika, lakini nasikia jana ulikuwa Micheweni kufungua hilo suala la uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa ajili ya kuzindua mfuko huo, lakini mimi Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni na mimi ndiye mwenyeji wa lile jimbo la Micheweni na kila siku mimi nawalaumu Mawaziri kama mkifanya mambo yenu hamtwambii, sasa kama hamtwambii tukija tukiwalaumu tutapata cha kuwalaumu. Kwa sababu shughuli imekwenda kufanyika katika Jimbo la Micheweni, mimi mwenyeji wa Micheweni nipo hapa tuko pamoja, basi usingelinong'oneza tukaondoka pamoja, lakini umekwenda Micheweni, mimi mwenyeji wako siko, hilo nalo nakulaumu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka nikulaumu, je, nakuuliza Micheweni kila kitabu ninachokifungua unaona Micheweni inaongoza kwa umasikini. Kipindi kilichopita nilisema na leo narudia tena kulisema kwa sababu sauti ya Micheweni kwa muda huu, ninayewasemea ni mimi ndiye mdomo wao, watu wa Micheweni walinituma nije niwasemee mimi, nakubali kama Micheweni Mwenyezi Mungu ametujaalia ni sehemu moja ya umasikini, na ni sehemu moja ambayo inakuwa na ukame kwa sababu sisi tunapata mvua kwa msimu maalum na jua likitoka kweli kweli Micheweni ukija majani yake yote yameungua.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niliwaambia kipindi kilichopita, je, serikali ina mpango gani wa kudumu wa kuwasaidia watu wa Micheweni ili wanajinasua na wao kuondokana na haya masuala na ndiyo maana ukaona kwamba kuna vijana wengi Micheweni wanaojiajiri ni nyingi. Ni kweli kwa sababu lazima iwe hivyo, kwani hali ni mbaya mtoto atakwenda shule kama hajapata chakula hawezi kwenda akasoma akili ikafanya kazi, kama anataka kwenda shule ikiwa hana *uniform* za shule hawezi kwenda. Ni kwa sababu kuna ukame, lazima wajisaidie wao na wawasaidie na wazee wao.

Mhe. Mwenyekiti, je, wewe kama umepewa nafasi hii ya uwezeshaji wananchi kiuchumi, una mpango gani wa kudumu wa kuwasaidia wananchi wa Micheweni ili waondokane na suala hili la matatizo yao katika jimbo lao ikiwa wao, ni watu ambao kuwa wana jimbo kame, kwa sababu nilisema kama kwenda kuwasaidia chakula haliondoki, kwa sababu leo mfano watasaidiwa chakula wakishasaidiwa chakula kitaliwa na siku ya pili hakipo, hutarudi tena siku ya pili pale pale kwenda kuwasaidiwa, lakini wanataka kusaidia nyenzo za kujiendeleza na iwe ni za kudumu ili kuondoa ule umasikini, kwa sababu tukisema kwenye vitabu kama ni masikini ikawa hatuwasaidii nyenzo itakuwa bado.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naiomba serikali kupitia wizara yako iwaangalie watu wa Jimbo la Micheweni na iwaandalie mpango maalum wakati ule Mhe. Waziri wa Elimu, kabla hajaja Wizara ya Elimu nilizungumza akaniambia kwamba kule tumemuwekea kijiji cha *Millennium*. Sasa nilimuuliza Mheshimiwa kijiji cha *Millennium* watu hawali na hiki ni cha muda mrefu, akaniambia mimi nataka nije nitoe kwenye jimbo langu basi, lakini sasa ni kweli ni maendeleo kijiji cha *Millennium*, lakini ni mpango wa muda mrefu siyo wa leo leo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa lile suala la kuwasaidia wananchi kila leo ambapo serikali itaandaa mpango maalum. Hivyo, vikundi vinavyoandaliwa, lakini wakawezeshwa kwa nyenzo. Kule kuna mawe watu wanabanja mawe, saa zote wanajibanja vidole kwa kubanja mawe walisema wataletewa *machine* wakaambiwa hii kwamba itawasaidia. Hivyo, wanaweza wakajiendeleza ikawa ni mpango maalum, lakini sasa mipango hiyo nakuachia wewe nisikupangie mimi. Mimi nakuuliza tu kama utanijibu umeandaa mpango gani wa kuwasaidia wananchi wa Micheweni kuweza kuwawezesha ili kupunguza huo ukame wa umasikini. Hilo ni suala jengine.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine amelizungumza kuhusu suala la ajira kwa watu wetu, serikali lazima ijipange na hili suala la ajira umepewa wewe. Kwa hiyo, wewe ndiye unayetakiwa uikumbushe serikali kama vijana wetu walio wengi ajira hawana na ajira zinapatikana kwa serikali na watu binafsi na mashirika na taasisi, lakini sasa hizo taasisi na mashirika lazima zipitie kwako, wewe ndiye utakayetafuta hizo ajira kwa vijana wetu kwa sababu dhamana hii umepewa wewe.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo nataka nikuulize ni suala la mwenge, kunakuwa na mbio za mwenge, lakini mbio hizi zikija watu huwa wanachangisha fedha na zinachangishwa fedha nyingi kwa ajili ya kufanya maendeleo. Sasa mimi naomba niulize kitu kimoja kwa sababu hili suala la mwenge limefanywa kama ni suala la Muungano, ukilitizama kwa mtizamo hivi liko kama la Muungano, kwa sababu mwenge unaanza kuwashwa Kilimanjaro unakujamalizia Micheweni au unawashwa Micheweni unaenda kumalizia Kigoma. Sasa hizi fedha zikishakuchangwa za mbio za mwenge, je, zinagaiwa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar au zinakuwaje? Na kama zinagaiwa kama za Tanzania Bara, zinatumika kule na za Zanzibar zinatumika huku, je, vile zikishachangwa hazikaliwi kitako zikachambuliwa matumizi yake, huwa zinatumiwa tu? Na je, kama zinatumiwa, hatuoni kama kuna wilaya nyengine hazifaidiki na maendeleo ya mchango huu wa mwenge na wakati na wao wanachangia na majimbo mengine ambayo yanachangia?

Mhe. Mwenyekiti, naomba hili atakapokuja Mhe. Waziri, unieleze ili nijue kama je, hizi pesa zikishachangwa zinagaiwa Kitaifa, yaani zinagaiwa zile za Bara na za Zanzibar zinachanganywa, halafu zikagaiwa hizi za Zanzibar

na hizi za Tanzania Bara au je, za kule zinatumika kule na za kisiwani zinakaa huku, halafu zikatumiwa kwa vipi? Mgao wake wa matumizi unakuwaje? Hilo ni suala jengine ambalo nataka ukija ulieleze.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tatu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, suala jengine katika ukurasa wa 49, kama kuna uhamasishaji wa Baraza hili la Vijana baina ya nchi nyengine na nchi yetu ya Zanzibar. Sasa nilikuwa nataka unifafanulie katika huu uhamasishaji, je, ni nchi ngapi ambazo mmefaulu kuweka uhusiano juu ya hawa vijana baina ya nchi yao na nchi yetu? Na je, vijana wetu hawa wa Zanzibar wamekwenda nchi gani kujifundisha kuona aidha Mabaraza ya Vijana au Maendeleo ya Vijana katika nchi nyengine? Na je, ni nchi gani ambayo imekuja Zanzibar kwa mashirikiano kuja ikaona wale vijana wetu jinsi ya uendelezaji wa vijana ulivyo? Na hili nalo naomba kama lipo unisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, la mwisho ambalo namalizia ni suala la uundwaji wa Baraza hili la Vijana. Hili Baraza limeshasemwa sana na limeshaahidiwa sana. Hivyo, naomba serikali ione kama sasa ni wakati wa utekelezaji, maana tumeshasema sana mpaka sheria tumeshapitisha. Kwa hiyo, naona sasa iwe ni wakati wa utekelezaji hili Baraza liundwe na tuone kama limeundwa hili Baraza ili liweze kufanya kazi na tuone maendeleo ya Baraza la Vijana wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo, nitaomba majibu anipe akiwa atanijibu vizuri, kwa sababu sina nia ya kuja kumpigia buti, wala kumzuilia vifungu vyovyote. Kwa hiyo, naomba majibu, kama sitapata majibu ndiyo nitapiga buti ili kupata ufafanuzi zaidi, lakini sina nia ya kumzuilia, naunga mkono.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu *Subhanahuh Wataalah* aliyetujaalia uhai, lakini pia, akatupa na uzima na akatuwezesha kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, pia, nikushukuru na wewe kunipatia na mimi nafasi yakuweza kutoa mchango wangu mfupi katika wizara hii. Niseme kwamba nampongeza sana Mhe. Waziri, kwa uwasilishaji wake mzuri tena amekwenda kwa *speed* sana. Pia, niwapongeze sana kabisa watendaji wa wizara hii. Baada ya utangulizi wangu huo wa kupongeza, niseme kwamba wizara hii imebebeshwa mzigo mkubwa ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa, lakini pia, ina malezi ya wanawake, wazee na watoto. Kama utafanya mchanganuo, utaona hasa jinsi wizara hii ilivyo na majukumu yaliyo mazito kabisa, kiutendaji ni sawa na kusema kwamba mambo mengi ya wizara hii yanavutana mno na wizara nyengine mbali mbali. Ukiiangalia kwa undani utaona hasa kwamba hii wizara mikono yake mingi imepenya ndani ya wizara mbali mbali, kitovu chao kinaanza katika wizara hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze na mchango wangu labda kwa kutaka ufafanuzi kidogo katika ukurasa wa 60 wa kitabu hiki katika jadweli au kiambatanisho. Niseme kwamba nimeona kuna Idara ya Wanawake na Watoto, nataka nipate ufafanuzi. Nimeona kuwa makadirio yao katika mwaka 2013/2014 wanasema kuwa wametaka shilingi 103,000,000 mishahara, lakini kilichopatikana ni shilingi 90,000,000. Ningemuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa aniambie je, akisema makadirio na mapato yake kwa mishahara yanakuwa hakuna makadirio? Maana yake mshahara ni mshahara tu. Kwa hiyo, anambie kwa nini alipata shilingi 90,000,000; alipunguza wafanyakazi au kulikoni. Kwa sababu katika mishahara makisio yake yalikuwa hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili, ni hili la mikopo, nimeona mshahara wao ni shilingi 98,000,000 makadirio, lakini wamepata shilingi 107,000,000. Hapa ameongeza wafanyakazi au vipi? Ningependa kujua hilo.

Mhe. Mwenyekiti, la tatu, ni uwezeshaji, nimeona kwamba matukio yake yalikuwa shilingi 71,000,000, lakini amepata shilingi 54,000,000, je, amepunguza wafanyakazi? Baada ya kupata ufafanuzi huo, niendelee na mchango wangu ukurasa wa 55 wa kitabu hiki juu ya Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika kitabu hiki kuwa kumepokewa malalamiko 119 yanayohusu wanawake, nilipoyaangalia katika mchanganuo nimeona kwamba Pemba kuna malalamiko 95 na 24 kwa Unguja. Mhe. Waziri, atakapokuja hapa ningeomba anieleze labda amewahi kufanya utafiti wowote kuhusu kuonekana kwamba malalamiko mengi yanapatikana katika Kisiwa cha Pemba kuliko Unguja na kuona ni tatizo gani hasa kwa upande wa Pemba linawakwaza wanawake mpaka wakawa na malalamiko mengi zaidi kuliko hapa Unguja?

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba wanawake kwa kweli tunakwazwa na mambo na vikwazo vingi. Mhe. Waziri, nimuulize anayo taarifa ya wanawake au amefuatilia vipi kuhusu wanawake wanaoajiriwa katika mahoteli ambao mara nyingi hufukuzwa kiholela na kukosa haki zao na mikataba yao iliyokuwa haieleweki na kuwapelekea wanawake hawa kupata matatizo? Kwa upande wake Mhe. Waziri, kwa wanawake ambao wanafanya kazi katika mahoteli na sehemu mbali mbali wamewashughulikiaje kuhusu haki zao za msingi?

Mhe. Mwenyekiti, pia, kwa mahotelini kama nilivyosema mwanzo kuwa wizara yake imekutana na mambo mbali mbali na inagusa kila sekta, vijana nao naomba anipatie jibu, vijana hawa ambao mikataba yao inakuwa haieleweki vizuri na mara nyengine hufukuzwa, hukosa haki zao, hebu aniambie yeye kama waziri ambaye anahusika na vijana na wanawake katika ajira hizi za mahoteli ameshirikiana vipi na Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kuhusu habari hii.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu niende katika ukurasa wa 42 katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Kuna kesi nyingi ambazo zimeripotiwa za udhalilishaji kama walivyosema wenzangu. Kwa hakika niseme kama alivyoligusa kidogo Mhe. Subeit Khamis Faki, tatizo la ubakaji na udhalilishaji Zanzibar, tumekiuka mila na tamaduni za Kizanzibari. Tuna mila na silka zetu, tuna tamaduni zetu ambazo mara nyingi wageni wengi wanapokuja Zanzibar huvutiwa na hizo tamaduni zetu, leo tumekwenda mbali mno katika utandawazi, hali imekuwa ngumu kwa upande wa Zanzibar. Jambo hili ni gumu, ni zito na lazima kwa wakati huu sasa tulivalie njuga ipasavyo ili kurejesha zile tamaduni zetu tulizokuwanazo au walizokuwanazo wazee wetu waliotangulia.

Mhe. Mwenyekiti, leo tumeacha kuleleana hata watoto wetu, kila mtu analea mwanawe, imefika mahala mtoto hata umuone kutwa nzima kacheza hapo hakwenda chuoni au hakwenda skuli, unaingia na gari yako, unaingia ndani kwako ukitoka bado unamuona yupo muda wa chuoni au skuli, huwezi kumuuliza, tamaduni hazikuwa hivi. Ustaarabu wetu hasa Wazanzibari haukuwa huu, hebu tujiulize kulikoni. Niiombe sana jamii maana serikali itashughulikia kiserikali nayo nasema kwamba ina taratibu zake ilizojiwekea za kisheria na kimahakama. Kwa upande wa serikali juu ya kesi hizi imegonga mwamba haina hukumu, ndio kweli kwa sababu jibu la kesi hizi zilizotajwa zote zimebakia vile vile isipokuwa kesi nne tu ndizo zilizotolewa hukumu, mbili hukumu, mbili zimesamehewa na mchezo umekwisha mambo yanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme kwamba umefika wakati Wazanzibari kushirikiana pamoja kwa hali na mali kuona tunarejesha mila, silka na tamaduni zetu. Kuna mambo mbali mbali ya *Tuition*, ni kweli watoto wanahitaji kusoma, lakini tujiulize wale waliosoma zamani tunao wataalamu wakubwa kina Bi Fatma hawakusoma hao, hakukuwa na *Tuition* wakati huo, kwa nini wamekuwa watendaji wazuri? Tamaduni zilikuwa zinawalinda na kuwasimamia leo hatuna hilo, *Tuition* mwanamke na mwanamme wanakaa pamoja, Mwenyezi Mungu kasema *pair* mbili zikikaa pamoja, hapo shetani anatokea na mambo yanakuwa, ndivyo ilivyo na kitabu cha Mwenyezi Mungu ndivyo kilivyosema. Leo vijana wetu wako huru, *open* hakuna kuuliza, utamaduni na mila za Mzanzibari hazisemi hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi enzi hizo mtoto kabla hajaolewa hajawa mtu mzima, leo watoto ndio wanaoamua kufanya *kitchen party*, ndio wanaoongoza hizo harusi za wazee wao, ndio tamaduni za Zanzibar hizo? Nasema hivi kwamba tushirikiane ili tuone hii hali inayoendelea sio nzuri, ubakaji huu hasa wamekuwa watoto wa kike, lakini hata wale watoto wa kiume, jamani udhalilishaji ule, jambo limekuwa linasikitisha mno.

Mhe. Mwenyekiti, vijana hawa tunawategemea, *Al-rijjalu-Kawwamuna Alan-nisai*, waje wasimame kuliongoza Taifa hili wakati huo wamekuwa wote ni watoto wa upande wa pili, itakuwaje jamani. Mhe. Mohammed Haji Khalid kasema iko siku Zanzibar wataibuka waseme na wao wana haki zao za msingi watengenezewa sheria iletwe humu, ni hatari sana. Niiombe sana serikali, lakini na jamii tushirikiane tuone tunarejesha yale mambo na tamaduni zetu ambazo tulikuwanazo tangu zamani.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ya Ustawi wa Jamii imesema kwamba imeendelea na kutoa misaada ya kijamii kwa watu wasiojiweza wanaoishi katika mazingira magumu. Hali hii ya kutoa na misaada yenyewe imetajwa kabisa kwamba ni ya kifedha, ukimpa fedha mtu ambaye ana mazingira magumu hajala atakula huyo, atakwenda kununua chakula kwa sababu kula ndio haki ya kwanza kabisa ya msingi ya mwanadamu, madhali anaishi lazima ale, ukimpa fedha mama ambaye anaishi na mazingira magumu hamsomeshi mtoto atakwenda kupima sembe pamoja na ubwabwa azitumie basi, *Alhamdulillah, minalfaidhina*.

Mhe. Mwenyekiti, tujenge basi utaratibu maalum wa kuona hizi familia zinazoishi katika hali hizi zinawezeshwa miradi endelevu ambayo itaweza kuwazalishia na kuona wanaendelea kumudu shughuli zao za kiuchumi, pia za kusomesha watoto wao pamoja na kukidhi mahitaji yao. Hapa utakuwa umemsaidia, mtu akiwa na shida ya samaki ukimgaia samaki tu, basi utampa atakula siku ile, maana ndio shida yake, lakini ukimpa mshipi, chambo na ndoana unamwambia vua samaki na hata kutegemea wewe tena, badala yake yeye atakuwa na uwezo mzuri wa kuweza kuvua samaki, pengine na yeye aweze kumhamasisha mwenzake na kumsaidia mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe serikali wakitoa misaada ya kifedha mkononi haitoshi na wala hawa wenye mazingira magumu hawatafanyia hicho mnachofikiria nyinyi na ndivyo ilivyo. Ilivyo ni kwamba shida yao ya kwanza ni mlo unahitajika mara tatu, kwa haki za msingi za binadamu umpe fedha umwambie yeye azalishe, si kweli Mhe. Waziri, watafute utaratibu ambao unawezekana kuwaanzishia miradi ambayo itakuwa endelevu, iliyofanyiwa tafiti za kimaendeleo ili iweze kuendelea, maana yake ikue hiyo miradi, iweze kuwazalishia mahitaji yao na kuwawekea hakiba hatimaye na wao kuibuka katika maisha yanayostahiki kuishi yoyote yule katika misingi ya haki za mwanadamu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Vijana, nimeona kwamba linasemewa mno kabisa shamba la *Rossela* la Tunguu kwa muda mrefu. Na mimi ni mmoja katika Wajumbe ambao kwa miaka iliyopita nilikuwa katika Kamati ya Ustawi wa Jamii nilikwenda kuliona shamba. Kwa hivyo, kama hivyo ilivyoelezwa ndivyo wamefaidika wanataka sasa kuja kuigwa, wanataka uwe ni mfano. Nimesikia hapa imesomwa mpaka kwenye maelezo ya hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba Mhe. Waziri, anisaidie tathmini yao baada ya kufanya vijana hawa wanafaidika kiasi gani kukidhi maisha yao mmoja mmoja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwa ushirika watakuwa ni hivyo na kitakuwa vile vile kipo kwenye ushirika, kimmoja mmoja wanaishi vipi kutoka hapo walipoanzisha hadi hivi leo tulipofikia katika shamba hili ili tutakapokuja sisi wengine kutoka Kaskazini 'B' na Kaskazini yote huko tuone wenzetu hawa walifanya hivi, wamefanikiwa hivi na kwa mtu mmoja, basi kwa kuwa tunataka kuiga ana uwezo wa kupata kiasi hiki na anakidhi maisha yake kiasi hiki ili na sisi tuje tujifunze Tunguu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na hali hii, niseme kwamba Mhe. Waziri amekabidhiwa vijana, kuna Taasisi ya Utalii kwa wote dhana ambayo inamgusa waziri huyo, lakini nilisema mwanzo kwamba anagusana na wizara tofauti. Nataka aniambie ana mpango gani au mashirikiano gani baina yake na waziri huyu akiwemo Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Waziri wa Katiba na Sheria, nayasema hayo kwa msingi mkuu ufuatao:

Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ana uwezo wa kufungua viwanda mbali mbali na akaweza kupata ajira kwa vijana wake, lakini je, wana mahusiano gani ya kuona kwamba wanaweza kuwajengea jambo ambalo litaweza kutoa ajira kwa vijana hao, lakini na utalii nao unaendelea wanaoajiriwa huwa sio wale unaowafikiria wewe, kuna utaratibu gani wa kulisimamia hilo?

Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Katiba na Sheria kuna ucheleweshwaji mno wa vyeti vya kuzaliwa vya watoto, yeye ndiye anayehusika na hizo haki zao zinaanzia hapo maana malezi unayo wewe. Hebu atwambie huyu waziri akiwachelewesha haoni kwamba watoto wanakosa haki zao, kwamba akizaliwa tu hakusajiliwa akapewa cheti chake cha kuzaliwa, ndio mwanzo unamnyima haki yake ya msingi. Pia, nimuulize kuna vijana wengi mno ambao hawana vitambulisho na ambao ni Wazanzibari, vijana hawa hupata nafasi za ajira, lakini mara nyengine wanatakiwa vitambulisho vya Uzanzibari hawana na yeye ndiye anayehusika na hili.

Mhe. Mwenyekiti, akija aje anijibu atawasaidia vipi vijana hawa ili kuona na wao wanafanikiwa kupata haki yao ya msingi katika Taifa lao wakaweza kushiriki katika mambo mbali mbali, yakiwemo ajira na mengine ya kimaendeleo katika Taifa lao hili, lakini pia, kujikomboa na wao kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika tano ya ziada.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, namalizia. Nimeona kwamba kuna Idara ya Mikopo imetolewa, imetolewa mikopo 550, 328 kwa Unguja na 202 imetolewa kwa Pemba kupitia Mfuko wa kujitegemea.

Mhe. Mwenyekiti, ningependa labda nielewe kwamba mikopo hii watu wake hawa waliopatiwa mikopo walipatiwa taaluma ya kuchukua mikopo hiyo, lakini pia walifanya *Study* gani kwao kuona kwamba wana uwezo wa kurejesha

fedha hizo na hiyo miradi ambayo wanaifanya ina uhakika na endelevu. Kwa wale ambao wanachukua fedha hizo za mikopo kuwawezesha wanayo masoko, ndio msingi. Wengi wao ni wanawake hawa, wanayo masoko ya kupeleka bidhaa zao? Kama hawana, ana utaratibu gani wa kuona kwamba fedha hizo kiuwezeshaji, lakini pia, anawatafutia soko ili waweze kukidhi hicho ambacho serikali ndio nia yake kuwawezesha wananchi hao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije hapa kwenye ushirika. Idara ya Ushirika ilianza kwa miaka mingi nyuma na kwa kweli kila wakati huwa inakuja tu hivi ushirika, ushirika, nimeona humu katika kitabu, waziri kasema amekagua, ukaguzi wa ushirika huu ni wa uhakika, unafanywa kweli ukaguzi huu wa hizi shirika? Kwa sababu tumegundua kuona kwamba mara nyingi viongozi wa juu wa ule ushirika ndio wanaonufaika na shirika hizo, lakini wale wanachama wa ushirika huishia vikao tu na si vitu vyengine, kunataka kupitishwa mapato, kunataka kufanywaje, tuidhinishe, tuingiziwe, wale viongozi wa juu, ndio hufaidika na shirika hizo na wale wanachama wengine wakabaki kwenda kwenye vikao vya kupitisha tu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri, amefanya tafiti na kuona kwamba hao wanachama wa ushirika huu wanafaidika na hizo shirika zao? Lakini pia, ukaguzi yakinifu unafanyika kweli? Je, hiyo mitaji ni endelevu kweli wamewahi kuona hilo? Je, hao washirika jamani wana mbinu za ubunifu hasa, maana watu wakiwa si wabunifu huwezi kufikia, yeye ametoa taaluma gani Mhe. Waziri, kuwa shirika hizo kuona kwamba wamekuwa wabunifu watu wetu kuweza kumudu zile fedha au ule ushirika wao na kuona kwamba wanaweza kuuendeleza na kuleta tija kwao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, nataka ufafanuzi kidogo na kwa kuwa wizara hii imebebeshwa mzigo mkubwa kama nilivyotangulia kusema mwanzo, kwa sababu vitu vyote wamepewa wao, anambie Mhe. Waziri, je, hawa wazee wanaobakia mitaani wote ni wa kwake yeye? Bado wanapatiwa ile shilingi 5,000 tu? Kama wanapatiwa hiyo inaweza ikakidhi kweli haja na ugumu wa maisha tulionao sasa? Ningependa hilo nalo Mhe. Waziri, atakapokuja hapa unipatie, lakini kama ndivyo inatoka tano kwa maisha ya leo tuliyonayo ni kudanganyana, hiyo ni pesa ya skuli ya mtoto wa kawaida.

Mhe. Mwenyekiti, ndio ukweli hawataweza kumudu, hesabu kilo moja ya mchele, hesabu maisha yake mpaka ufike mwisho uone hiyo hali ilivyo. Kwa hiyo, ningeomba sana Mhe. Waziri kwenda kuomba huko. Mkikutana Baraza la Mapinduzi wafikirieni sana, hao ndio wazee waliosimamia Taifa hili hadi tukafikia leo kuwepo sisi hapa. Ni vyema mkawaangalia tunahuzunika mno, tusipende wale watakaokusanywa ukawalea wewe tu, lakini na hawa waliopo huko nje bado ni wazee wetu na serikali ina haki ya kuwatunza wazee hawa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, tena kwa mara nyengine ya pili, nasema kwamba nitaunga mkono hoja sikusudii kuweka pingamizi ya aina yoyote katika hotuba hii, lakini naomba nipate ufafanuzi nitaunga mkono kwa asilimia 92 na 8 zangu ninabakisha mpaka hapo ambapo kidogo nitapata ufafanuzi. Ahsante.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia na mimi uzima na afya njema nikaweza kusimama hapa na kutoa mchango wangu mfupi sana katika Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, lakini kwanza nataka nichukue fursa hii kukupongeza na wewe pia Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii. Jengine nimpongeze Mhe. Waziri, nisiwe mwizi wa fadhila kwa kukosa kumpongeza yeye na watendaji wake kwa juhudi kubwa wanazozichukua katika kutuletea ufanisi kwa watoto wetu tukiwemo sisi wanawake na vijana, ni jukumu kubwa kwa kusema kweli. Kwa hiyo, haitakuwa jambo jema kutokuwapongeza kwa kazi yao kubwa hii wanayoifanya pamoja na watendaji wake.Pia, niwapongeze Kamati na wao kwa kumpa mashirikiano Mhe. Waziri, ili katika kufanikisha suala lake hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwanza nataka nianze mchango wangu katika ukurasa wa 30 Idara ya Ushirika.Idara ya Ushirika katika ripoti ya Kamati pia wameeleza suala moja kuwa na jengo la Idara hii ni bovu. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, alisema kuwa wana mpango wa kuwapatia jengo Migombani, lakini hilo pia lilizungumzwa kwenye kipindi cha nyuma katika maagizo ya Kamati. Sasa Mhe. Waziri, aje atwambie hilo jengo limefikia wapi kwa sababu tunasikia hilo jengo nalo ni bovu zaidi kushinda maelezo na ni gharama kubwa ambazo zitafanikisha kupatikana kwa jengo hilo mpaka litakapofanikiwa. Kwa hiyo, Mhe. Waziri, aje atueleze hatua gani wamefikia kwa sababu ni agizo la Kamati tangu mwaka 2013 na mpaka leo hii bado linaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, jengine niende katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Waziri, ametueleza katika kitabu chake kuwa wamekusanya taarifa za udhalilishaji wa watoto na chini huku ametoa malalamiko ambayo yameripotiwa ya udhalilishaji wa watoto. Sasa hii mimi kwanza kwa sababu Wizara yake na kupitia Wizara ya Katiba na Sheria kwa

masuala haya watakuwa wana mahusiano makubwa. Kwa hiyo, takwimu tulizozipata juzi katika kitabu cha Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria na takwimu anazotupa Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto naona zina tofauti kidogo. Kwa hiyo, nataka Mhe. Waziri aje atwambie je, wana mashirikiano gani kwa Wizara yake na hii Wizara ya Katiba na Sheria. Hivi tunapotoa hizi takwimu, basi ziwe zote zinaenda sambamba, lakini isiwe Wizara hii anatwambia kesi za udhalilishaji ni 10 na akija Wizara hii anatwambia kuwa kesi za udhalilishaji ni 20. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri hili aje atupe ufafanuzi kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wamechangia wengi katika suala hili la kubakwa kwa watoto au udhalilishaji huu unaoendelea. Watu kwa masikitiko makubwa na sote tunasikitika, lakini juzi nilipochangia hapa, nilisema katika Wizara ya Katiba na Sheria kuwa kama tunataka tufanikishe hili, basi lazima tushirikiane kwa sababu sisi tunawawakilisha wananchi wetu humu. Tusiwawakilishe humu kwa maneno tu, tuwawakilishe kwa kufuatilia yale matokeo yanayotokea kule nje ili tujue kama ni kweli hili suala linatukasirisha kiasi fulani. Kwa hiyo, kusema hapa au kumtaka Mhe. waziri tukasema kuwa hana ufuatiliaji mzuri au kwa nini matokeo ya kesi kama hizi hakuna hukumu, itakuwa hili bado hatujasaidia serikali au hatujazisaidia Wizara husika.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kumezungumzwa kuwa mavazi nayo yanachangia. Sasa mimi nataka niseme kuwa tofauti kwanza juu ya suala la kubakwa na kuna tofauti ya masuala mengine kama ya kubebeshwa mimba na nini. Sasa unaposema kuwa pengine yanachangia mavazi, hebu tuangalieni mtoto wa miaka mitatu anavaa mavazi gani ya kuweza kumvutia mtu mpaka akenda akamfanya kitendo kibaya. Huyu mtoto wa miaka mitatu ana mavazi gani anayovaa ya kumvutia mtu. Mimi nasema hili ni tatizo tu Mwenyezi Mungu ameshatujaalia. Kwa hiyo, lazima tuyafuatilie masuala haya na kukomesha vitendo hivi vya udhalilishaji wa kijinsia wa watoto hasa waliokuwa katika umri wa chini ya miaka 18, kwa sababu mtoto wa miaka mitatu hana uwezo wa kujipamba, hana uwezo wa kuvaa vizuri, hana uwezo wa kufanya chochote.

Mhe. Mwenyekiti, sasa yote yanatokea haya watoto wa miaka mitatu, minne wanafanyiwa vitendo hivi. Kwa hiyo, tukisema ni kwa mavazi hao wanavaa wanaofika umri wa miaka 18 basi, lakini hawa watoto waliopo chini ya umri wa miaka 18 ndio wa kuwasikitikia, yule anayekwenda kutafuta mwenyewe atajua tena huko mbele kama ataolewa au vipi. Kwa hiyo, ili tufanikishe hili namuomba Mhe. Waziri, hizo Kamati unazoziunda katika Wilaya au Shehia washirikishe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ili watusaidie. Kwa sababu tutakaposhirikiana, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi watakapofuatilia masuala haya ndipo tutakapojua ukorofi uko wapi? Kama ukorofi upo Kituo cha Polisi au Mahakamani au kwetu sisi jamii, basi tutajuana.

Mhe. Mwenyekiti, jengine Idara ya Maendeleo ya Vijana Mhe. Waziri, katika kitabu chake amesema hapa kwamba kuendeleza na kuimarisha miundombinu ya uzalishaji wa mazao ya kilimo cha *Rossela* na mboga mboga kwa vijana wa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa aliyetangulia kwamba kikundi hichi cha Tunguu tayari kimeshapata utaalam wa kutosha sana. Kwa hiyo, kupitia Wizara yako naomba sasa kufanya wilaya nyengine ili na wao wapate taaluma hii. Tusibakie siku zote tunakuja hapa kuelezea Tunguu wamesaidia kitu kadhaa. Kwa hiyo, tunaomba na wilaya nyengine zihamasishwe ili waweze kufanikisha suala hili na wao katika kujipatia maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto katika *paragraph* ya 61, hapa kasema katika kuratibu na kusimamia haki za wanawake na watoto katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji na watoto imeanzisha Kamati hiyo inajumuisha Wawakilishi 30 kutoka katika Taasisi za Serikali na zisizo za ki-Serikali.
Mhe. Mwenyekiti, sasa ukisema Taasisi zisizo za ki-Serikali na nakumbuka mwaka jana tulidai hapa tukasema kuwa watu kama Polisi washirikishwe katika vikundi hivi kwa sababu na wao ni wadau wa masuala haya. Naomba Mhe. Waziri, akija kujumuisha anieleze kuwa hawa watu 30 kutoka Taasisi za Serikali na zisizo za serikali ambazo za kijamii, uje utueleze ni taasisi gani na gani inayowashirikisha, lakini pia, nakuomba tena haya yote unayoyafanya Wawakilishi wa Majimbo wapo pia na wao unatakiwa uwe nao katika kusimamia suala hili la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine kuna kiambatanisho hapa Nam. 2 ajira mpya, uhamisho, waliofariki dunia na kadhalika, lakini chini hapa ameandika kuwa kuna walioacha kazi. Sasa walioacha kazi niliona hapa kuwa ni wanawake wawili jumla yao. Hebu aje atueleze Mhe. Waziri, wanawake hawa walioacha kazi ni kwa sababu ya ugonjwa, kufukuzwa au kwa masuala gani, ili tupate kujua.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala jengine katika viambatanisho vyake hivi wanasema kuna mradi uliopatiwa katika mbio zile za mwenge. Mmoja wamesema kuwa kuna mradi wa kilimo cha mahindi uliopo pale Mziwanda. Naomba Mhe. Waziri, aje anipe ufafanuzi pale Mziwanda kile ni kikundi, ni mradi wa kitu gani. Kwa sababu tunavyofahamu lile ni shamba walinyang'anywa watu kwa kuonewa tu kwa kusema kweli wala hakuna kilichofanywa. Sasa wamepewa watu pale ambao si wa eneo lile ambapo shamba lile lilikuwa lina watu wanaolima katika eneo lile, tena watu maskini. Hawa maskini wanaotajwa wa kipato cha chini, ndio waliokuwepo pale wanalima. Leo tunapiga kelele shamba lile amepewa mtu limetiwa uzio, wanaofaidika sasa hivi sidhani mimi kama ni wananchi wa eneo lile pale. Kwa sababu ingelikuwa huu mradi unafaidisha wale wananchi waliopo pale, basi njoo utueleze nani wenye mradi ule na wanaolima pale ni nani?

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nilikuwa sina mchango mkubwa sana, bila ya kupoteza muda wako kwanza mimi naunga mkono bajeti hii asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.
Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa vile muda umebakia mchache sana. Kwa hiyo, tuahirishe Baraza hili hadi saa kumi na moja jioni. Naomba kuahirisha.

(Saa 6:55 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 jioni Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla hatujamkaribisha Mhe. Kazija Khamis Kona kuendelea na majadiliano yetu, tuna wageni kwa jioni yetu ya leo ambao wamekuja kututembelea.Wageni hao inaonekana kwa namna moja au nyengine wameguswa sana na bajeti ambayo inaendelea ndani ya taasisi yetu.

Wageni hao ni wanafunzi kutoka kozi ya *social work* kutoka Chuo cha Utawala wa Umma Tunguu. Jumla yao ni wanafunzi 30. Naomba wasimame ili waonekane.(*Makofi*)

Ahsanteni sana, kaeni.

Sasa tunaendelea tunamkaribisha Mhe. Kazija Khamis Kona.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi jioni leo hii ya kuchangia ya wizara ya Mhe. Waziri wa Uwezeshaji na Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara kwa kazi wanayoifanya na kutekeleza majukumu yao ipasavyo wanayojipangia. Kitabu cha Mhe. Waziri, ukurasa wa 44 kinaelezea kwa mujibu wa taarifa alizozipata kutoka Mahakama mbali mbali, katika kitabu chake jumla ya kesi 85 za udhalilishaji amezipata katika Mahakama zetu mbali mbali. Kati ya kesi hizo kuna nyengine za ubakaji, kulawitiwa watoto na nyenginezo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka Mhe. Waziri, anifafanulie katika hizi kesi mbili ambazo watoto wale walioapiwa ambazo zimeruhusiwa, anifafanulie vipi kesi hizi zimeruhusiwa anifafanulie vipi kesi hizi zimeruhusiwa. Kesi yenyewe ukiziangalia ni ngumu mno, kesi za kulawitiwa. Kwa kweli ni hatari kubwa sana. Watu kama hawa wanaowalawiti watoto huwa wanakataliwa hata Mwenyezi Mungu anawachukia sana watu kama hawa. Sasa leo wizara inatupa taarifa kwamba kesi hizi zimeruhusiwa kwa makubaliano yepi. Mhe.Waziri, aje anifafanue hizi kesi mbili.(*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, halafu pia na kesi nyengine za Pemba pia, hivyo hivyo nazo zimetolewa hukumu. Sasa ninataka Mhe. Waziri hapa hapa aje aniambie, hizi za Pemba hukumu ya aina gani iliyotolewa katika watu hawa. Kwa sababu watu hawa hata sijui sisi tuwafanye nini, wakati Mwenyezi Mungu yeye mwenyewe anawachukia watu hawa, sisi ndio kwanza tunawaruhusu wakaendeleze kwa watoto wengine waendelee na masuala haya. Serikali hapa mimi ninadhani bado haijawa na umuhimu wa kuwashughulikia hawa watoto wanaobakwa, kwa sababu kama inaona umuhimu isingetoa ruhusa kiholela.Hukumu wasizihukumu kama hivi, lazima hukumu iendane na kosa lenyewe lilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo, ninaelekea Idara ya Ushirika, ilipokuwa Idara hii ya Ushirika tunaifanyia kazi sisi katika Kamati ya Habari, Uwezeshaji na Mifugo kwenye lile jengo lao tulikuwa tukilitembelea tukaona jengo

halifai. Jengo lipo hatarini. Sasa sijui Mhe. Waziri, amejipanga vipi ili kulitatua tatizo hili ili wafanyakazi hawa wa Idara hii wafanye kazi zao ipasavyo na wakiwa katika hali ya usalama kuondokana na wasi wasi na jengo lile jinsi lilivyo, halafu jengine ni kuhusu Idara ya Mikopo. Idara ya Mikopo inatoa mikopo, lakini mikopo huwa ina riba kubwa. Baadhi ya wananchi wetu wengine hii mikopo iliyokuwa na riba hawaitaki kabisa kabisa, kwa sababu kutokana na dini yao na itikadi ya dini yao ilivyo hasa, wenyewe wanasema riba ndogo ni sawa sawa na kuzini na mama yake mzazi au baba yake. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa Mhe. Waziri, kwa kuwa wananchi wetu wanahofu hii na hii riba. Sasa wananchi kama hawa kuwawezesha kiuchumi na kutaka kujiendeleza kimaisha, ikiwa hawaitaki hii riba na dini yao inakataza. Je, Mhe. Waziri, utawasaidia vipi wananchi hawa ili kujikwamua na umaskini na kukosa lile pato la riba wanalolikataa.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee tena kutokana na hizi ajira kwa vijana, ajira kwa vijana hapa, vijana wetu ukiwaangalia wengi hawana ajira. Mhe. Waziri, wizara yake inahusu sana na vijana pia na kuwawezesha vijana. Sasa Mhe. Waziri, aje aniambie vijana wangapi wa Zanzibar aliowawezesha ili kujikwamua na umaskini waliokuwa nao.

Mhe. Mwenyekiti, halafu hapa kitabu chake kinatuelezea kwamba shamba la Tunguu la mauwa hili. Hebu Mhe. Waziri, ukija njoo uniambie kikundi hichi cha shamba la mauwa, kina vijana wangapi na wanatoka maeneo gani? Kwa sababu shamba hili limekuwa kama mfano na kila mwaka linafiwa shamba hili. Umewasaidia nini, hata wamefika malengo ya kwamba mambo yao yamekuwa mazuri kiasi. Hebu Mhe. Waziri, njoo unielezee hili shamba lina vijana wangapi na wanatoka maeneo gani?

Mhe. Mwenyekiti, halafu kwa kuwa ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, inaonekana hapo sijui ipo simu iko wazi, inawaumiza wale watu wa mitambo ndani.

Mhe. Kazija Khamis Kona: Sina simu mimi.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa sijui ni pahala gani pana mawasiliano haya. Hebu tujitahidi kurekebisha haya matatizo. Tuendelee.

Mhe. Kazina Khamis Kona: Mhe. Mwenyekiti, simu yangu mimi nimeizima kabisa, sijui labda ni mitambo yenyewe tu hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, haya mashamba kama haya ya mfano tunamuomba Mhe. Waziri, atuwekee kwa kila wilaya tuwe na mashamba ya vijana, ili tuwapime vijana wetu jinsi ya mwenendo wao wa kujiajiri.

Mhe. Mwenyekiti, pia, niende katika watu wenye mazingira magumu. Hapa alisema pana familia 75 Unguja, 55 Pemba zimepatiwa misaada ya fedha za kujikimu. Hebu Mhe. Waziri, njoo utufafanulie fedha hizo, ni kiasi gani walizopewa ili kwa kujikimu kwa kuendesha maisha yao pamoja na watoto wao.

Mhe. Mwenyekiti, halafu pia, watu kama hawa tusiwape fedha kwa sababu mtu umeshamwambia huyu ana maisha magumu, leo unampa hizi pesa, yeye ataona asubuhi ikifika ananunua boflo, mchana ukifika anapika hichi hichi. Isipokuwa tuwafungulie miradi ili miradi yao iwe endelevu kwa kujikwamua wao pamoja na watoto wao na Taifa lao kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, watu wenye mazingira magumu serikali iwaone sana na iwaangalie sana na iwasaidie kwa hali na mali zote, kwa sababu mtu akishalipwa ana mazingira magumu. Huyo kwa lugha nyengine tunaita ameshakuwa fukara tena huyo. Sasa hapa serikali iangalie kwa umakini kwa kuwasaidia kwa vyovyote vile, kwa sababu elimu watoto wao wapate kuwasomesha na wao wenyewe wapate kujikimu katika maisha yao. Kwa hivyo, Mhe. Waziri, hapa wizara yako ichukue juhudi kubwa sana ili watu wetu hawa nao waondokane mazingira kama hayo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu pia, Mhe. Waziri kuna hizi ajira za watoto. Ajira hizi za watoto, wizara yako sijui inashughulikia vipi kutatua hizi ajira za watoto wadogo. Kwa sababu ukiangalia watoto wengi huwa wanajihusisha na ajira ndogo ndogo hususan mwambao wa pwani, wanajihusisha na kupara samaki, kama sehemu za utalii utawakuta watoto wanaranda wamechukua vidude vyao wanauza uza. Sasa Mhe. Waziri, sijui hili utanaliangalia

vipi katika wizara yako na nikushauri hasa katika maeneo haya upange uende kuangalia hasa uwatizame jinsi watoto wanavyojihusisha na ajira hizi ndogo ndogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nimuombe Mhe. Waziri wetu, Mhe. Mgeni Hassan Juma hapa alikuja na hoja binafsi, hoja ile ninataka kumuuliza Mhe. Waziri, wameifanyia kazi vipi? Kwa sababu tumetoa maazimio humu na tukapendekeza sisi. Sasa sijui Mhe. Waziri, ameifanyia kazi vipi hoja yetu ile na kuitekeleza.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, sasa tutamkaribisha Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, wakati tunawasubiri na wale ambao tulikuwa tumewataja mwanzo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ingawaje ndio ninaingia ninajitayarisha, lakini pia, si vibaya, nitamuomba Mwenyezi Mungu nitakayokuwa nayo nitayazungumza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi nimpongeze Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake wote kwa kutuletea hotuba hii mbele yetu na tukaweza kuichangia. Mimi nianze na ukurasa wa 55 unaosema, "Idara ya Maendeleo ya Wanawake na Watoto". Nikija katika Idara hii, niseme kwamba kuna kifungu hichi cha 3, kinachosema;

"kuimarisha, kuratibu shughuli za kiuchumi maendeleo ya wanawake na watoto".

Mhe. Mwenyekiti, nimuulize Mhe. Waziri, ni maeneo mangapi na yepi ambayo ameyaimarisha na faida gani waliyoipata katika maeneo hayo katika kuimarisha maendeleo hayo? Lakini pia, katika kifungu cha 4 kinachosema kwamba;

"kuimarisha mashirikiano ya Kimataifa, kikanda, Kimataifa kwa mambo yanayohusu wanawake na watoto".

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, nimuulize Mhe. Waziri, ni nchi ngapi ambazo mumeshirikiana katika kuimarisha hayo mashirikiano na faida gani mumepata. Naomba Mhe. Waziri, atakapokuja hapa anieleze, lakini vile vile, nije katika ukurasa wa 42 unaosema kwamba; "Idara ya Ustawi wa Jamii".

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii kwanza niende katika kitabu kikongwe anachosema kwamba Idara ya Ustawi wa Jamii. Hapa walisema kwamba kuimarisha huduma za ustawi kwa wazee, lakini vile vile, kuratibu na kuthamini masuala ya makuzi ya awali kwa mtoto na vile vile kusimamia masuala ya fidia kwa wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kitabu hichi chengine kilichokuja mara hii, kinasema hivyo hivyo. Nimuulize Mhe. Waziri mwaka 2012/2013, haya yote waliyoyaandika hapa hayakuwahi kutekelezwa. Akija hapa anieleze kwa nini hayakuwahi kutekelezwa, hata kitabu hichi chengine kinachokuja mwaka 2013/2014 kinajirudia yale yale, lakini pia, niseme kwamba katika Idara hii, kwenye kifungu cha 4 kinasema kwamba; "Kusimamia ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali kazini". Nimwambie Mhe. Waziri, moja kati ya ajali kazini, kwanza pia na wapo watu wetu ambao ni wachumaji wa karafuu na hao nao tutasema nao wapo katika ajali kazini, wakiwemo vijana wetu pamoja na wazee. Hapa nimwambie Mhe.Waziri, wizara yako inasimamia vipi katika kupata haki zao wakiwemo wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha kuimarisha hifadhi ya wazee.Niseme kwanza tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa wazee wetu waliopo Sebleni kwa kutengenezewa nyumba zao vizuri sana. Hii tunamshukuru Mwenyezi Mungu na tunaishukuru pia wizara tunaipongeza, lakini vile vile, niseme kwamba wapo wazee wetu ambao wapo waliopo Pemba katika nyumba za wazee zile.

Mhe. Mwenyekiti, wazee hawa nyumba zao ni mbovu ambazo hazina thamani ya uzee kukaa. Tukiangalia hasa hawa ni wazee wetu ambao ni wazazi wetu, lakini tukiwaangalia bado hatuwafanyii lilekuwa la haki, kwa sababu mzee ni mzee na sisi tukiangalia tupo nyuma yao tunakuja.

Mhe. Mwenyekiti, leo Mhe. Waziri, ikiwa yeye wazee wale na wao pia hawakutendea haki hiyo, tutambue kwamba na sisi tunakuja huko huko, tutakuja kufanyiwa na watoto wetu kama hivyo. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri,

aliangalie sana suala hili la wazee Makondeni Pemba, kwamba nako kunahitaji wazee wale kujengewa nyumba na kuhifadhiwa, lakini licha ya hilo, kuna pia wazee hawa fidia yao ni kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, shilingi elfu kumi ni tatizo. Ikiwa ni kilo mbili za mchele, nusu kilo ya sukari hapati chengine. Kwa hivyo, na hili tuliangalie hasa tukiangalia na nchi za wenzetu, wazee wanavyotunzwa na sisi wazee wetu tuwatunzeni. Nimuomba Mhe. Waziri, hili aliangalie sana atakapokuja ili na kuwafanyia haki wazee wale walioko Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 48, "Idara ya Maendeleo ya Vijana". Bado vijana wetu hawana ajira na tukisema hawana ajira ni tatizo kubwa sana, tena ni tatizo ambalo la mtihani mkubwa sana, ndio utakutia vijana wetu hivi sasa wapo vijiweni wanavuta bangi, wanavuta unga. Vijana hawa tukiwaangalia tatizo la ajira ni sugu, lakini vile vile, tuseme kwamba hii ajira ikiwa watoto tutawafanyia ajira hamna, ndio sababu zinazowaletea kuvuta unga.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana tatizo la vijana kuwapatia ajira. Hii ajira pia asiangalie vijana tu, tukisema kwamba vijana tunawaachia kuwa hawana ajira, wanavuta bangi, unga na hatimaye tutakuwa na Taifa ambalo la watu waliokuwa walevi tu, kwa sababu ni wengi vijana hivi sasa wapo vibarazani, hawana kazi, hawana chochote kazi yao kuvuta unga akipita mtu pale kumyang'anya basi. Hili ndio tatizo la vijana wetu sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, namuomba Mhe. Waziri, aliangalie sana suala la watoto wetu kupata ajira. Pia, sitoacha kusema kwamba ni waziri tu, hasa tuangalie na serikali kuu Mhe. Balozi Seif Iddi hayupo, lakini hili aliangalie sana Mhe. Balozi Seif Iddi kwa sababu ikiwa watoto tutawaachia hivi na serikali haitosimama kidete kutengeneza ajira. Kuna mengi, kuna viwanda hapa vikiwekwa watoto wetu watapata ajira, kuna mengine yatakayofanywa watoto wetu watapata ajira, lakini ikiwa ni serikali imekaa kimya na kuwaacha watoto wetu vibarazani wanavuta unga na bangi. Hii tutakuwa na athari kubwa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile, nije katika ukurasa wa 74 kifungu cha 4. Kifungu cha 74 nije katika utoaji wa mikopo kupitia mfuko wa kujitegemea. Katika kifungu cha 7 kinachosema Wilaya ya Mkoani kuna wanawake 11 na kuna wanaume 11, halafu jumla ni 22 na halafu kuna vikundi vitatu ambavyo vimepata mkopo huo shilingi milioni 18.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja anieleze hivi vikundi vitatu ni kutoka wapi. Pia Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 79 unaohusu kukashifu, kuna umri wa chini ya miaka 18, hawa ni watu 280 na halafu kuna zaidi ya miaka 18 ni watu 28, halafu kuna wanawake 418, halafu wanaume 0 jumla ni 726. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifafanulie hawa wanawake waliokashifiwa 280 ni kutoka wapi na wapi na halafu kuna wanawake 28 ni zaidi ya miaka 18, pia namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anifafanulie.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa wa 80 ambao unasema kutoka idadi ya kesi 43 za kubaka, wanawake 31 Chake Chake, Mkoani wanawake 4, Wete 4, Micheweni 4, watoto 43 wanawake, halafu kuna 43 na Mahakamanini 3. Namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anipe maelezo zaidi, ingawaje Mahakamani wako 3, lakini hasa waliochukuliwa hatua za kisheria za kufungwa sijui ni wangapi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa anieleze.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema kwamba sijajitayarisha, lakini kuna ukurasa wa 36 unaosema Idara ya Mikopo. Idara hii kutoa mikopo 1,000 kwa vikundi vya kiuchumi na watu binafsi, wajasiria mali mmoja mmoja yenye thamani ya shilingi milioni 300,000. Halafu Mhe. Mwenyekiti, ukija huku chini imetiwa mikopo 550, Unguja 328 na Pemba 222 kwa kupitia mfuko wa kujitegemea yenye thamani ya shilingi milioni 298.

Mhe. Mwenyekiti, nimuulize Mhe. Waziri kwamba katika mikopo hiyo waliotoa, sijui ni shehia ngapi na wilaya ngapi na katika Wilaya ya Mkoani kuna mikopo mingapi waliopata na vikundi vingapi vilivyopata mikopo hiyo, au ni watu gani na gani ambao wamepata mikopo hiyo. Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo naomba nikae kitako ahsante nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Sasa tunamkaribisha Mhe. Salim Abdalla Hamad na baadaye Mhe. Saleh Nassor Juma.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwa kupata nafasi ya kuchangia chochote katika Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, moja kwa moja nianze na programu ya jinsia Zanzibar, ambayo inaonekana katika kifungu cha 24, ukurasa wa 13 ambacho kinasomeka kama ifuatavyo:-

"programu hii inatekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu *UNFPA*"

Madhumuni ya programu hii ya jinsia Zanzibar, ni kusaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuzingatia masuala ya kijinsia, katika sera, mipango na bajeti pamoja na kuzijengea uwezo taasisi mbali mbali na wananchi katika kupambana na udhalilishaji wa kijinsia.

Pia nikikisoma kifungu cha 25 ili nichangie kwa pamoja katika ukurasa huu wa 13 kinasema kuwa, katika mwaka wa 2013/2014 wizara kwa kupitia programu hii imetekeleza yafuatayo. Kwanza imetayarisha muongozi kwa viongozi wa dini, yaani dini mbili kuu, dini ya Kiislamu na dini ya Kikristo kwa ajili ya kuwafundisha waumini wao, juu ya masuala ya kupinga udhalilishaji wa kijinsia. Miongozoi hii imeshafanyiwa majaribio na marekebisho na iko tayari kwa kutumika.Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia hapa.

Tukiangalia sisi hapa na mimi nazungumza kwa dini ya Kiislamu na dini yetu imeleta mfumo wa maisha kwa wanawake na wanaume na tukisema kuwa wizara imetayarisha miongozi kwa dini mbili kuu ya Kiislamu na dini ya Kikristo kwa ajili ya kuwafundisha waumini wao, juu ya masuala ya kupinga udhalilishaji wa kijinsia, mimi nafikiri kila kitu kinajulikana katika dini zetu.

Kwa hivyo, katika kutengeneza muongozo huu, naomba kujua hii wizara ilikuwa ikishauriana na Masheikh wakati mambo haya yapo katika dini, au kwa upande mwengine wa dini au alikaa tu kwa kufuata maelekezo ya ulimwengu wakafanya mambo ambayo mengine yanakwenda kinyume na dini. Mtu yeyote anayekwenda kinyume na dini ilivyoelekeza, huwa huyo amekufura na huenda akenda mahali pabaya.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika ukurasa wa 14, wizara hii hii inasema imefanya tathmini ya mapungufu yaliomo katika sheria ya usajili wa ndoa ya mwaka 1966, sura ya 91 na 92 ambayo tathmini hiyo iligundua kwamba sheria hii imejikita zaidi katika masuala ya usajili na haikugusia masuala muhimu yanayohusu ndoa, likiwemo suala la haki na wajibu wa wana ndoa na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyojua kuna kitabu maalum kinaitwa *Kitabu Nikah* na hiki kitabu kinahusiana na ndoa tu. Haki za mke kwa mume na haki za mume kwa mke na kuwa watu wanapoozeshwa kwa dini yetu ya Kiislamu, baadhi ya Masheikh husema, *Uzawijuka ala Amaraahu bihi min imsaakin bimaarufin Au tasrihin Biihsaan (Makofi)*

Yaani ukitaka kuozesha mtu kama alivyoamrisha Mwenyezi Mungu katika hii ndoa, na ni kukaa naye kwa wema na pia kama itabidi ambalo ni jambo Mwenyezi Mungu analichukia la talaka na kutengana, basi ni kutengana kwa wema. Hii kukaa naye kwa wema kuna maelezo marefu sana. Sasa ikiwa dini yetu imeshaweka namna ya mtu anavyotakiwa kukaa na mkewe na mke akae na mume wake, haya mengine yanatoka wapi mpaka ikabidi tubadilishiwe sheria na mambo haya yako kwenye Mahakama ya Kadhi. Tunavyojua serikali yetu pamoja na katiba yake ya nchi hayaingilii mambo ya dini ya mtu.

Kwa hivyo, naomba nipate maelekezo ni mapungufu gani yalioko katika dini ya Kiislamu, mpaka ikabidi wizara kuweka mambo haya na wakati tunaambiwa kuwa dini haina mapungufu yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije kwenye kifungu kinachoeleza programu ya kupunguza usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi. Hapa imeeleza kuwa programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano na Shirika la *UN Woman*, kwa lengo la kusaidia jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, hebu nisaidie kwa nini hapa kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii, isingewezekana bila ya kutia usawa wa kijinsia, kwa sababu Mwenyezi Mungu tayari ameshawaumba wanawake na ameshawaumba wanaume na kila mmoja kampa daraja yake. Sisi tukisema usawa wa kijinsi, tokea lini usawa baina ya mwanamke na mwanamme. Kwa hivyo, mimi naunga mkono hasa suala la kuwawezesha wanawake kiuchumi,

kisiasa, kijamii na mengi mengineyo, lakini hili suala la usawa wa kijinsia naona ni jambo ambalo halina ulazima wa kuingizwa katika kitabu hiki, kwa sababu haitatokea kuwa na usawa baina ya wanawake na wanaume, utaweka usawa huku lakini huku kwengine itakuwa sio sawa na Mwenyezi Mungu alivyoumba ndio hivyo hivyo na alipoteremsha katika maisha baina ya mwanamke na mwanamme ndio hivyo hivyo. Kwa hivyo, tuhadhari sana kuingilia dini za watu katika kupanga mambo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ninaloomba kueleza ni kwamba kuna huu umoja unaoitwa UVIKIUTA, ambao vijana wanahusika sana katika umoja huu, lakini pengine leo itakuwa ni mara ya tatu nataka nijuwe hasa UVIKIUTA maana yake ni nini, asili yake ni nini na inafanyakazi gani hapa Zanzibar, kwa sababu huambiwa eti ni umoja wa vijana. Nataka nielezwe hasa UVIKIUTA ni upi na unatusaidia nini kwa vijana wetu, isijekuwa kuna mambo ambayo kama tungeyajua mwanzo basi angalau tungetoa muongozo vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningeomba nilizungumze ni kuhusu Idara ya Mikopo na hii iko kwenye ukurasa wa 36 na kuendelea. Mhe. Mwenyekiti, idara hii ya mikopo kwa mujibu wa maelezo yake inashughulikia mikopo ya aina mbili, kuna fedha hii ya kujitegemea ambayo inatolewa kwa mikopo na kuna fedha ya AK na JK ambayo pia inatolewa kwa mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, tukifungua kwenye ukurasa wa 74, kiambatanishao nambari 4 ambacho kinaeleza kuhusu utoaji wa mikopo kupitia mfuko wa kujitegemea. Kuanzia Julai 2013 hadi Machi 2014. Mimi nitazungumza kwa ufupi, lakini nipate maeleze ya kina kuhusu namna mikopo hii inavyotolewa. Kwa sababu tukiangalia hiki kiambatanisho.

Kwa mfano, nambari moja ni Wilaya ya Mjini, hii ina jumla ya watu 58 waliokopeshwa ambao walifanya vikundi 7, na walikopeshwa jumla ya shilingi milioni 37,500,000. Lakini ukija katika Wilaya ya Kaskazini B, ina jumla ya watu 75 waliokopeshwa zaidi ya kule mjini na ina vikundi 13 badala ya 7, lakini imekopeshwa shilingi milioni 32 tu. Kwa nini kule kulikuwa kuna watu kidogo na vikundi kidogo wakakopeshwa pesa nyingi na huku kulikokuwa kuna watu wengi na vikundi mara mbili zaidi wakakopeshwa fedha kidogo.

Vile vile ukenda kwa upande wa Pemba, kuna kikundi hiki cha Chake Chake kinajumla ya watu 120 waliokopeshwa, ambao wamefanya vikundi 17, lakini wamelipwa shilingi milioni 25,500,000. Naomba kujua kwa nini kule pesa ikawa nyingi na hapa ikawa kidogo, utaratibu uliotumika ukoje. La kusikitisha kila siku sisi tunapiga malele hapa kwa Wilaya ya Micheweni ambayo ni wilaya iliyokuwa chini kabisa kiuchumi, kwa maana hiyo ilikuwa ifaidike zaidi. Ina vikundi 9, jumla ya wakopeshwaji 40 lakini imepewa shilingi milioni 20 tu, wilaya kama hii inayopigiwa malele. Kwa hivyo, hapa naomba nipate maelezo ni vigezo gani vilivyotumika na kwa nini ukopeshaji ukawa katika hali hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande mwengine nizungumzie fedha inayoitwa ya AK na JK. Fedha hii ilikuwa ikitumika kwa kukopeshwa, lakini ulipaji wake ulikuwa ni mzito sana kiasi ambacho ikakatishwa hasa, ikawa badala ya kukopeshwa sasa watu wanadai kupata fedha iliyokopeshwa ili irudi.

Mhe. Mwenyekiti, kama utaangalia humu basi utaona kuwa hii fedha imeshaanza kukopeshwa na watu wanadaiwa. Napenda kujua je, ukopeshaji huu ni ule ule wa zamani kuwa benki ni lazima itowe maamuzi kwa mtu anayekopeshwa au masuala yote yako kwenye wizara husika. Pia vipi hali ya urejeshwaji wa mikopo kutokana na hali ilivyokuwa hapo zamani.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo napenda nilizungumze ni kuhusu Idara ya Ustawi wa Jamii. Idara hii Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 42, kifungu cha 52(4) na vile vile imeelezwa katika ukurasa wa 48, kifungu cha 54(6) ni kuwa idara hii mambo iliyojipangia ni kutekeleza ni kusimamia ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali kazini.

Mhe. Mwenyekiti, kama alivyozungumza Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na mimi nazungumza hivyo hivyo. Mhe. Mwenyekiti, tunajua kwamba kuna watu wanapata ajali kubwa kazini, na huwa wanapitia katika njia zote ili waweze kupata haki zao, lakini sijui fedha inalipwa vipi. Kuna wenzetu walipata ajali tokea mwaka 2009 na mpaka hivi karibuni katika kufuatilia sijui kuanzia juzi na jana, lakini huko nyuma watu hawa walikuwa hawajalipwa na vielelezo tokea hospitali na ngazi zote zinazohusika, ili watu hawa waweze kulipwa wamekamilisha.

Mhe. Mwenyekiti, mmoja kati ya hao naomba kulitaja jina ili Mhe. Waziri kama hana kumbukumbu ajitayarishe kunieleza. Ni kijana mmoja, naomba radhi kwa sababu ni mwanamke sijui kama kaolewa au vipi, lakini anaitwa Asha Rubea Hafidh. Huyu ni mmoja katika watu waliopata ajali kazini na hivi sasa kama hajapata uhamisho basi yuko Mahakama ya Ardhi pale Wete, na mpaka hivi karibuni katika kufuatilia haki zake wakati njia zote keshapita na vielelezo vipo na nimeshavipeleka Wizarani bado hajalipwa.

Mhe. Mwenyekiti ningeliomba kujua kwa lile tamko la mwanzo la kifungu 52(4) cha ukurasa wa 42 kuwa malengo waliyojipangia Wizara hii ni kusimamia ulipaji wa fidia kwa wakaazi waliopata ajali kazini Je, kwa mwaka huu wa 2013/2014 waliwalipa wangapi na hawa waliowaekewa malengo katika mwaka 2014/2015 ambayo ni kifungu 54(6) ukurasa wa 48 waliobakia ni wangapi. Mpaka mwaka gani wamelipa na kuanzia mwaka gani bado hawajalipa, kwa hivyo na hilo Mheshimiwa naomba nipatiwe maelezo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ninaloomba kuzungumza ni kuwa tuna vijana na kijana ni kijana kijana ana matayarisho ya kujiendesha kimaisha, ana mahitaji ya lazima na kushughulikiwa, ujana ni jambo la lazima, lakini mimi niliposoma hiki kitabu uwezo mkubwa sana nimeona ni uhamasishaji wa kijinsia kwa upande wa kinamama, sipingi hilo lakini vijana wetu hawakupewa kipaumbele stahiki.

Wakati Mhe. Waziri anashughulikia pia vijana mimi zaidi ya haya mambo madogo madogo yaliyomo katika kitabu amewapangia vipi hasa vijana wetu kuweza kujiajiri wenyewe na kuajiriwa na waweze kuendelea na maisha yao ili baadae wasiwe vijana wapotofu, kwa sababu sote tunajua hakuna kitu kibaya kama shida na uwezo wa nchi yetu tunaujua ni mdogo sana kimapato. Vijana tukiwalegezea wanaingia katika mambo ambayo mwisho tunawalaumu, kwa hivyo ningeliomba kujua ni mpango gani mahususi hasa vijana wetu wamewekekewa ili waweze kujiendeshea maisha yao vilivyo.

Halafu jengine Mhe. Mwenyekiti, nililoona katika kitabu hiki ni kuwa Mhe. Waziri kasema kuwa atafanya utafiti ni kwa kiasi gani vijana wetu wameporomoka kimaadili kutokana na utalii tuliokuwa nao. Mimi Mhe. Mwenyekiti kwa hili ningeliomba kuzungumza kuwa tusiangalie utalii tu; utalii kwa upande wangu naona ni sehemu ndogo sana, lakini tuangalie Zanzibar ilivyokuwa mara baada ya Mapinduzi na Zanzibar ilivyo hivi sasa, Zanzibar ikitangaziwa kuwa nchi ya kiislam asilimia 99 kulikuwa watu wetu wakivaa kutokana na mila, silka na desturi zetu zilivyo, lugha zetu, mtizamo wetu ulikuwa humuoni mtu kwenda kinyume na maadili yetu na hata Mhe. Rais hapa wakati mmoja ilibidi achane suruali za watu kwa sababu ya kuwa wanavaa nguo za kubana.

Sasa tumesema Zanzibar ni njema atakae aje na nashukuru kuna watu wamekuja hapa kwa njia ya anga, baharini, na kadhalika wamejazana ambao sio Wazanzibari na kila mmoja anakwenda na desturi anayoitaka mwenyewe, tunasema haki za binaadamu huwezi kuwaingilia lakini inaporomoa maadili yetu, zinaporomoa utamaduni wetu, inaporomoa silka zetu na inatupeleka pabaya sana.

Mhe. Mwenyekiti, hapana asiyejua kwamba sasa Zanzibar imebadilika sio Zanzibar ya zamani ile ya sifa ya kuwa na waislam wengi kwa jina tu lakini kwa vitendo mtu akija ataona hali ilivyo sivyo inavyozungumzwa, tunanyamaza kimya tunaachia halafu tunakwenda kuingia utalii mimi kwanza ninaloomba hivi Mhe. Mwenyekiti, kama kweli tunataka Zanzibar iwe kama ilivyokuwa zamani nchi ya heshima, nchi inayoheshimika na kila anayejua ajue kuwa anaingia Zanzibar kwanza tuiangalie hali ilivyo na sababu kutokana na uhuru wetu wa kuachia yanayotokea yaende yalivyo, na kutokuweza kuyarekebisha nakuhakikishia huko kwenye utalii kutakuwa hakuna haja hata ya kuwagusa.

Mhe. Mwenyekiti, vyenginevyo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa wajumbe si lazima simu iwe yake hata kama jirani ana simu basi inari *-act* naomba tuangalie na tujitahidi ku-*control* simu zetu, tuendelee Mheshimiwa Salim.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Sasa Mhe. Mwenyekiti kama hatukuyatilia maanani haya tukaiwacha nchi hii watu wakaingia wanavyotaka, wakawa wanavaa wanavyotaka, wanafanya wanavyotaka na tunajua sivyo hata dini zetu zote zinakataza, halafu tena tukiingia kwenye utalii naona hatujafanya jambo. Mheshimiwa tujue kakabidhiwa vijana na vijana ni umri wa hatari sana na Zanzibar imebadilika aanze huko halafu ndio tuingie kwenye utalii.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kila vikundi watu wamekaa, wamejiajiri Mheshimiwa ndio mwenye fedha ya kukopesha hivi vikundi pamoja na watu binafsi, lakini jambo ambalo nasikitika, kwa sababu na mimi katika jimbo

langu kuna vikundi vingi sana nikiona kwamba Wizara bado haijatia mkazo wa kutembelea vile vikundi. Kuna vikundi watu wamepoteza nguvu zao nyingi sana hasa katika ufugaji wa samaki na mengineyo, wanataka waelekezwe wanavunjika moyo wanaharibikiwa.

Kwa hivyo namuomba kuanzia sasa rasmi kama kweli hii ni Wizara katika moja ya matawi yake ni uwezeshaji wananchi, kwa hivyo avitembelee vikundi hivi afanye ratiba kama alipokuwa akifanya Mheshimiwa Haroun Ali Suleiman alivyokuwa section hii, kuona vikundi vinavyofanya kazi na pa kusaidia asaidie na inshaalla kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, naamini kuwa mabadiliko yatapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika siku ya leo tukawa hai na hatimae kutupa uwezo wa kutoka majumbani kwetu hadi hapa kwenye jengo hili kuja kuyapanga na kuyasema maneno, hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Allah na kwa vyovyote hatuna budi kumshukuru.

Ama mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumtakia rehema Mtume wetu (S.A.W) nadhani nitakuwa mchoyo wa shukurani kama sikutumia fursa hii kukushukuru wewe kwa kuweza na mimi kunipatia hizi dakika 20 au 15, sijui za kuweza kusema lolote kuhusu mada iliyopo mbele yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya dibaji fupi naomba kwanza niende moja kwa moja katika hiki kitabu ambacho hii leo tunajadili Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Hii Wizara ni miongoni mwa Wizara muhimu sana katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar hususan ukiangalia sisi ni miongoni mwa nchi masikini katika uso huu wa ulimwengu, ni nchi ambayo uwezo wa Serikali yetu kutengeneza ajira sio mkubwa, kwa hivyo hii Wizara ya SMZ imeletwa hapa kwa ajili ya kuweza kuwasaidia wananchi katika ujasiriamali na mambo mengineyo ndio ikawekwa neno uwezeshaji.

Kwa mnasaba huo Mheshimiwa kiongozi wa Wizara hii ana jukumu kubwa sana na huyu mama katika hili nimpe pole kwa sababu hii ni Wizara ambayo anatakiwa kwanza awe makini katika kufanya kazi zake, na asiegemee upande wowote anatakiwa afanye kazi zake katika mizani sawia bila ya kujali jinsia au kujali jografia ya mtu alipo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende kwenye ukurasa wa 30 ibara ya 44 hapa panazungumzia Idara ya Ushirika, naomba uniruhusu ninukuu Ibara hii katika katika ibara ya 44(4)

"Mhe. Spika, katika kipindi cha mwaka 2014/2015 Idara ya Ushirika imejipanga kutekeleza malengo yafuatayo".

Sasa kifungu kidogo cha nne kinasema:

"Kuwezesha upatikanaji wa mitaji kwa kuendeleza vyama vya ushirika".

Ile dibaji yangu nilisema kwamba huyu mama anatakiwa asiwe *bias* katika kufanya kazi zake, awe mtu wa kati kati. Sasa inasikitisha sana kwamba katika kuwawezesha wananchi kuna baadhi ya mwahala sidhani kama mama kafumba jicho au uwezo wake wa kutembelea katika maeneo unakuwa mdogo, kama kuna watu wanaohitaji kuwezeshwa na katika mambo ya kupata *Income generating* ni watu wa ukanda wa Mashariki katika kisiwa kile cha Pemba kuanzia anakotoka Dk. Hija huko ukaja zako mpaka hapa kwetu Vitongoji ukenda zako mpaka Micheweni. Huku kwahala kubaya kimaisha, nimejaribu kuangalia mimi, naangalia kwa mfano wa pale kwangu Wawi jimbo la Wawi katika ukanda huu wa Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, pale watu wengi hasa akina mama wengi nataka kwanza niwapongeze akina mama wa jimbo langu la Wawi walivyojikita katika masuala ya kuwekeza katika vikundi vidogo vidogo, lakini wanapata tatizo pamoja na hawa akinamama kujiweka katika vikundi lakini wanasumbuliwa sana; kwanza kupatiwa usajili wa vikundi vyao inakuwa ni tatizo kubwa, unapomhangaisha mwanamke wa kijijini kwa mfano Vitongoji Umangani, Vitongoji Kibokoni, Vitongoji Mfikiwa, Wawi, Furaha unapombabaisha kumpatia usajili wa vikundi basi huyu unamuhangaisha sana kwa sababu sisi tuko vijijini kule. Mambo haya ya mijini kwamba lazima ufuate maofisi mijini, sasa unamtoa leo, kesho afuate, keshokutwa afuate anapata tabu, anatulia pale pale kwa hivyo vikundi vyao vinakosa usajili.

Kuna vikundi pale ambavyo vinajitahidi sana kwa mfano kikundi cha kubanja kokoto pale Vitongoji Umangani, akina mama wamejikusanya tena wanadai *project* kwa sababu ni kikundi kimoja lakini wana sehemu nyingi, unakuta wanabanja kokoto msimu wa kaskazi lakini mvua ikinyesha wanakwenda kulima tungule na mchicha Makaani, ikinyesha mvu wanakwenda kulima, mvua ikipungua kidogo wanakwenda kuvua pweza katika bahari, alimradi ni kikundi ambacho kinalima tungule, kinabanja kokoto, kinafuga nyuki, lakini tatizo ni kwamba wanaopata mikopo ni watu wa mijini huko.

Sasa Mhe,Waziri hii ni *biasness* ya Wizara yako. Huu naweza kusema ni ubaguzi kwa sababu walipa kodi waliopo katika vijiji na walioko katika miji ni sawa sawa wanavyolipa kodi, lakini leo unakuta nitakuja kukutajia huko mbele unipatie ufafanuzi wa ile mifuko ya AK na JK . Kuna watu wangapi na hawa wanatoka wapi, uje unambie, lakini kwanza niwache niendelee.

Mhe. Mwenyekikti, kuna kikundi cha wanawake wanaofuga nyuki Kibokoni pale wale wametaka usajili mwaka wa ngapi, kuna kijana mmoja anaitwa Khamis Suleiman anafuga nyuki na vikundi vyake pale huko huko Kibokoni, kuna kinamama wapo Vitongoji Matungu hawa mama wanafuga nyuki katika mfumo wa kisasa maana wameziweka mpaka nini, lakini nimehangaika kutafuta AK na JK hawajapata, sasa wewe unafikiria Mheshimiwa juzi juzi ndio alikwenda mke wa Makamu wa Kwanza wa Rais pale akawasaidia sijui shilingi laki tano pale, akenda muwakilishi wao akatoa vile vile hela wakapata angalau mizinga mingine kidogo pale.

Sasa mimi nashangaa sana hazina kama ile watu wamejikusanya pamoja, wanazalisha mali, wanajitegemea leo mikopo hawapati wanapata watu wa mijini. Watu wa mijini wao angalu huuza udi, huuza madira lakini kule nani anauza madira Vitongoji. Wanauza modo kwa mujibu nilivyoambiwa na wataalam hapa. Nilitegemea wale wanawake wa Kibokoni, Vitongoji Umangani wanawake wa Matungu waliojitokeza katika kufuga nyuki ungewachukua mama wenzako wale ukawapeleka kwa Mhe. Waziri Mkuu Pinda, wakenda kujifunza. Kwa sababu hawana utaalam katika mambo ya ufugaji unawavunja moyo wale mama, leo unatuambia hapa kesi za kubaka zimekuwa nyingi kwa sababu hamuwaendelezi wale, wameshajitokeza mnataka warande rande mitaani hapo wabakwe huku wakidhalilishwa sasa.

Nakuomba sana Mhe.Waziri katika hili Mhe. Zainab Mkwe wangu nakuomba sana katika hili hawa akinamama wenzako uje Kibokoni uende kwa Khamis Suleiman, uje pale Vitongoji Umangani kina mama wenzako wanabanja kokoto, kuna mmoja kagongwa na jiwe hapa katika kugonga hapa hata wanja inabidi hawezi kujitia siku hizi kwa sababu huwafikirii hata miwani. Wale wanataka wasaidiwe angalau *clove.* Haya muwakilishi weye na mbunge wasaidiwe mara ngapi na mifuko ipo hii. Kila siku Muwakilishi/Mbunge huu mfuko mnaupeleka mjini tu hautufiki sisi kule, kule ndio mukawapa hawa akina mama mtatukata roho.

Mhe. Mwenyekiti mimi nafikiri katika hili uje uone wale vijana akinamama na akina baba walivyojikusanya pamoja katika kikundi cha VEKA yaani hiki ni kikundi *Special* cha kupanda miti kipo Vitongoji Udusini Makao yao Makuu wanaita VEKA (*Vitongoji Environment* C*onservation Community.* Kitu kama hiki VEKA hao wamepata usajili, lakini hizo pesa za JK amebabaishwa sana kuzipata kusukumana na miti, na hivi sasa anakuja Mhe. Fatma Fereji Mhe. Waziri wa Mambo haya ya Mazingira anatwambia kuna mabadiliko ya tabia nchi. Wale kule nendeni mukaangalie miti wanavyopanda lakini uwezo hawana. Mhe. Waziri VEKA wale waliokuwa Vitongoji Udusini ndio Makao Makuu yao tena wanaongozwa na mwanamama mwenzako Suifuni Ali Haji, anawaongoza mwanamama wenzako wanapanda miti sana kule lakini pesa hamuwapelekei mukawawezesha. Hakuna wafadhili wanavunjika moyo na huku tuna mabadiliko ya tabia nchi leo wanajitahidi kurekebisha mazingira. Wapeni moyo kwa kuwapelekea mikopo na misaada na wafadhili, ili watu wa pale VEKA na wao pale Vitongoji Umangani, Udusikni, Kibokoni waweze kupanda miti na kuweza kuhifadhi yale mazingira sawa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika vitendo vya ubakaji; kwa kweli inasikitisha sana watoto wanavyoendelea kudhalilishwa, sasa hivi akina mama hasa hawa watoto. Wazungu wanasema *children are sonorous and malleable that means we can mold a child as you want.* Sisi waswahili tunasema watoto ni sawa sawa na udongo, tunaweza kuupatiza ulimaji, ukalimaji ndio unaupatiza kuu-*mold.* Lakini binaadamu akiwa mdogo anakuwa *molded* vile mtu anavyotaka, inasikitisha Mheshimiwa hivi sasa vitendo vya ubakaji wa watoto wadogo, vimekuwa vingi, vimezidi na kesi zinaletwa Polisi mpaka Mahakamani tumepiga kelele mwaka jana hapa yaani zinadharauliwa kesi, na mimi nilipokuwa katika kamati ya wanawake na watoto ya Baraza hili, kipindi kilichopita na mwenzangu Mhe. Jabu

Hashim Ayoub na Dr. Hija. Tulikwenda kumuona mtoto wa miaka 6 kabakwa *live* tulimuona, kesi ile haikuja juu hadi leo hii. Mbakaji anaendelea kudunda.

Ndio nikasema unawabaka watoto tunataka tuwe na kundi la sijui nitumie neno gani bila ya kukiuka katiba lakini hawa watoto wanawake wanaobakwa na watoto wanaume wanaolawitiwa ni kuwa-*mold* watoto katika kuleta kundi hapa la deni la hawa mabaradhuli katika nchi. Inasikitisha sana tatizo ni nini? Tatizo ni sheria. Mhe. Waziri hebu nenda Baraza la Mapinduzi unaingia huko, waambie watunge sheria za kuwaghasi hawa wanaowalawiti vitoto wadogo na hawa akina mama wakubwa karibu mia tano na wametoa takwimu yao. Mtuletee sheria ya mavazi, kwa sababu wanatuvalia visuruwali vifupi, nguo zinawabana utafikiri maiti.

Sasa ukibakwa hapo utakuja kumskitikia nani, tatizo ni hawa watoto wadogo. Tungeni sheria ya kuwaghasi wanaobaka watoto chini ya umri wa miaka 18 mtuletee Barazani na watakaovaa vimini tutungeni sheria tuwapige bakora kabisa kabisa Mheshimiwa. Yaani msiba wa kujitakia hauna matanga wala kilio. Humo barabarani hampitiki siku hizi kwa viguo vifupi vimeenea humo, vimodo vimeenea humo na mambo haya waheshimiwa labda sisi tunaojikaza sana, lakini tendo la ndoa ni *hormonal problem,* ndio siku moja nilizungumza Mhe. Abubakar yeye ni mwanasheria si mtaalam ni mtaalam katika fani hii ya binaadamu.

Sexual intercourse ni hormonal *controlled process*, jicho likishaona linapeleka kwenye akili, inaanza kukupa maamuzi nenda kamvamie fanya hivi, fanya hivi. Dr Sira ndio anatoka mtaalam zaidi, lakini mambo haya jamani ni ya sayansi sio *Act* ya sheria. Msivimbe humu ndani, mimi ni mtaalam. Mimi ni mtu wa *biology, chemistry with education*. Hii fani ya binaadamu nimeisomea.

Kwa hivyo mimi naomba kwamba Serikali ituletee sheria ya kuweza kuwabana wanaovaa nguo fupi hawa tuwakamate, tuwafunge halafu tuwapige bakora. Ninakuhakikishia ukimwi utapungua na idadi ya kubakwa itapungua.

Nimalizie Mhe. Mwenyekiti, kwenye ile nyumba ya wazee kule Wete. Mhe. Mwenyekiti, ile nyumba ya wazee Wete yuko kijana mmoja anashughulikia wale wazee kule. Yule kijana anakaa Kangagani na kutoka Kangagani mpaka Wete kwenye nyumba ya wazee ni karibu maili 8 yule kijana ana baskeli.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemalizika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Kwa hivyo nimalizie kwa kuiomba serikali yule kijana anayewashughulikia wazee Mhe. Mwenyekiti, wampatie kipandio cha vespa ili aweze kuwahudumia wale wazee vizuri, halafu pazungushwe uzio mle kwa sababu kuku wanawatilia kinyesi mule na wengine wamepofua macho wanakalia vinyesi.

Baada ya maelezo hayo Mheshimiwa, hii hoja iliyopo ni nzuri ya Mhe.Waziri, ninamuomba sana ende Vitongoji umangani, Kibokoni, uwandani; aende kule aone akifika kinamama wenzake jinsi wanavyopata tabu katika kubanja kokoto, katika kupanda miti na awapelekee wafadhili na awapatie mikopo. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii angalau na mimi nikaweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri Zainab inayozungumzia juu ya Ustawi wa Jamii na Uwezeshaji na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii ya Mhe. Zainab ni Wizara kubwa sana na ina ukubwa wa aina mbili; ukubwa Wizara yenyewe lakini ukubwa wa mambo mazito ambayo imepewa au majukumu mazito iliyopewa. Kwa sababu inashughulikia maeneo muhimu, makundi muhimu, makundi makubwa ambayo yanahitaji umakini mkubwa sana katika kuyashughulikia. Unapozungumzia vijana inahitaji umakini, unapozungumzia wanawake; wazee ni maeneo makubwa sana katika nchi. Kwa hivyo Wizara hii ni kubwa aliyopewa mwenzetu mwanamama hapa Bi. Zainab kuisimamia sera zake pamoja na watendaji wake.

Kwa hivyo mimi kwanza nimpongeze sana kuweza kusimamia vizuri majukumu yake pamoja na watendaji wake ambao wanamsaidia wamefanya kazi vizuri. Mhe. Mwenyekiti, kabla ya maelezo nilikuwa naangalia bajeti ya Mhe. Waziri ya kipindi kilichopita, kwa sababu masuala ya fedha haya ndio mambo yote. Mwaka jana alipokuwa akiwasilisha hapa bajeti yake alituomba tumuidhinishie pesa kwa ajili ya kwenda kutekeleza malengo yale ambayo amejipangia.

Kwa hivyo la kwanza mimi kawaida huwa ninaangalia zile fedha ambazo tulimpitishia amezipata? Kwa sababu hana miujiza mengine kama fedha hakuzipata kwa maana hana miujiza ya kuweza kufanya yale ambayo amejipangia. Sasa nimeona hapa kwenye muhtasari wa mapato na matumizi yaani makadirio yaliyokadiriwa lakini na fedha aliyopatiwa kuanzia July 2013 mpaka Mei; yeye mwenzetu kaenda mbali zaidi kenda mpaka Mei 2014 kwa mujibu wa maandiko. Na kwa mujibu wa fedha aliyopatiwa kwa matumizi mengineyo mimi mara nyingi siangalii mishahara kwa sababu mishahara Waziri wa Fedha pale anatwambia ndio *first charge.*

Mimi ninaangalia matumizi mengineyo ambayo hizi ndio fedha za kufanyia kazi amepatiwa asilimia 49, sasa sijui kama kuna maalim hapa mwanafunzi anapopata Maalim Abdalla Mohammed mwanafunzi akipata *marks* 49 anapewa alama gani sijui, kama anapewa C au F au vipi.

Nikiangalia zaidi kwenye fedha za maendeleo hapa ndio kwenyewe, fedha alizopatiwa ni asilimia 29 ya fedha ambazo alikadiriwa mpaka kufikia mwezi wa Mei; hizi zikiwa ni pamoja na fedha za wahisani ambao kwa mujibu wa takwimu humu inaonekana hawa watu wamechoka. Kwa hivyo tuwe makini sana kwa sababu fedha ambazo walituahidi ni nyingi bilioni 1.3 lakini milioni 400,000,000 zilizopatikana. Lakini hata serikalini nako sijui kama na wao wamechoka, fedha za serikali zilizokadiriwa zilikuwa milioni 520,000,000 na zilizopatikana milioni 140,000,000 kwa maana hiyo hapa hakuna kazi. Lakini tuna matumaini kwamba fedha hizi na kwa bajeti ya mwaka bajeti halisia pengine mambo yanaweza yakabadilika na ile mipango ya serikali ambayo ametueleza katika bajeti iliyopita tabaan huenda mwakani tukaona *changes*. Lakini kwa mwaka huu hali sio ya kuridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia juu ya fedha na mambo mengine ambayo ameyazungumzia, Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika maelezo yake hapa amezungumzia bajeti yake jinsi ilichozingatia na ametwambia moja katika mazingatio ya bajeti yake amesema kwamba imezingatia ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi - CCM ya mwaka 2010/2015 na muelekeo wa sera za CCM za mwaka 2010/2020 tena na mambo mengine huku Mkuza na mambo mengine dira, ndio vipimo ambavyo amevitumia.

Mimi nije kwenye hivi vipimo viwili ambavyo amevieleza. Juzi Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa kwenye semina hapa wenzetu wametuwezesha sana, niliwahi kumuuliza mtaalamu katika semina juu ya utekelezaji wa sera na serikali ina jukumu gani katika utekelezaji wa sera za chama. Mtaalam akajibu kwamba serikali haina jukumu la kutekeleza sera zile za vyuma zilizomo au ilani ya uchaguzi ya chama isipokuwa pale ambapo chama kitatangaza ilani yake ya uchaguzi na wananchi wakakichagua chama kile kutokana na sera zake basi serikali ile inapokuwa madarakani ndio yenye wajibu wa kuandaa sera ambazo zitakuwa zina muelekeo wa ilani yake. Kwa kweli tumefarijika sana juu ya kauli ile na kwa kweli tumeondoka nayo.

Sasa nini kitu ambacho nimekusudia, nilichokusudia suala la sera ya hifadhi ya jamii ambapo Mhe. Waziri humu amekuwa akiisema kila wakati, ametueleza humu katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji amezungumzia juu ya Wizara kwamba imefanya vikao 10 vya Kamati Tendaji na Kamati za Uongozi na mambo ambayo ameyajadili katika Kamati; hizo ni pamoja na rasimu ya sera ya hifadhi ya jamii, sera ya maendeleo ya vijana na sera ya maendeleo ya ushirika.

Haya mambo Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia yamo kwenye ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, nadhani Bi. Zainab anakuwa anaiangalia sana. Lakini hata kwenye muelekeo wa sera za msingi za Chama ambazo zitatekelezwa kwa muda wa miaka 10 kuanzia 2010 mpaka 2020. Lakini bado tuna wasiwasi juu ya *speed* ile tuseme uharaka juu ya jambo hili, kwa sababu miaka 5 si mingi keshokutwa tumeshamaliza lakini bado hatujaona sera ya hifadhi ya jamii jambo ambalo tumekuwa tukizungumza sana, ambayo ni jambo muhimu sana.

Hili ni jambo muhimu na kwa sababu limezungumzwa na lina umuhimu wa aina yake. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri ajitahidi sana sera imalizike ije. Mimi binafsi ninampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi anayoichukua kwa kuwahifadhi wale wazee wa nyumba za wazee kule Sebleni, bahati nzuri ziko ndani ya Jimbo la Magomeni. Ameweza kufanya juhudi kubwa, ameweza kufanya ukarabati katika majengo mbali mbali majengo ambayo yalikuwa mabovu, sasa hivi kidogo yanatia sura.

Pia tumpongeze Mhe. Rais kwa kuwapatia wale wazee na wanashukuru sana wanapata chakula asubuhi, mchana na jioni, chakula kizuri hawana malalamiko. Mimi wakati mwengine nakwenda kuwauliza. Kuhusu chakula hawana malalamiko na malazi hawana malalamiko wanashukuru sana.

Kuna jambo moja ambalo wanalilalamikia sana. Sasa hili sijui liko kwako au liko kwa Mhe. Waziri wa Fedha wanachelewa sana kulipwa posho zao, wakati mwengine wanafika mpaka tarehe 15 sisi tuliogaiwa gaiwa huku tumeshazimaliza wao hawajapewa, kwa kweli hatuwatendei vyema wazee wale. Wale nao zile fedha ni sawa sawa na mishahara yao na kwa sababu wao wako pale hawana uwezo lakini bado wana mahitaji yao. Pamoja na kwamba tunawapa chakula ambayo ni mahitaji muhimu lakini bado wana mahitaji mengine ambayo wanahitaji kuyatumia.

Sasa kitendo cha kuwachelewesha wale maana yake tunawatia unyonge. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri ikiwa hili unacheleweshewa weye jitahidi, ikiwa zile fedha zinachelewa Wizara ya Fedha Mhe. Waziri wa Fedha bahati yupo anasikia. Lakini wale wazee ni lazima tuwatunze, tuwahifadhi vizuri na wasiwe na manun'guniko na ndio sera ya Chama cha Mapinduzi inavyosema, kwa hivyo tutekeleze ilani hii kupitia serikali ili wazee wale wasiweze kubabaika.

Katika suala la hifadhi ya jamii kwa watu wote ambapo hapo nataka nipaeleze, hili ni muhimu pamoja na umaskini tuliokuwa nao, hapa kwetu Mhe. Mwenyekiti, mzee ni yule ambaye ametimiza zaidi ya miaka 60 na kuendelea. Na wazee wale wanaopewa pencheni na si wazee peke yao wale waliotumikia serikali, lakini hata wale wakulima na wafugaji na wavuvi wakishatimia umri ule wanahitaji hifadhi, wanahitaji kusaidiwa. Serikali ina jukumu la kuwaenzi sio wale wazee ambao tumewaweka tu pale au wale tunaowagaia shilingi elfu tano tano, wazee wote wa nchi hii wanahitaji kuenziwa.

Kwa sababu wazee na wao wana mchango katika serikali, hizi kodi wanazolipa ambazo sisi ambao tulikuwa watumishi wa serikali tunajipendelea ndio tunapeana viinua mgongo na pencheni lakini hawa wakulima watapata nini ambao walikuwa wanahangaika na maisha yao. Kwa hivyo hawa wanahitaji nao kuenziwa na serikali. Mzee akishatimia zaidi ya miaka 60 anahitaji kutunzwa na serikali ndio yenye jukumu la kumtunza. Sasa kama tunawaachia ndio maana wanakufa mapema.

Wakati mmoja tulipokuwa kwenye semina fulani na bahati wizara yako ndio iliyotufanyia semina walitupa takwimu juu ya wazee wa nchi nyengine, walitupa mfano Malaysia ukiangalia wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 na kuendelea zaidi ya asilimia 15, lakini ukija kwetu hapa ni asilimia 4 tu ya wazee wenye umri huo sasa hapo tujiulize kulikoni? Kwa nini wazee wa Malaysia wanachelewa kufa wazee wetu katika nchi za Afrika wanakufa haraka.

Sasa hilo ni suala la kujiuliza linatokana na namna serikali inavyowahifadhi wazee wao, tayari wenzetu wanawatunza, wanawafanyia kila linalowezekana na wanapata kuishi na kwa sababu wanakuwa hawana wasiwasi mkubwa katika maisha yao. Hilo jambo ambalo linasababisha waishi zaidi. Kwa hivyo Mhe. Waziri wala hili halihitaji fedha maana watu wanaogopa ogopa kwamba labda fedha zitakuwa nyingi, hatuwezi kuwaendeleza, si suala la fedha ni mipango tu Mhe. Waziri.

Tukiwa na mipango mizuri ukituletea sera hapa tukizielekeza uwezo wa kuwahudumia wazee waliozidi zaidi ya miaka 60 upo na tunaweza tukawahudumia wote. Kwa hivyo pitisheni sera mtuletee na sisi *at least* tuione pamoja na kwamba sera mnapitisha wenyewe, lakini na sisi tutatoa mchango wetu katika sera hiyo na kuhakikisha wazee wenye umri kama huo basi na wao wanakuwa wanaenziwa na wao wanapata haki zao. Kwa sababu nao wana haki.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo Mhe. Waziri ametueleza kwenye kitabu chake ni suala la mikopo.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante mimi sina mchango mkubwa najua wenyewe kina mama wanatuelewa wataichangia.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la mikopo ni kwamba ametoa mikopo, makadirio yake ya mikopo ambayo alitegemea kutoa ni kiwango kikubwa milioni 3 na amejitahidi kutoa karibu milioni 294,000,000 katika kipindi hiki, kwa kweli amejitahidi. Pia ameonesha hapa nani amepata mkopo na nani hajapata mkopo. Mhe. Waziri nataka aje anieleze katika eneo hili la Wilaya za Mjini ambao watu waliopata mikopo wameelezwa hapa mpaka Machi jumla wanawake 28 na wanaume 30 *total* ni 58 na vikundi 7 ambazo fedha zimetajwa.

Mhe. Mwenyekiti, bado kuna malalamiko kwa wananchi wangu wa Jimbo la Magomeni wanasema wamekuwa hawapati mikopo, sasa hebu Mhe. Waziri utakapokuja kufanya majumuisho utwambie maana hapa umetuletea kwa

jumla jumla, uje uniambie katika watu hawa waliopata mikopo na hivi vikundi vilivyopata mikopo wananchi wa Magomeni ni wa ngapi waliotoka katika shehia hizo ambao wamefaidika na mikopo hiyo. Na hivi vikundi ni vikundi vingapi katika jimbo langu ambavyo vimepata mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka wananchi nao wasikie kwa sababu isije ikawa wanalalamika kumbe huku wanapata. Pengine wao wakishamuona kiongozi wao wanadeka Mheshimiwa, hatupati mikopo kumbe mikopo inapatikana. Kwa hivyo, hebu Mhe. Waziri uje utoe kauli wananchi wa Magomeni wakusikie kwamba ni wangapi kati ya hawa uliowataja waliotoka katika Shehia za Magomeni na vikundi ambavyo viko Magomeni ambavyo vimepata mkopo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kweli sitochukua muda wako mwingi hoja yangu kubwa ilikuwa ni kuzungumzia sera ya hifadhi ya jamii nimuombe Mhe. Waziri aje atueleze ni mipango gani na lini sera hiyo ataileta ili wazee ambao wanaishi hapa Zanzibar na wao waweze kufaidika kama wazee wa nchi nyengine.

Vile vile Mhe. Waziri aje anieleze wakati wa kufanya majuisho kwa sababu sasa hivi wako katika hatua za kuandaa sera, wazee wa Zanzibar ambao wangestahiki kupata hifadhi hii au posho hii ya kujikimu ni wa ngapi wameshafanya *research* hiyo. Ni wazee wa ngapi wa Zanzibar ambao ni asilimia ngapi ya watu waliopo. Kwa sababu atakapotupa takwimu hiyo basi tutajua tutakuwa na moyo wa kuona kweli wizara yake ina lengo la kutekeleza jambo hili.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana na namtakia kila la kheri Mhe. Zainab Omar na naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru ahsante.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu Subhanahu Wataala kwa kutujaalia kuwa hai, wazima na tukiwa na nguvu ya kuendelea na shughuli ambazo zimetuweka hapa. Nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kutoa mchango wangu katika bajeti ya Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kuwasilisha bajeti hii baada ya kuwa wameiandaa wizarani kwao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kuchelea muda naomba nianze kwanza kwenye vifungu halafu muda ukiniruhusu nichangie maeneo machache ambayo nataka kuyatolea maoni.
Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi kama sikupata maelezo ya ziada bajeti hii nitaizuia, nitaiondolea shilingi kwa upande wangu, lakini ikiwa nitaridhishwa na maelezo ya Mhe. Waziri basi shilingi hiyo nitairejesha. Hiyo ni kwa upande wa mafungu lakini baadae nitakuja kwenye sera vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema nitaizuia kwa kuiondolea shilingi ni kwamba najiuliza tena na tena kama nilivyouliza katika wizara kadhaa, hivi kipaumbele cha serikali yetu hii katika utendaji wa wizara zake kiko katika kuwahudumia wananchi au kiko katika watendaji na viongozi wa wizara mbali mbali kutafuna fedha kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika hali ya kawaida serikali huwa inagawa sekta mbali mbali katika wizara, sekta hizi zinategemewa zitoe huduma kwa wananchi, tukisema Wizara ya Afya maana yake wizara ile imepewa jukumu la kusimamia kutoa huduma ya sekta ya afya kwa wananchi.

Tukisema Wizara ya Elimu inatakiwa itoe huduma ya sekta ya elimu kwa wananchi na tukisema Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto maana yake ijikite kutoa huduma zinazohusika katika maeneo hayo ya uwezeshaji, ustawi wa jamii, vijana, wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, napata wasi wasi sana kwamba inavyoonekana kipaumbele si huduma zilizokusudiwa katika wizara kama jina lake linavyoonesha, lakini badala yake ni posho, safari na mambo mengine kama hayo. Kwa sababu hiyo namuomba Mhe. Waziri anipe maelezo ya kutosha.

Serikali imetwambia katika mwaka huu wa fedha imeamua kupunguza safari, imetwambia semina imekusudia kufanywa katika kumbi zake zenyewe na kupunguza gharama zake. Lakini bajeti hii kama ilivyokuwa bajeti za

wizara nyengine mwelekeo wake unaonesha uko pale pale bado kipaumbele cha safari, bado kipaumbele ni viburudishaji kwenye semina na mambo kama hayo Mhe. Mwenyekiti. Naomba nitoe mifano Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika ofisi kuu Pemba na haya ninayoyataka ndiyo nitakayoyaombea maelezo, na kama sikuridhishwa nitayazuia katika bajeti. Mhe. Mwenyekiti, ofisi kuu Pemba gharama za safari mwaka jana zilikuwa zimeombwa milioni 15,285,000 mwaka huu zimeombwa milioni 25,302,000. Sasa najiuliza hapa kweli serikali lengo lake ni kupunguza safari au kuongeza safari?

Mhe. Mwenyekiti, yale yale niliyoyahoji kama deni la afya gharama za mafuta na vilainisho sina muda wa kusema moja moja. Lakini kwa jumla mwaka jana ilikuwa ni milioni 20, 870,000 mwaka huu ni 31, 634,000 hiyo ni kwa ofisi kuu Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kwenye vifaa na huduma za ofisi mwaka jana ilikuwa 12,720,000 mwaka huu ni 24, 355,000. Katika fungu la matengenezo ya zana mwaka jana ilikuwa ni milioni 8,700,000 mwaka huu ni milioni 11,646,000.

Mhe. Mwenyekiti, angalia sasa kwenye ruzuku ofisi kuu Pemba kwenye huduma hasa imekusudiwa basi maendeleo ya wanawake na watoto mwaka jana ilikuwa milioni 9,000,000 mwaka huu imeteremka imekuwa milioni 4,000,000. Lakini mwenge wa uhuru imepanda kutoka milioni 3,600,000 mwaka huu ni milioni 6,300,000.

Sasa najiuliza Mhe. Mwenyekiti, kwamba hivi ndivyo vipaumbele bado sehemu kubwa ya bajeti inakwenda kuhudumia wataalamu na watendaji wa ofisini badala ya kujielekeza kutoa huduma zinazohusika katika sehemu hii.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo hivyo kwa sababu ya muda naomba Mhe. Waziri aangalie Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwenye fungu la safari mwaka jana lilikuwa ni milioni 47,960,000 mwaka huu ni milioni 75,870,000. Tunaambiwa mwelekeo wa serikali mwaka huu ni kupunguza safari, lakini bajeti imetoka 47 milioni imekuwa 75 milioni. Kwenye fungu la vifaa na huduma za ofisi kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti Mhe. Mwenyekiti naomba maelezo hususan katika kijifungu 220514 sera na sheria (*Policy and Laws*) kumeombwa milioni 25, 455,000 mwaka jana kuliombwa milioni 27,515,000. Naomba wenyewe wanambie ni sera na sheria zipi ambazo kila mwaka zinaombewa mafungu makubwa kama haya ya fedha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ingelikuwa fedha hizi za sera na sheria ni za kufanya utafiti kwa ajili ya kuandaa sera na sheria hizi bado kuna fungu jengine katika ruzuku katika idara hiyo ya mipango ya sera na utafiti kwenye huduma za utafiti kuna 33,255,000 milioni. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo kuhusiana na fungu hili.

Mhe. Mwenyekiti, lakini halafu kuna mikutano ya ushirikiano wa kimataifa katika matumizi mengineyo pana milioni 1,200,000. Mimi najiuliza milioni 1,200,000 zinafanya shughuli gani ya mikutano ya ushirikiano wa kimataifa. Maana hii ushirikiano wa kimataifa maana yake ninavyofahamu ni nje ya nchi, najiuliza katika milioni 1,200,000 zinafanya shughuli gani wakati pia kuna fungu la safari. Naomba maelezo katika maeneo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika Idara ya Wanawake na Watoto gharama za safari tunaambiwa lengo ni kupunguza mwaka jana ilikuwa milioni 14, 000,000 mwaka huu imeombwa milioni 15,820,000. Lakini siishii hapo tu naomba maelezo vile vile kwa Mhe. Waziri kwamba kwa nini wizara yake inaonekana kama vile kuna ubaguzi katika *allocation* ya misaada. Kwenye fungu la misaada ya kijamii, maendeleo ya wanawake na watoto nikiamini idara hii inahudumia Unguja kuna milioni 15,410,000 lakini kule Pemba kulikuwa kuna milioni 4,000,000 kwa nini uwiano huu umepishana kiasi kikubwa namna hii.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile katika Idara ya Mikopo fungu la viburudishaji limechupa kutoka milioni 9,290,000 mwaka jana, mwaka huu linaombewa milioni 12,760,000. Mhe. Mwenyekiti, katika Idara ya Maendeleo ya Vijana fungu la safari lilikuwa milioni 8,000,000 mwaka jana mwaka huu limebakia milioni 8,000,000 tunaambiwa lengo ni kupunguza safari lakini gharama hazioneshi ama kubakia pale pale au kuongezeka. Nilikuwa naomba maelezo katika mafungu hayo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, eneo jengine ambalo naomba maelezo kuna ada ya mikataba imeonekana katika idara mbali mbali za wizara hii, sitaki kutoa mfano mmoja mmoja kwa sababu ya muda naomba anisaidie kwa ujumla wake hii ada ya mikataba inahusu mikataba gani katika idara tofauti ambazo kaziombea fedha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile naomba nisaidiwe kuna Idara ya Ustawi wa Jamii, Unguja jumla ya fungu lake ni 744,644,000 najua imechanganywa na mishahara. Lakini Pemba kwa ujumla wake idara hiyo hiyo imetengewa milioni 78,000,000.

Kwa Pemba kuna upungufu mwaka jana ilikuwa milioni 105,000,000 mwaka huu imeombewa 78,000,000 milioni, lakini kwa Unguja kuna ziada mwaka jana ilikuwa 687,000,000 mwaka huu 744,000,000. Naomba anipe *justification* yakutokuwa na uwiano kabisa katika masuala haya.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile hebu anisaidie sijui takwimu zikoje katika gharama za kuendesha nyumba za wazee na wa ngapi wako Unguja na wa ngapi wako Pemba. Lakini katika fungu la misaada ya kijamii katika Idara hii ya Ustawi wa Jamii kwenye gharama za kuendesha nyumba za wazee kwa Unguja kumetengwa milioni 120,000,000 lakini kwa Pemba kumetengwa milioni 12,000,000 tu asilimia 10 ya kile ambacho kimetengwa kwa upande wa Unguja. Naomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo katika eneo hili.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda naomba nimalizie kwa mafungu Idara ya Utumishi na Utawala. Idara ya Utumishi na Utawala naomba kwanza nipewe maelezo kuhusu huduma za mtandao wa serikali *E-government* ni milioni 20,000,000 kama mwaka jana. Mimi sijaona mpaka leo hii *E-government* ikifanya kazi wala sijaona mradi huu kama umefika popote, hizi 20,000,000 zinaombwa kila mwaka zinafanya shughuli gani wakati *E-government* haija-*take off* mpaka hii leo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile viburudishaji katika idara hii mwaka jana vilikuwa milioni 5,750,000 mwaka huu ni 11,900,000 milioni takriban mara mbili. Hii ni Idara ya Utumishi inayohudumia pale ofisini ongezeko hili kwa nini limekuwa kubwa kiasi hicho.

La kutisha zaidi Mhe. Mwenyekiti katika gharama za safari katika idara hii mwaka jana ilikuwa gharama za safari ni milioni 10,320,000 mwaka huu imeombewa 43,800,000 hiki ndiyo kipaumbele cha Waziri Mhe. Zainaba na watendaji wake kwamba bajeti ya safari ambazo tunaambiwa zinapunguzwa mwaka huu imeongezeka kwa asilimia 400, na safari hizi anakwenda nani maana mama yangu Mhe. Zainab namuona siku zote yuko hapa hapa labda achukuliwe na Mhe. Rais katika safari zake. Hizi safari hizi za wizara wanakwenda nani na tumeambiwa madhumuni ya serikali ni kupunguza safari kwa mwaka huu kuelekeza kutoa huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo katika gharama za mafuta na vilainisho sijaona kama kuna mpango wa kununua gari mpya katika fungu la idara hii. Lakini ajabu gharama za mafuta na vilainisho zimetoka 28,270,000 mwaka jana zimekuwa 58,795,000 kwa mwaka huu, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Pia naomba maelezo kuhusu matengenezo madogo ya ofisi katika idara hii ambapo kumeombwa milioni 48,000,000 ukilinganisha na milioni 8,000,000 za mwaka jana.

Mhe. Mwenyekiti…

Mhe. Mwenyekiti: Dakika tano ya ziada.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante na kwenye matumizi mengineyo vile vile katika Idara ya Utumishi na Uendeshaji mwaka jana ilikuwa milioni 1,450,000 mwaka huu ni milioni 7,300,000 naomba maelezo. Mhe. Mwenyekiti, na moja kwa ujumla wake naomba Mhe. Waziri akija anitosheleze kwa miradi yote ya maendeleo ambayo iko katika wizara hii iliyopo katika kitabu hiki cha makisio ukurasa wa 595 mpaka 596 kwa sababu kile kitabu hotuba yake ya bajeti nimeangalia sikuridhika sana na mchanganuo wa miradi hii imekusudia kufanya nini na kuleta tija gani kwa wananchi wake.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie hizo dakika zangu tano kwa kusema nimeuliza haya nilikuwa namchokoza mwenzangu hapa, sisi tulidhani kwamba hizi huduma hazifiki labda katika majimbo kama yetu sisi ya Mji Mkongwe, lakini nimeshtuka kusikia Mhe. Salmin Awadh pia na yeye leo anataka maelezo kwa sababu anapata malalamiko kwamba Magomeni hayajafika vile vile.

Sasa najiuliza kwamba tunaunda wizara zile mishahara tu na safari na maposho lakini huduma zilizokusudiwa hazifiki kwa wananchi. Kwa nini mwananchi mnyonge na masikini ya Mungu wa Zanzibar anayekwenda hospitali

hakuna dawa, skuli akaambiwa achangie, vitabu hakuna, hakuna hiki lakini bado achangia mamilioni haya kuendesha wizara ambayo haimletei tija yoyote kwa sababu huduma hasa hazimfikii mwananchi. Naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama nilivyosema haya yalikuwa ya mafungu wala sijutii kutumia muda wangu takriban wote kudai mafungu kwa sababu nadhani huko ndiko wananchi wanakotaka kujua fedha zao zinatumika vipi.

Jengine nilikuwa naomba kusaidiwa sasa katika sera, wizara hii imepewa jukumu la kulea makundi ya kijamii. Moja katika makundi yaliyotajwa ni kundi la vijana. Mhe. Mwenyekiti, kiu kubwa ya vijana ni kuandaliwa kielimu hayo tuyaache tutakuja kuyazungumza katika Wizara ya Elimu tukifika.

La pili ni kuwawezesha na kuwasaidia kupata ajira, sasa ningeomba Mhe. Waziri akija atwambie serikali ambapo kwa sekta hii ni wizara yake inayosimamia imeandaa mpango gani wa kuwasaidia vijana wetu waliochoka kukaa mabarazani wakiwa hawana kazi za kufanya.

Mhe. Mwenyekiti, *ZASOZE* haiwezi kuwa ajira ya mtu kutegemea maisha yake yote, hizi ni ajira za kujishikiza za kupita, serikali ina mpango gani wa kuwapatia hili jeshi kubwa la vijana katika nchi yetu ambayo kila mwaka wanatoka tena maskuli kwa maelfu wanahitaji kupata ajira. Ina mpango gani kuendeleza vijana humu katika bajeti yake Mhe. Waziri mimi sioni kitu, naona mafungu yamenona katika safari, posho, viburudishaji, semina na mambo mengine kama hayo. Namuomba Mhe. Waziri akija anisaidie maelezo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile imesemwa hapa kuhusu wazee, mtu akishafikia umri wa mzee maana yake ameshapitia utoto na ujana, keshatoa nguvu kazi yake kutumikia nchi yake. Sasa Taifa ambalo haliwaheshimu wazee haliwezi kuwa Taifa la kistaarabu na la kiungwana, huu utaratibu uliozoeleka miaka na miaka kwamba huko tulikotola Mzee Karume alionesha utaratibu mzuri tu, Mungu amlaze mahala pema. Lakini leo wazee wetu wamezagaa ovyo mitaani humo wamegeuka omba omba watu ambao wametoa jasho lao kuijenga nchi hii Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, wizara ina mpango gani katika hili, na nimwambie kabisa nilipomuomba maelezo na katika mafungu nitakuja kumzuilia kama hakunitosheleza, katika miradi ya maendeleo tumezoea kila mwaka kuona panatengwa fungu hili kuhusu sera, sera hizi hazifiki mwisho zikazaa tija kwa wananchi wanaohusika? Kuna mpango gani wa kuweka sera.

Mwaka jana tulizungumza mimi na Mhe. Salmin Awadh Salmin katika bajeti hizi hizi, serikali ina sera gani kuhusu kuwezesha kulipa wazee wanapofika umri wa kustaafu kuwahudumia, Ustawi wa Jamii, *Social Security.* Hatuna kitu leo hata wale wanaotumikia serikali wanadhalilika, kila siku wanatwambia mnatetea wafanyakazi sisi mbona mnatusahau, posho wanayolipwa, kiinua mgongo, pencheni, ni kiwango kidogo kabisa hawezi mtu akakidhi mahitaji yake haya ya siku tano katika mwezi. Sasa wizara hii imekuwa inafanya nini?

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nimalizie la mwisho kwa dakika mbili tu, nimuulize Mhe. Waziri aje anambie, hivi hiki kitu kinachoitwa Mwenge wa Uhuru kinaleta tija gani katika nchi ya Zanzibar? Nimeangalia katika ukurasa wa 92 wamesema pamechangwa shilingi 66,000,000 kwa ajili ya kuhudumia mwenge wa uhuru, lakini sijui katika kile kinachoambiwa kinafaidisha kwamba kinakwenda kuzindua miradi ya wananchi, miradi ya wananchi si lazima izinduliwe kwa mwenge, ingeweza kuzinduliwa katika sherehe za Mapinduzi. Kuna sherehe nyingi za kitaifa, lakini najiuliza kuna gharama kiasi gani zinazotumika kwa kukimbiza mwenge ambazo pengine zinaweza kutumika kusaidia masuala yanayohusu ustawi wa jamii katika nchi hii na hata historia nao Zanzibar hatuna. Mwenge wa uhuru ni asili ya Tanganyika umetokana na *TANU,* Afro Shirazi haikuwa na mwenge katika nchi hii.

Sasa mwenge huu kwa wananchi wa Zanzibar kuambiwa waugharamie ukazunguka kwa gharama zao, lakini haujaleta tija yoyote katika nchi hii mwananchi wa Zanzibar anafaidika nini, kwa nini tuendelee kuwa na kitu kama hicho. Naomba majibu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo kama nilivyosema siiungi mkono bajeti ya wizara hii mpaka nitapopata maelezo ya kutosha katika vifungu hivyo ntakavyosema. Kuna suala la shilingi moja nilozuia katika matumizi sijaridhika na maelezo, lakini pia namwambia kabisa na shilingi mia kuhusu sera katika mambo mawili

niliyozungumza, Sera ya Vijana na Sera ya Wazee. Naomba maelezo kuhusu Ustawi wa Jamii ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa katika hali ya uzima na afya njema sote, pia nikushukuru wewe Mwenyekiti kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyotutolea hapa. Pia niwapongeze watendaji wote wa wizara yake kwa kazi yao nzuri waliyoifanya na ya kupigiwa mfano kiutendaji. Lakini pia nimpongeze sana Mwenyekiti wetu wa Kamati, Mhe. Mgeni Hassan Juma na wajumbe wake wote kwa kutuletea ripoti yao ya kamati na imefafanua mambo mengi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze katika ukurasa wa 10 kifungu nambari 18, ambacho kinaeleza, Ilani ya CCM mwaka 2005 na Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwa kweli niipongeze sana ilani hii kwa kuona hii wizara ina umuhimu wake kwa vijana, wanawake na watoto wetu hasa suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nianzie hapa katika ukurasa wa 23 kifungu 39. Kwanza niipongeze sana wizara na serikali kwa ujumla, imetoa mafunzo kwa wanachama 2,372 wakiwa wanawake 1,569 na wanaume 803, kwa kuwapa taaluma na mafunzo mbali mbali ya kibiashara, kilimo, ufugaji na ushoni; yote haya ni moja ya ujasiriamali katika kuwawezesha hawa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, serikali ina nia njema kwa wananchi wake kuwawezesha kuwafundisha ujasiriamali, lakini tatizo kubwa la kuwawezesha hawa wananchi wetu hasa katika kuwapa hii mikopo nafuu, ili waweze kujikwamua na kazi ngumu na kuweza kufanya maisha yao na biashara ndogo ili wapate riziki zao za kila siku. Lakini vigezo na masharti vimekuwa vigumu hasa katika taasisi hizi husika. Wananchi wetu wanakwenda kuomba mikopo wanapata tabu, ukitizama masharti wanakuwa hawana vigezo wanashindwa kutimiza malengo yao katika kupeleka vigezo hivyo na kushindwa kufanya makusudio yao katika dhamira zao za kufanya biashara ya kujikwamua na hali ngumu ya maisha.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa zaidi ni kwamba wanakosa hii mitaji ambayo ndio mikopo. Kwa hivyo, hali zao zinakuwa duni na mawazo yao yanawapelekea kubaya, wanakwenda kwenye mambo ya madawa ya kulevya na mambo mengine ambayo sio sahihi kufanya kwa vijana wetu. Kwa hiyo, naomba sana haya masharti ya hii mikopo yapunguzwe, wananchi wetu waweze kuaminiwa na wapate fedha hizo za kufanyia kazi ili waweze kurejesha kwa muda mfupi na kujipatia kipato ili kufaidika na maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, niende pia katika ukurasa wa 36 kifungu cha 48. Hapa serikali imeonesha kitu kizuri kwa nia njema kabisa kwa wananchi wake na mfano mzuri wa kuigwa kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwakopesha shilingi 300,000,000. Ukipiga mahesabu pesa hizi kuwakopesha wajasiriamali basi kila kikundi kimepata shilingi 3,000,000. Kwa kweli sio kazi ndogo ni kazi kubwa na mimi nawapa pongezi serikali nzima kupitia wizara kwa kazi hii waliyoifanya kubwa kabisa.

Kuna vikundi 1,000 vya uchumi ambavyo baadhi ya watu wameungana kufanya biashara na watu binafsi wamepata mikopo hii. Lakini mimi naomba sana hizi pesa zinapotolewa viangaliwe vikundi hivi binafsi, mara nyingi utasikia kuna vikundi binafsi lakini inakuwa ni vikundi vya familia kama baba, mama, mtoto; wanapewa pesa halafu inakuwa urejesho wake sio mzuri au inakuwa kikundi cha ubinafsi fulani hivi kwa mtu fulani.

Kwa hivyo, naomba sana waangalie vikundi hivi tumewapa pesa hizi watu binafsi hawa hapa, wawapitie na waangalie kwa umakini isiwe pesa zile wanafaidika familia moja tu, iwe familia tofauti. Naomba hapa Mhe. Waziri aangalie sana suala hili la utoaji wa pesa kwa vikundi.

Mhe. Mwenyekiti, vijana sote tunaamini kwamba kukosa ajira kwa vijana wanawake wanapoteza malengo, wanakosa mwelekeo wa maisha kabisa, wanapoteza dira yao ya maisha na malengo waliyojipangia kwa kukosa ajira. Ajira ni kitu muhimu sana katika maisha ya binadamu, mara nyingi watu kama hao wanapotea na wanakwenda kwenye madawa ya kulevya, kwenye biashara haramu au kwenye umalaya ambapo si kazi nzuzi na mwisho wake

kupata maradhi ya UKIMWI. Mara nyingi tunapiga vita UKIMWI lakini utakuta ajira ni kitu muhimu, wananchi wana shida wanapata tabu katika maisha anakwenda kwenye biashara haramu. Sasa ili apate kipato ndio maana mara nyingi wananchi wetu wanaathirika kwenye ugonjwa wa UKIMWI.

Jana nimeangalia televisheni ya *Channel Ten* kuna mfanyabiashara mmoja kwa kweli kanisikitisha sana, anachukua wanawake kutoka India analeta Dar es Salaam pale anawachezesha ngoma, anawafanya biashara anayoijua yeye na yule Muhindi kachukuliwa mpaka na vyombo vya habari na atachukuliwa hatua. Mimi naomba sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yule jamaa anavyowadhalilisha wale wanawake wadogo miaka 16 achukuliwe hatua, afungwe hata miaka 10 au 20, akae jela iwe funzo kwa wengine wanaopenda kuwadhalilisha wanawake.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili lipo na tumeona mfano mzuri kwenye televisheni hiyo juzi wanavyodhalilishwa wanawake. Kwa kweli hili lichukuliwe hatua na apate adhabu kubwa mfanyabiashara huyo kwa kuwadhalilisha hawa watoto wa kike chini ya miaka 18.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala la ajira. Serikali itizame sana suala la ajira za watoto, watoto mitaani wanapokaa wanakuwa wanafanya ajira za ajabu ajabu. Kwa hivyo, serikali iangalie sana ajira za watoto wa mitaani. Baadhi ya wakati utakuta watoto wanakosha magari, wanafanya kazi ndogo ndogo ili wapate pesa za hapa na pale kwa vile maisha yao ni magumu, hivyo aangalie suala la watoto katika suala la ajira.

Pia sasa hivi utakuta watoto wengi wanaombaomba chini ya miaka minane, kumi, hawafanyi kazi, hawasomi na kwa Zanzibar sasa hivi hicho ni kitu cha kawaida sana, kumkuta mtoto anaomba mitaani ili apate pesa za matumizi.

Mhe. mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aliangalie suala hili la ajira za watoto na haileti taswira nzuri katika nchi yetu, linasikitisha sana suala hili kuwa linatendeka.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie katika ukurasa wa 36 kifungu namba 49. Kwanza niwapongeze sana hawa ndugu zetu wa Benki ya *CRDB*, kupitia Mfuko wa Vijana kwa mikopo. Kwa kweli benki hii imeonesha uungwana na imeonesha imani kubwa kwa vijana wetu kuweza kuwakopesha katika kitabu hiki cha Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, naomba na benki nyengine ziige mfano kama huu wa kuwasaidia vijana wetu kuwakopesha mikopo nafuu ili waweze kujiendesha. Benki hii imeweza kuwapa vikundi 116 sawa na shilingi 200,045,000 ili waweze kufanya biashara zao za kawaida na kujipatia kipato. Kwa kweli ni mfano mzuri na iwe mfano kwa benki nyengine pia wajitolee kama hivi kusaidia wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wetu wana mawazo mazuri na nia njema ya kufanya kazi, wanajitahidi sana lakini tunapowapa fedha kama hizi pia tuwafungulie milango ya kufanya biashara. Mimi nasikitika sana nitaizungumza hapa lakini Mhe. Waziri pia aangalie madhali wadau wake vijana awatizame anapofanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wanachukua mikopo wanafanya biashara, wana mawazo mazuri ya biashara, wanatoka hapa na mizigo wanapeleka Dar es Salaam, lakini la kusikitisha wakifika Dar es Salaam wanalipishwa ushuru wa ajabu. Kwa kweli hata hii mikopo inafilisika kwa sababu ushuru iliopo pale ni mkubwa. Kwa hivyo, Mhe. Waziri azungumze na wizara husika waweze kuondoshewa ule ushuru wa pale Dar es Salaam ili vijana wetu waweze kufanya kazi vizuri wapate kwenda na kurudi ili kuondosha ajira za serikalini kila siku.

Vijana wengi hivi sasa wanasikitika kwa ushuru huo, friji moja dola 70, utakuta mtaji wake shilingi milioni moja sasa unakuta hawezi kurudisha pesa zake, televisheni moja *used* analipishwa shilingi 15,000. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri hawa ni wadau wake awatetee sana kufanya biashara hizi wasije wakafilisika, awaoneshe milango ya kupita na waweze kufanya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika mikopo hii wananchi mbali mbali wanakuwa wanachukua mikopo wanataka kusoma, lakini unakuta wakati mwengine mikopo hii hawapati wakati inayotakiwa. Wanafunzi wengi wanataka kwenda Vyuo Vikuu kusoma lakini hawana fedha. Kwa hiyo, naomba pia suala hili wizara ilifuatilie suala la mikopo na hizi benki aweze kuzungumza nazo kuweza kuwakopesha wanafunzi hawa wanaotaka kwenda kusoma kwa sababu wana nia njema ya kusoma ili kuendesha taifa letu hili siku za baadae.

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya vijana pia wamekata tamaa kabisa na maisha yetu, yaani wamejitolea kufanya mambo ya ajabu ajabu kwa sababu zile fedha hawazipati na mawazo yao yashakuwa yana tamaa wanaona sisi ndio tumeshafika kwenye hali hii, hatutokwenda mbele ndio maana wanaingia kwenye uhalifu na madawa ya kulevya wanaona ndio njia yao ya kupata fedha. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri tuangalie sana mikopo hii vijana waweze kuingia kwenye miradi mizuri na masomo ili waweze kufanya kazi vizuri. Naomba sana aliangalie hili Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kidogo suala la ajira, wananchi wengi wanalalamika kuhusu suala hili, lakini suala la ajira sio la serikali peke yake. Mimi naomba sana taasisi binafsi, jamii pia, wafanyabiashara, wawasaidie hawa vijana ili waweze kupata ajira kwa njia ya hali hii au nyengine. Kwa sababu hili suala isiwe mzigo kwa serikali peke yake, haitaweza kuajiri vijana wote, haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika ukurasa wa 12 suala zima la ubakaji. Suala la ubakaji limekuwa ni tatizo kubwa katika nchi yetu hii ya Zanzibar hasa Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba. Ukitizama matukio mengi yanayotokea ya watoto kubakwa basi ni katika sehemu hizo mbili, cha kusikitisha hawa watoto wakishafanyiwa mambo haya wale wanofanya mambo haya hawapati ile adhabu . Kwa hiyo, mimi naomba sana matatizo haya yaondoke wapate adhabu hawa wanaofanya vitendo vya kishenzi na vibaya kabisa, naomba kesi hizi sitaki kuzisema sasa hivi, lakini Kaskazini Unguja na Kaskazini Pemba suala la ubakaji limekuwa tatizo kubwa. Naomba lifuatiliwe vizuri ili waweze kupewa adhabu hawa na iwe fundisho kwa wengine wasifikirie kabisa suala hilo kulifanya.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye ukurasa wa 12 na hapa niipongeze sana serikali kwa kupiga hatua vitendo vya unyanyasi wa wanawake na watoto ukilinganisha na nchi nyengine za Afrika hasa kuzipitia sheria zinazowahusu watoto na wanawake. Niipongeze serikali kwa hilo imejitahidi kidogo kila hatua zinavyokwenda inazidi kujitahidi, lakini bado nataka msukumo uendelee.

Mhe. Mwenyekiti, kuna watoto hali zao ngumu, masikini, hawawezi hata kusoma skuli hawana hata ile ada ya kutoa skuli. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri hawa watoto wasaidiwe. Kwa sababu watoto hawa wanatembea mitaani sasa hivi ukimkuta mtoto ukimuuliza usharudi skuli anakwambia siendi skuli wala popote kwa sababu wazazi wangu hawana fedha ya nauli au ada ndogo ndogo kama mabuku, *uniform* hawawezi watoto hawa wanahangaika mitaani na wanakuwa sio taifa zuri la kesho.

Nilikuwa naomba waziri aliangalie sana suala hili na ukitizama watoto hawa hasa wanawake. Kwa sababu tatizo katika jamii yetu hawa wanawake kidogo watu wa staha na watu wa kupata kazi nzuri, mimi naomba sana hasa wanawake wajitahidi wasome kwa sababu inapokuwa hawajasoma wanabeba zege kufanya kazi za ajabu haipendezi. Kwa hivyo, naomba wajiangalie watoto wanawake na serikali pamoja na wizara iwaangalie sana kwa kuwasaidia kuwasomesha watoto hawa kwa sababu mazingira yao sio mazuri kufanya kazi kama za wanaume haipendezi.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika majimbo yetu madaktari bingwa hamna hasa kwa hawa watoto, wazee wanapata tabu watoto wanapoumwa hawajui waende wapi, wakienda hospitali kuchangia matibabu inakuwa shida. Kinamama wanapata tabu pia kuchangia matibabu kwa sababu hali zao duni.

Kwa hiyo, naomba wizara iangalie pia mama na watoto kitu muhimu sana katika jamii yetu kuwasaidia hasa wakiwa waja wazito. Kwa hivyo, wizara hii itie mkono wake kupitia Wizara ya Afya kwa mama na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, ukienda kama upande wa mama na watoto kwenye mahospitali yetu hushindwa wazee hawa kulipa gharama za matibabu hasa ukitizama baadhi ya matibabu wanakuwa wanashindwa hata kupata vipimo kama vile *X-Ray machine* na *MRI*, inakuwa tabu sana na uwezo wao ni mdogo ndio wanaishia kufa watoto au mama kwa kukosa matibabu mazuri katika hospitali zetu.

Mhe. Mweyekiti, nimalizie kwenye ukurasa wa 17 katika suala la wazee. Wazee wanapata tabu sana katika maisha yao ukilinganisha wazee na vijana wazee wapo kidogo sana kuliko vijana. Sasa Mhe. Waziri nafikiri aangalie sana pale familia zetu zinapoyumba kwa kweli wazee wanapata tabu, wanadhalilika wanashindwa hata kujishika hizi familia zetu.

Mhe. Mwenyekiti, maisha ya wazee yanakuwa ya shida, kipato chao cha tabu, japo serikali inasema ina nia njema kabisa kuwahudumia wazee hawa, lakini tiba zao pia inakuwa tabu. Wakienda hospitali kama nilivyosema *MRI, CT-Scan,* X-ray hawawezi kutibiwa hawa, wazee hawana fedha na vipimo hivyo inakuwa tabu kuvipata, kwa hiyo, mwisho wanaishia kufa tu. Naiomba wizara iwaangalie sana wazee hawa, watoto na kinamama kwa maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi kuna baadhi ya watoto wakishaona wazee wao watu wazima hawawezi kuwatunza wanawapeleka nyumba za wazee, utakuta wanasubiri mpaka yule mzee afariki, kwa kweli kitendo hiki mimi nakipiga vita na wizara vile vile ikipige vita sana. Kama watoto wana uwezo basi wakae na wazee wao wasiwapeleke pale Sebleni kumuacha na kumtupa mpaka siku ya kufa waje kumchukua. Kitu hicho kinanisikitisha sana, kwa sababu kama nilivyosema sisi sote tutakuwa wazee kesho na tutahitaji kuhudumiwa. Kwa hivyo, naomba hawa wanaofanya vitendo hivi sio kitu kizuri na naomba sana serikali iangalie suala hili ili waweze kuwaenzi vizuri wazee.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie suala la mwisho. Hawa wazee tumeambiwa wanapata chakula kizuri Mhe. Mwakilishi kasema hasa kule Welezo wanapata vyakula vizuri. Lakini mimi niseme Mhe. Mwenyekiti, hawa wazee wanataka kutembea pia, wanataka kwenda *day out,* wanataka na wao wapoteze mawazo. Mhe. Mwenyekiti, wamekaa pale wazee utawaonea huruma. Mimi naomba kwa kupitia sisi Wawakilishi na Wabunge. Mimi nasema mara nyingi hii, sisi tuna uwezo Wawakilishi na Wabunge, sio kama hatuna uwezo. Serikali yetu inatulipa kwa hiyo kuchangia fedha kuwapeleka hawa wazee wetu *day out* kutembea hatutoshindwa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hili suala la wazee ni muhimu, sote tunatoka kwenye njia hii tunakwenda kule kwenye wazee. Kwa hiyo tuangalie na sisi sote tutapita kwenye njia ile. Hawa wazee wanataka kutembea kuona maisha bora, wanataka kuona hali halisi, wanataka wapoteze mawazo yao. Kwa hiyo naomba Mhe. Mwenyekiti, hawa wafanywe kila mwezi wapate japo kwenda out kutembea wapate chakula chao wale. Mhe. Mwenyekiti, mara ya kwanza nitapeleka mimi gari kuwachukua wazee hawa kwenda kuwapeleka mashamba wanayotaka kwenda ili watembee. Na kama nitakuwa na uwezo Mhe. Mwenyekiti, basi mimi nitawachukua kila mwezi hawa wazee ili wakatembee. Lakini naomba kupitia na Wabunge na Wawakilishi sote tunalipwa na Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar tusaidie Serikali yetu kwa kuwasaidia wazee hawa. Huu mzigo kuiachia Serikali peke yake, Serikali haiwezi kuwalipa wazee au kuwawekea mambo mazuri ili wale wazee wafarajike mpaka unapokuwa mwisho wa maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa hayo naunga mkono hii hotuba ya Waziri asilimia mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala ambaye ametujaalia jioni hii tukaweza kukutana hapa. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia na mimi nafasi hii nizungumze machache.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuanza na mimi nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Waziri wa Wizara hii ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, pamoja na watendaji wake wote kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara hii inaongozwa na mama, na Katibu wetu Mkuu ni mama. Kwa hiyo wanawake tunasema tuna nafasi kubwa kabisa ya kukushukuruni na kukupongezeni kwa imani zenu kwa sababu ninachojua mama ni mtu ambaye ana imani sana, ana upendo sana kwa wale watoto wake anaowalea. Na sisi tunakubali kwamba unatulea katika misingi mizuri tunakushukuru na kukupongezeni sana.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi nianze mchango wangu katika Idara hii ya Uendeshaji na Uratibu wa Programu za Uwezeshaji. Mhe. Mwenyekiti, Idara hii inajitahidi kushughulikia wajasiriamali. Kwa kweli pamoja na jitihada kubwa za Wizara kuwapatia mafunzo mbali mbali, lakini bado wajasiriamali wanakabiliwa na changamoto kubwa za kukosa masoko na vifungashio vya bidhaa zao ambavyo jambo hili nyinyi wenyewe mmeliona. Vifungashio ambavyo vingezifanya bidhaa hizi zikawa katika viwango bora na kutangaza bidhaa zao. Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana Serikali kwa juhudi kubwa walizozifanya kwa kuwasomesha wajasiriamali, kwa kweli wajasiriamali wetu hivi sasa wameweza kuzalisha bidhaa zilizokuwa nzuri na bora.

Kwa hiyo niiombe Serikali bado iendeleze jitihada kila inapopata uwezo kuwaendeleza wajasiriamali hawa, ikijua Serikali katika kuwasaidia wajasiriamali basi inajipunguzia mzigo wa kuwaajiri vijana. Kwani vijana wengi ambao

wameweza kujiajiri wenyewe wanaonekana wana maendeleo na pia wanaweza kujikimu katika mahitaji yao. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri hawa ambao tayari wameshapiga hatua basi tusiwaache mkono tuwaendeleze ili vijana waweze kujiajiri wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kuna wanawake ambao wanajishughulisha na biashara mbali mbali katika kujikwamua na umaskini. Kuna wanawake wanajishughulisha na biashara ya samaki na tunawaona wanauza kila upande na kwa kweli wanajitahidi na kujikwamua. Kuna wanawake ambao wanashughulika na biashara za dagaa, hasa kwetu Kaskazini biashara hii ni kubwa sana. Kuna wanawake wanalima mwani.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri wanawake hawa kuwajali na kwa kuwasaidia kuwatafutia masoko ili bidhaa zao ziweze kupata soko waweze kupata mahitaji makubwa zaidi. Lakini pia kuwatafutia maeneo ambayo wataweza kukaa wanawake hawa na kufanya biashara zao bila ya wasiwasi, kwa sababu wanamofanya si mwahala mwa uhakika. Huwa wanakaa mara wanatimuliwa, inakuwa wanahangaika na biashara zao hapa na pale. Kwa hiyo Serikali izingatie kuwatafutia kinamama hawa maeneo ya kukaa na wakatulia wakafanya biashara zao kwa utulivu, maana yake wanajipunguzia umaskini, wanawasaidia kinababa katika kuwasomesha watoto. Lakini kuna wanawake wameweza kujenga nyumba za kisasa kwa biashara zao hizi hizi. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, si busara wanawake hawa tukawaacha tu, ni lazima tuwatafutie ndege ya kuwaongoza ili waweze kujikimu katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, pia wanawake wale ambao wanashughulika na ufugaji. Mhe. Mwenyekiti, mmeeleza hapa kama wafugaji hawa pia wana changamoto ya upatikanaji wa mashine ya kutotolea vifaranga. Lakini pia mkaeleza kama mashine hii ya kutotolea mayai inayotengenezwa kwa kutumia teknolojia rahisi na rasilimali zilizopo nchini. Mhe. Mwenyekiti, mimi nimuombe Mhe. Waziri kufanya busara zake wakaweza kupata mashine hii ili wafugaji hawa wakiwemo wanawake na vijana wetu wa kiume wakaweza kupata mashine na wakaweza kuzalisha vifaranga kwa wingi wakajizalishia mali.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, mimi niipongeze sana Serikali kwa kuwaunganisha vijana hawa. Idara hii imeweza kuwaunganisha vijana wa Visiwani hapa, lakini na vijana wa Tanzania Bara. Vijana hawa katika kuunganishwa kwao, Idara hii imewahamasisha vijana juu ya uzalendo wa kuipenda nchi yao. Mhe. Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kuipongeza sana Wizara kwani vijana ndio ambao tunawategemea, vijana ndio warithi wa nchi hii, lazima vijana wawe na upendo wa nchi yao, waweze kukaa na kubadilishana changamoto juu ya matatizo wanayoyapata.

Mhe. Mwenyekiti, niombe katika hili pia msisahau kuwafundisha vijana historia ya nchi yao. Mhe. Waziri vijana muwafundishe historia ya nchi yao ndipo huo uzalendo utakapojengeka zaidi. Kwa sababu vijana wanaonekana historia ya nchi yao hawaijui na ndio maana ukaona wanayumbayumba. Mhe. Mwenyekiti, historia ni kitu muhimu, asiyeijua historia ya nchi yake ni sawa na mtumwa. Naomba sana jambo hili muweze kuwasaidia vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ustawi wa jamii. Wenzangu wengi waliotangulia kuchangia wameeleza kuimarisha uhifadhi wa wazee wetu. Mhe. Mwenyekiti, jambo hili ni zuri na kwa kweli pia nichukue fursa hii kuipongeza Wizara kwa sababu juhudi mnafanya, si kama hamfanyi. Mnajitahidi kwa sababu majumba yale yalikuwa mengine mabovu lakini Wizara imechukua juhudi ya kuweza kuzitengeneza ili wazee wetu waweze kukaa mahala pazuri.

Mhe. Waziri umekuwa ukiwatembelea wazee mara kwa mara kujua changamoto zao. Tunakupongeza sana na kwa kweli mimi niungane na wenzangu tu kusema wazee wetu hawa ni watu ambao wametutoa mbali. Sisi tumerithi kutoka kwao kwa hiyo ni vizuri tukawaenzi hasa tukizingatia kuwaongezea lile posho kama ni dogo ili na wao waweze kujisikia.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye udhalilishaji wa watoto. Wenzangu wengi wamesema kuhusu suala hili, lakini kusema kweli linatusononesha na linatuumisha matumbo sote tukiwa wazazi. Mhe. Mwenyekiti, vitendo vya udhalilishaji kwa kweli vimekuwa vikitusononesha baada ya kuona vinazidi siku hadi siku badala ya kupungua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi niiombe tu Serikali kwa kuwa kuna kinga ambayo inawafanya watu labda waone huko ndio kwenye kivuli cha kujificha kwamba hakuna kile chombo cha *DNA*. Kwa hiyo Serikali lazima tujitahidi chombo hiki tukipate lakini na sisi kama wazazi kwa upande wetu jamii tuweze kukaa pamoja katika vikao katika vijiji vyetu, katika shehia zetu kuliona suala hili kama ni tatizo na tusiliachie Serikali peke yake. Lazima tuone sasa hii ni changamoto ya kitaifa na tunaikalia kitako kwa pamoja kuweza kutatua changamoto hii ambayo imetukabili.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Mikopo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka hapa nimuulize Mhe. Waziri katika mikopo hii ambayo mumeanza kutoa nilitaka kujua tu kama mumezingatia utoaji huu wa mikopo kuwapatia wale ambao wao hawajawahi kupata, kuliko tukarejea kwa wale ambao tayari wao wameshapata mara kwa mara itakuwa wale wanaokosa hatujawatendea jambo la haki. Nilitaka kujua kama jambo hili mlilizingatia katika utoaji wenu wa mikopo ili waweze kufaidika na wale wengine ambao hawajaweza kupata mikopo hiyo.

Jengine niungane na Mhe. Salim Abdalla Hamad pale aliposema vikundi vidogo wamepata pesa nyingi lakini vikundi vingi wamepata pesa kidogo. Mhe. Mwenyekiti, na mimi hili nilitaka kujua ufafanuzi wake kwa sababu inaonekana kuna vikundi vipo vichache lakini wamepata fedha nyingi, lakini kuna vikundi vipo vingi wamepata fedha kidogo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi mchango wangu haukuwa mkubwa sana lakini pia nimuombe Mhe. Waziri vikundi vinalia wivu. Kuna vikundi umekuwa unavitembelea lakini wivu wanaolia ni wa maendeleo. Kwa hiyo wale ambao wao hujawahi kuwatembelea na wao wanaomba uwatembelee ili wajisikie kuwa na Waziri wao wakipata nasaha kutoka kwako.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache mimi naunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja. Namtakia kila la kheri ili aweze kufanikiwa katika bajeti yake hii tukijua wanawake tutafaidika na tutakuwa na maisha mazuri. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, awali yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi za kufika mpaka muda huu Alhamdulillah tupo katika afya njema.
Mhe. Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii vile vile kuishukuru Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Waziri na Mwenyekiti wake aliyekuja.

Mhe. Mwenyekiti, kutokana na hasa mwezi huu wa Shaaban na vitu vilivyokuwemo humu ndani katika ukurasa wa 78 labda nianze kwa *Inna Lillah Wa Inna Ilayhi Rajiun.* Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki kwa kweli kwa sisi kwa kwa utamaduni wa Zanzibar kuandikiwa ripoti suala la ubakaji, jinsia na mambo ambayo ni tabu sana kwa sisi Wazanzibari kuzungumza jambo kama hili, leo kinakuja kitabu vinakuja vitu hivi vilivyokuwa vimejitokeza katika karne hii hapa Zanzibar. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, kwa nini nikasema *Inna Lillah Wa Inna Ilayhi Rajiun.* Nataka nitoe mfano uliokuwa hai.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja Mtume wetu Muhammad (SAW) alikaa na masahaba wenzake, sasa palikuwa na kibatari ukaja upepo kikazimika kukawa kiza. Basi Mtume wetu Muhammad (SAW) akasema *Inna Lillah Wa Inna Ilayhi Rajiun.* Masahaba wake walivyokaa pale wakamuuliza *Ya Rasulallah* hebu tuambie ni kitu gani ambacho kilichokuwa kikubwa ukakisema kitu hiki ambacho kilichofanyika. Akasema naam! Nafikiri hata humu ndani tuliokuwepo tumekaa zikizimika taa tutakuwa tunahuzunika kidogo.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki kwa kweli kwa sisi khulka yetu ya Wazanzibari na wakati kama huu kuandikiwa vitu kama hivi halafu tukavitazama tukaja tukasoma. Mimi Mhe. Mwenyekiti, nasema namheshimu sana mama yangu Mhe. Waziri, lakini naheshimu na bajeti. Mhe. Mwenyekiti, vitu hivi lazima vipate jawabu, na jawabu zake zitakuwa ni ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja kulikuwa na jeshi la Bibi Aisha na huku kulikuwa na jeshi la Sayyidna Ally. Masahaba wakamuuliza Sayyidna Ally tuelekee wapi. Sayyidna Ally akajibu pale pale tafuteni haki iko wapi.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala la ubakaji na vitu ambavyo wala siwezi kuvizungumza sina utamaduni navyo kwa kitabu hichi lazima vipatiwe jawabu. Na jawabu si la Wizara wala si la Mhe. Waziri. Mhe. Waziri hakamati, Mhe. Waziri na watu wake hivi vitu vizito, na wanaoathirika ni watu ambao hawana sauti wazee wao maskini, uwezo wao ni mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, anapobakwa mtoto kwa rika zote yupo shamba maskini hawezi kula kwake muhogo, viazi na mashelisheli. Kesi imeletwa mjini kwa kweli inahuzunisha, achukue shilingi elfu sita aje nayo mjini. Aende pale kwenye Mahakama ya Wilaya, au ya Mkoa, akifika pale anaambiwa Jaji leo hajaja anaumwa, ni kazi ya Mwenyezi Mungu. Shilingi elfu sita ameshazitoa halafu unamwambia baada ya wiki mbili arejee tena.

Mhe. Mwenyekiti, hivi vitu tusivifanyie mchezo, na wanaoathirika ni watu ambao maskini. Tungelikuwa humu ndani mmoja angeliathirika angeua, lakini leo kwa sababu mtu hana uwezo, hana pa kusemea anapata vitu kama hivi tumekaa. Sasa mimi nafikiri kuwepo na *task force* maalum ya vitu kama hivi na mambo mengine.

Mimi nakumbuka mwaka jana Mhe. Mgeni Hassan Juma alileta hoja binafsi hapa kwenye Baraza hili. Mhe. Mwenyekiti, hivi vitu vitaendelea na vitaendelea Mungu atunusuru kwa sababu tunaviacha, tunavitazama na wala hatuvishughulikii. Kwa sababu haya mambo yanataka mashirikiano ya pamoja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, mimi ningelishauri hili suala la jinsia hali halisi ilivyo ningemuomba Mhe. Waziri namheshimu sana aunde kamati ndogo ambayo itakuwa na uwezo wa mfuko maalum na itushirikishe na sisi. Mimi nipo tayari naomba kazi hiyo katika kamati itakayoundwa. Halafu tuone hawa watu wanaofanya mambo kama haya wataiona *June July*. Lakini vitu vipo, tunafanya kama jambo la kawaida na wanaofanya ni watu, kwa mfano juzi Mhe. Mwenyekiti, kuna familia moja ya Mkoa wa Kusini Unguja. Kuna askari pale alimlawiti mtoto. Wale wazee kwa maelekezo wakenda kwa Waziri wa Katiba na Sheria Alhajji huyo hapo mzee wangu, baba yangu Mhe. Abubakar Khamis Bakary.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary kamuandikia barua kamanda wa Mkoa wa Kusini Unguja, sio Pemba. Bwana njoo kuna suala hili njoo tuzungumze. Hatua aliyoifanya, Jaji Msomali, Mtuhumiwa Msomali, mtoa hukumu Msomali. Kamuandikia barua Kamishna aliyepita wa Polisi wa Zanzibar, kamuandikia Mhe. Abubakar Khamis Bakary akamuambia wewe CUF, huna uwezo wa kumuita huyu kamanda. Haya niambie haki itapatikana wapi. Mtoto wa Mkoa wa Kusini Unguja. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lazima tuwe wakweli. Kilichobakia hapa tunakuja tunapitisha bajeti lakini kila mmoja atabeba jukumu kwa Mwenyezi Mungu, *inshaallah*. Kuna vitu hatuwezi kuendelea navyo kwa utamaduni huu, kila mtu anaona yeye mbabe, kila mtu anajiona ana nguvu. Yule pale Mhe. Abubakar Khamis Bakary. Sasa kuna vitu hivi Mhe. Mwenyekiti, tunavielea tunaviacha na hawa watoto wataendelea kupata mateso kama haya, hawana sauti. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye suala la ajira. Suala hili vile vile ambaye hana sauti ndani ya serikali, hana sauti ndani ya jamii, mtu mzima kamsomesha mtoto wake kwa kuuza kuni, muhogo, shelisheli. Leo mtoto wake kapasi hapati ajira kwa sababu hana mtu ndani ya serikali. Huo ndio ukweli Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*).

Mimi kwa sababu nina uwezo wa kuajiri, nitaanza kuchukua Mohammedraza Hassanali familia ya watoto wangu, shemegi yangu, ndugu yangu, hiyo ndio iliyokuwepo. Sasa nikitaka kumuomba Mhe. Waziri ninamuheshimu sana *wallahi laadhim*, ninamuheshimu sana huyu mama kwa sababu amenielewa na nimefanya naye kazi. Hivi vitu hivi lazima avitizame atake msaada kwetu sisi, atake mashirikiano kwa watoto wake, kwa wajuu zake. Lakini leo ajira inatoka kwa upendeleo, ajira inatoka kwa umimi umimi.

Hatuwezi kufika tutawasomesha watoto wetu watamaliza ajira hizi zitaendelea ndani ya serikali kwenda na upendeleo. Huu ndio ukweli na mimi ninao ushahidi wote, hatuwezi kufika. Tumekuja hapa Mhe. Mwenyekiti, kuwatumikia wananchi, hiki kiti ninachokizungusha si changu, ni cha Uzini na nitaondoka hapa. (*Makofi*).

Lazima tujijue jamani tusikimbilie tu tukafika hapa saa hizi kila mmoja kakimbilia kusali, kila mmoja kakimbilia kufunga mwezi wa Ramadhani, hizi ni sawabu zetu. Lakini vile vile tuwe nafsi zetu Mhe. Mwenyekiti, tusiwe na upendeleo. Lakini unafika unazungumza na mwenzako juu ananiambia, hivyo hatuwezi. Tumekuja hapa tunazungumza maslahi ya nchi, maslahi ya kutupeleka mbele.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tumetoka huko. Kwanza Mhe. Mwenyekiti, hili suala la ajira Mhe. Waziri ninamuomba sana alitizame na kulipatia ufumbuzi. Kuna wazee Unguja na Pemba, vijijini watoto wao wamesoma hawana ajira. Ajira ikitoka watu wameshaambizana kila mmoja ameshapeleka majina kumi. Unaambiwa uje wilayani, mkoa, ukoo wao tu wanaingiza. Mimi nina mfano wa Uzini pale. Wamenijia wazee watoto hawana uwezo lakini ikitoka kila mmoja kishakumbatia, wewe afisa tia watu wako kumi. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, haya mambo *we are only in transit* hapa tulipo. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ningelimuomba Mhe. Waziri huu mzigo aliwokuwa nao ni mkubwa, Mwenyezi Mungu atamsaidia. Lakini ninataka tuwe naye, tufanye naye kazi, tumsaidie, tumpe hekima pamoja na wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa yako suala la uwezeshaji; ninakuja tena. Hili suala la ajira Mhe. Mwenyekiti, mimi nilimwambia wakati ule si kwa sababu ya sifa, kwa kupenda nchi yangu na Mwenyezi Mungu kanijaalia. Nilimpa *offer* Mhe. Nassor Mazrui Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ya kuwasaidia wananchi, milioni mia mbili bila ya riba, bila ya mkopo. (*Makofi*).

Kuna vitu vyengine nimevifanya Mwenyezi Mungu anajua Mhe. Mwenyekiti, na ninaendelea kufanya. Suala hili la ajira na kuwasaidia wakulima na maskini, lakini hili langu mimi na Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hili suala la wazee vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, suala la wazee linahitajika kutizamwa kwa urefu kabisa. Tunao wazee wetu wamestaafu sehemu mbali mbali. Wazee waliostaafu zamani ambao walikuwa vile vile katika taasisi zetu za serikali, hata hizo posho wanazozipata ni ndogo hazitoshi. Lakini kuna haja Mhe. Mwenyekiti, kwamba vitu tuvitazame kusaidiana, tukapata muafaka wa mambo haya. Tutakuwa wazee tunawaumiza sana na hasa suala la hali ya maisha ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, unaposema ajira. Unampa ajira mtu katika sehemu zetu za serikali, laki moja, laki moja na nusu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, leo dola moja elfu moja mia saba. Kwa hivyo kile ambacho walichokuwa wanakipata ukimwambia mshahara wake hata ukimzidishia elfu ishirini bado mazingira yake yapo pale pale. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ninafikiri katika hili suala la uwezeshaji vile vile, ninafikiri Waziri mama yangu pamoja na watendaji wake wakatizama namna gani ya kuweza kusaidia suala la uwezeshaji kuhusiana na suala hili la mikopo. Mikopo kuna sehemu nyingi sana Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile tuwe waangalifu.

Mimi ninakumbuka leo ninataka kusema suala hili la fedha ya uwezeshaji ambazo zilizochangwa. Tusije tukafanya kosa. Zile fedha ambazo za JK na AK. Ninakumbuka kaka yangu Mhe. Haroun Ali Suleiman aliwahi kutamka na gazeti hili ninalo, akasema pesa hizi zilikusudiwa ziwasaidie wananchi waliokuwa hali zao ndogo. Matokeo yake, Waziri kwa matamshi yake, alisema hizi zilitolewa mikopo hazikusimamiwa, matokeo yake waliokopa wamekwenda kumaliza gari zao na walikwenda kuongeza mke. Kwa hivyo yale matumaini ya kuondosha umaskini hayakupatikana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, sasa nilitaka kumshauri, wizara hii tuwe waangalifu sana katika kutoa mikopo. Kuna watu kweli mimi ninaweza nikawasaidia. Watu kweli wana hamu suala hili la kuwasaidia lakini mutizame kwa kina ili tuone kwamba wananchi wetu wa visiwa vya Unguja na Pemba wanakuwa na imani. Kwa sababu Wazanzibari mpaka ndugu zetu wa Bara Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri katika pesa ambazo wananchi waliotoa wafanyabiashara ilipindukia bilioni kwa lengo tu la kuwakopesha watu wetu, wapate kazi na hilo ndilo ilikuwa lengo la Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Alipoona Mhe. Rais kuna tatizo la ajira, kuna tatizo la zana za kufanyia kazi Mhe. Rais aliunda kamati kwa nia moja tu kuondosha umaskini na kuwapatia wananchi.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ninajua bado nina dakika 5 mimi kama sikosei.

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika 3.

Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali: Naam tatu! Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Mimi Mhe. Mwenyekiti, katika kumalizia kwamba vitu hivi vinataka nia. Lakini kwa kumalizia mimi sina tatizo na wizara hii. Ninaiunga mkono kwa asilimia mia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini kabisa, wala sitosimama hata siku moja. (*Makofi*).

Nasisistiza kwamba vitu hivi fimbo ya Mungu haina sauti, kila atakayefanya atachukua jukumu yeye kwa Mwenyezi Mungu. Ninaiunga mkono bajeti ya wizara hii, ninamuunga mkono Waziri wangu na watendaji wake lakini ninataka kumwambia tu kwamba hili suala ni zito, ana jukumu kubwa kwa Mwenyezi Mungu na Mtume wake Muhammad (*SAW*).

Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana na mtu wa mwisho kabisa kwa siku ya leo ni Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa na kama kuna mjumbe yeyote ambaye anataka kuchangia, naomba achangie kwa maandishi. Kwa sababu asubuhi tunafanya majumuisho kwa ajili ya bajeti hii. Ahsante Mhe. Mwanaidi tuendelee.

Mhe. Mwanaid Kassim Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii na mimi nikaweza kuchangia hotuba hii.

Nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuwasilishia hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Pia niwapongeze watendaji wote wa wizara hii jinsi wanavyofanya kazi zao vizuri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Idara ya Ushirika. Mhe. Mwenyekiti, niipongeze idara hii kwa kufanya kazi zake vizuri hasa kutoa mafunzo kwa vikundi vya *SACCOS* pamoja na vyama vya uzalishaji na utoaji huduma. Mhe. Mwenyekiti, wizara hii inajitahidi, inafanya kazi vizuri, inatoa mafunzo yake vizuri kwa sababu kama mimi ni mjumbe katika kamati hii, tuliwahi kwenda kuangalia *SACCOS* mbali mbali na kweli kazi zao ni nzuri wanastahili sifa.

Mhe. Mwenyekiti, ninataka niseme kwamba Idara hii ya Ushirika pale wanapofanyia kazi kusema kweli hawana ofisi. Ofisi yao kule viwanda vidogo vidogo walipokuwepo siku za mvua Mhe. Mwenyekiti, ofisi zao zote zinavuja. Ninaipongeza serikali kwa kuwapatia jengo lililokuwepo Migombani ingawaje sasa jengo lile kwa wao kama idara hawatokuwa na fedha za kulitengeneza. Kwa hivyo naiomba wizara kupitia Wizara ya Fedha iwasaidie fedha ili kuweza kulitengeneza lile jengo na waweze kuhamia katika jengo lao hilo.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Idara ya Ustawi wa Jamii. Mhe. Mwenyekiti, pia idara hii niipongeze kwa kazi nzuri wanazofanya. Mhe. Mwenyekiti, idara hii nianze kwa udhalilishaji wa kijinsia. Kusema kweli udhalilishaji wa kijinsia ni tatizo katika nchi yetu hii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kila tukenda masuala haya yanazidi kuendelea siku hadi siku na hukumu kama tulivyopewa katika kitabu hiki alichosoma Mhe. Waziri zinaenda kidogo kidogo. Lakini mimi ninataka niipongeze wizara hii kwa kusimamia vizuri kazi zake hasa kuweka vituo vya mkono kwa mkono.

Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli idara hii inajitahidi, tena inajitahidi sana kwa sababu vituo vya mkono kwa mkono, kuna watu wao pale kila wakati wakipokea taarifa wanajitahidi kupeleka mbele kunakohusika. Lakini zikifika katika maeneo ya Mahakama inakuwa wao ndio mwisho wao, hawawezi tena kuingilia. Hata hivyo wanajitahidi kwa nguvu zao zote, wanafuatilia taarifa, wanafuatilia kila kitu pamoja na madaktari katika vituo vyao walivyokuwa wameviweka.

Mimi niwapongeze pia kumaliza kile kituo Pemba cha mkono kwa mkono katika Hospitali ya Wete. Kituo kile nacho kimemaliza, Chake-Chake pia kipo. Kwa hivyo idara hii imechukua hatua kubwa kwa kufanikisha vituo hivyo na kazi wanafanya kwa hali na mali. Tatizo ni Mahakama na Polisi. (*Makofi*)

Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, akae na Waziri wa Katiba na Sheria kuona haya matatizo yanafikia mwisho. Kwa sababu kila siku tukiangalia, ukija kwenye redio kwenye kipindi cha mawio, tunasikia kabaka. Sasa tunaomba hebu wizara hizi mbili wakae pamoja ili tuone wanafanya nini ili tumalize hili tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, pia idara hii hii, niwapongeze kwa kuona wamesimamia vizuri nyumba za wazee na wazee wetu sasa hivi wanaishi katika mahali pazuri. Mhe. Mwenyekiti, tuseme ukweli nyumba zile zimepatiwa matengenezo mazuri na zipo vizuri. Kusema kweli wanastahili sifa Mhe. Waziri na watendaji wake wote wanastahili sifa, majengo yetu mazuri. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, pia niende katika Hospitali ya Welezo ya wazee. Mhe. Mwenyekiti, katika Hospitali ya Welezo kusema kweli kule wizara inajitahidi kwa kadri ya uwezo wake. Wazee wetu kule wanatunzwa vizuri. Sisi wenyewe kama kamati tumekwenda na tumeona na tumeridhika na kazi wanazozifanya. Lakini tatizo lililokuwepo pale kwamba wafanyakazi waliokuwepo pale kutoka Ustawi wa Jamii ni kidogo, kwa hivyo walikuwa wanaomba wapewe nafasi ili waajiriwe wengine. Kwa sababu pale pana kazi, wazee wale hawajiwezi, hivyo wafanyakazi waliokuwepo pale ni kidogo hawatoshi. Kwa hivyo ninamuomba Mhe. Waziri kuliangalia hili ili kuongeza pale wafanyakazi.

Pia nikiendelea, naomba nimuulize Mhe. Waziri kuhusu kusimamia ulipaji wa fidia kwa wafanyakazi waliopata ajali kazini. Mimi kwanza ninataka niipongeze wizara kwa kazi nzuri waliokuwa wamefikia; kukaa pamoja na Wizara ya Fedha kuona wanalitatua tatizo hili la fidia. Kusema kweli Mhe. Mwenyekiti, wizara imefikia hatua nzuri na wao wamejitahidi. Lakini nilikuwa ninataka nimuombe atakapokuja kuleta majibu aniambie wamefikia hatua gani kwa Wizara ya Fedha kuona wanalimaliza tatizo hili la fidia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nije Idara ya Maendeleo ya Vijana. Mhe. Mwenyekiti, pia niwapongeze idara hii kwa kazi nzuri waliyokuwa wanafanya kama vile tulivyopata taarifa katika kitabu hiki kuanzisha kilimo cha *Aloevera* na mboga mboga kwa vijana wa Tunguu. Mhe. Mwenyekiti, kusema kweli idara hii kwa vijana hawa wamejitahidi sana. Nako kama kamati tulifika na tumekwenda kuona jitihada zao wanazofanya.

Ninamuomba Mhe. Waziri ajitahidi kuzungumza na watu wa Wizara ya Kilimo ili vijana wetu hawa wazidi kupata elimu na wao wapate vijana wengine wawafunze. Mimi ninawapongeza tu kwa kazi yao wanayofanya na pia kuhamasisha vijana Zanzibar nzima kuona wanakwenda pale Tunguu na wao wakapate mafunzo ya kulima *Aloevera* na mboga mboga.

Mhe. Mwenyekiti, niende hapo hapo idara hii kuhusu masuala ya mwenge. Mimi Mhe. Mwenyekiti, ninawapongeza sana kwa kusimamia masuala haya ya mwenge kwa sababu michango inayopatikana inasaidia katika maendeleo ya majimbo yetu. Kwa hivyo ninawapongeza sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Mkoa wa Mjini/Magharibi, wanawake tunaunga mkono asilimia mia juu ya mia. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nichukue fursa hii kuwashukuru sana kutokana na mashirikiano ambayo mumenipatia tokea wakati wa asubuhi mpaka sasa hivi tunamaliza shughuli zetu. Kwa ajili ya kuweza kumpa nafasi Mhe. Waziri ili akakae na watendaji wake na kuhakikisha anatuletea majibu ambayo ni mazuri na yenye kutosheleza na kuwezesha bajeti hii kuweza kupita.

Kuna jambo ambalo Waheshimiwa Wajumbe ninaomba kuwaomba wote kwa ujumla wenu. Waheshimiwa Wajumbe kesho tunataka kufanya majumuisho ya wizara hii asubuhi, lakini pia tunataka kufanya majumuisho ya Wizara ya Afya jioni.

Mahudhurio yetu hayaridhishi kuweza kukamilisha kazi kama hiyo wakati wa kesho. Kwa hivyo niwaombe sana Waheshimiwa Wajumbe zile dharura zetu tuzipunguze kwa siku ya kesho ili hizi kazi mbili muhimu tuweze kuzimaliza na tuweze kujipangia utaratibu wa shughuli zetu nyengine.

Baada ya maelekezo sasa, ninawashukuru tena kwa mara nyengine na ninachukua fursa hii kuakhirisha kikao hichi hadi kesho siku ya Jumanne saa tatu barabara za asubuhi ya tarehe 20/06/2014.

Naomba kuakhirisha.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 10/06/2014 saa 3:00 asubuhi)